**22 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 22 Juni, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 694

### Kuipandisha hadhi barabara ya Mjele – Ikuwa – Mlima Njiwa kuwa ya Mkoa

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi barabara ya Mjele – Ikuwa hadi Mlima Njiwa kuwa ya Mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mbeya kupitia kikao chake cha tarehe 9 Januari, 2023 kilitoa mapendekezo ya kuipandisha hadhi Barabara ya Mjele – Ikuwa hadi Mlima Njiwa kuwa ya Mkoa. Baada ya mapendekezo hayo kuwasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, tarehe 24 Februari, 2023, Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara Katika Hadhi Stahiki *(NRCC)* ilitembelea barabara zilizoombwa kupandishwa hadhi Mkoani Mbeya ikiwemo Barabara ya Mjele – Ikuwa hadi Mlima Njiwa.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati yamewasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na yanachambuliwa na uchambuzi ukikamilika taarifa itatolewa. Endapo barabara hiyo itakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi, itakuwa barabara ya mkoa na itahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naishukuru Serikali vilevile kwa vile Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi amesharidhia hii barabara sasa hivi kuhudumiwa na *TANROADS,* lakini iko kwenye hali mbaya sana. Sasa je, ni lini barabara hii itaanza ujenzi ili irekebishwe kuanzia Mjele, Ikukwa na siyo Ikuwa mpaka Mlima Njiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika hali hiyo ya barabara, barabara ya Haporoto – Ileya – Ishinda ambayo inahudumia wachimbaji wa Migodi ya Ileya na Ishinda, ni lini barabara hii

itapata matengenezo kwa vile nayo iko kwenye hali mbaya sana? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani swali swali la nyongeza la kwanza linabidi lijibiwe na Ujenzi na uchukuzi. Mheshimiwa Naibu Waziri umelisikia swali hilo? Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema, baada ya kupandishwa hadhi hiyo barabara, *TANROADS* itaanza utekelezaji kwa bajeti ambayo tunaanza kuitekeleza kwa 2023/2024. Kwa hiyo kwa sasa wenzetu wa *TARURA* baada ya Juni watatukabidhi na sisi tutaanza utekelezaji huo kwa bajeti mpya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa kuongezea tu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, barabara hii wakati bado ipo kwa *TARURA* ilikuwa imetengewa shilingi milioni 500 na *Road Board* kwa ajili ya matengenezo yake. Sasa baada ya kupandishwa hadhi fedha ile itahamia kwa wenzetu wa *TANROADS* ambapo bado watatekeleza kwenye barabara hii hii shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili ya Barabara ya Haporoto – Ileya – Ishinda. Barabara hii ina urefu wa kilometa tisa na kweli nikiri kwamba kwa sasa hali yake si nzuri sana. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 ambao tunauanza mwezi unaofuata, tayari barabara hii imetengewa shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuweza kutengeneza yale maeneo korofi kwa kumwaga changarawe na kuhakikisha kwamba inapitika vizuri, kwa sababu inaelekea katika eneo ambalo lina machimbo. Kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Njeza, kwamba muda si mrefu

ataona utekelezaji wa matengenezo ya barabara hii kwa hizi kilometa tisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nijue tu Serikali ina mpango gani sasa kupandisha hadhi Barabara ya Bukama, Barabara ya Kinesi – Ruhu na Barabara ya Nyamagugu – Kirogo kuwa na hadhi ya mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, hiyo ni barabara moja au ni tatu? Ni barabara moja au ni barabara tatu tofauti?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, barabara tatu ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa ni barabara tatu tofauti?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa, uliza moja kati ya hizo. Kwa sababu ni swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nataka nijue Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi Barabara ya Bukama - Nyamagaro mpaka Kiangasaga kuwa hadhi ya barabara ya Mkoa?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, Kifungu cha 11 na Kanuni za Usimamizi wa Barabara ya mwaka 2009 imeelezea wazi namna ya kuomba kupandisha hadhi barabara. Inatakiwa waanze kukaa vikao vyao

kule na kupendekeza kwa Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa, Mkoa wao wa Mara. Wakishapendekeza pale, baada ya hapo wanawasilisha maombi yale kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi mwenye dhamana ya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Barabara ya Kibaoni – Endabash itapandisha kuwa hadhi ya Mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoka kusema hapo awali, kwa mujibu wa Sheria ile ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, kifungu cha 11 na Kanuni za Usimamizi wa Barabara ya Mwaka 2009, zinaelezea ule utaratibu, inatakiwa mchakato uanze kwao wenyewe kwa kupendekeza barabara hiyo kupandishwa hadhi kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa, kisha aandikiwe Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi mwenye dhamana ya barabara na atume timu kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa barabara hiyo, ndipo barabara hiyo iweze kupendekezwa na kufikiriwa kupandishwa hadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 695

**Hitaji la ukarabati Kituo cha Afya Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati katika Kituo cha Afya cha Nanyumbu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na uchambuzi na mapitio ya vituo chakavu vinavyohitaji ukarabati katika ngazi ya afya ya msingi ili bajeti ya Serikali ikiruhusu vituo hivyo chakavu viweze kufanyiwa ukarabati kikiwepo Kituo cha Afya cha Nanyumbu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY Y. MHATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu haya ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kituo hiki ninachokieleza ni cha muda mrefu sana. Cha kushangaza kituo hiki kililetewa vifaa, vifaa tiba, vyote vya kituo cha afya ambapo kituo cha afya hakijajengwa. Sasa nauliza vile vifaa walivyovileta walikuwa na malengo gani, yaani vitumike wapi wakati kituo hakijafanyiwa ukarabati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; vifaa vile sasa hivi vimepelekwa katika sehemu nyingine je, Waziri anawahakikishia vipi wananchi wa ile Tarafa kwamba endapo watafanya ukarabati vifaa vile vitarejeshwa pale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu hiki kituo cha muda mrefu ambacho kimepelekewa vifaatiba, ni wao wenyewe kama halmashauri ambao wanapanga vifaatiba viende kwenye kituo

gani cha afya. Kwa hiyo ina maana wao walifanya maamuzi ya kupeleka vifaatiba hivi vipya katika kituo ambacho ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nanyumbu kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kukarabati Kituo hiki cha Afya kongwe cha Nanyumbu wakati bado tunatafuta fedha. Nitakaa na Mheshimiwa Mhata kuona ni namna gani tunaweza tukapata fedha ya kupeleka kukarabati kituo hiki cha afya.

Mheshuimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la vifaa hivi tiba ambavyo vimehamishwa kwenda kwenye Kituo cha Afya cha Tarafa nyingine na kuhama hapa Nanyumbu. Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga bajeti ya bilioni 112 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Ni jitihada kubwa ya mama yetu Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba tunapata vifaatiba kuanzia ngazi ya zahanati mpaka vituo vya afya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mhata kwamba tutapeleka tena vifaatiba vingine katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Kituo cha Afya Tandale katika Wilaya ya Kinondoni ili kipate Jengo la Mama na Mtoto na hasa ukiangalia idadi ya watu wanaoishi katika Kata ya Tandale ni wengi sana? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutatuma timu katika kituo hiki cha afya ambacho amekitaja Mheshimiwa Kisangi kufanya tathmini na kuona ukubwa wa eneo uliopo na kama linaweza likahimili kupata majengo mengine. Baada ya tathmini hiyo kufanyika itawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya kukipanua kituo hiki cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 696

**Hitaji la ukarabati barabara ya Mbinga - Kikolo hadi Kihungu, Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha changarawe barabara ya Mbinga, Kikolo hadi Kihungu ili iweze kupitika wakati wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanyia matengenezo Barabara ya Mbinga – Kikolo - Kihungu yenye urefu wa kilometa 36 ambapo katika mwaka wa fedha wa 2021, barabara hii ilifanyiwa matengenezo sehemu korofi kwa gharama ya shillingi milioni 150. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, barabara hii imechongwa kwa urefu wa kilometa 30 na kuwekewa changarawe kilometa 14 kwa gharama ya shilingi milioni 247.12.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, lakini pia niishukuru Serikali kwa kuendelea kufanya ukarabati wa barabara hiyo mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Naibu Waziri kwamba ni kilometa 14 tu za barabara hizo zimewekwa changarawe na maeneo ya Mbinga ni maeneo ya mteremko na milima, naomba kujua sasa Serikali ina mpango gani wa kuendelea kuweka changarawe katika kilometa zilizobaki pamoja na kuhakikisha kwamba mitaro imetengenezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya kutoka Mbinga – Kitanda – Miembeni – Lupilo – Mpepai na Mtua iliharibika sana hasa katika kipindi cha mvua, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, hii barabara ambayo ni *Kitanda Road* yenye urefu jumla ya kilometa 32. Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kilometa sita kwa kiwango cha kifusi. Kama nilivyosema awali tayari ilikuwa imeshatengenezwa kilometa 14 na katika mwaka wa fedha unaofuata Serikali itatengeneza kilometa sita na kuweka mifereji katika maeneo ambayo huwa maji yanajaa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la barabara hii ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie kwamba katika mwaka wa fedha huu unaoanza 2023/2024, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuweka *concrete* (zege) katika yale maeneo korofi ya milimani kwa sababu jiografia ya kwa Mheshimiwa Mbunda kule ni ya vilima vingi. Kwa hiyo tutaweka *concrete* katika maeneo korofi na vilevile nimpe taarifa tu Mheshimiwa Mbunda kwamba ana Barabara hii ya Utili – Mahande ambayo ina kilometa 14 inaenda kuwekewa lami

kama ambavyo aliomba yeye kwenye Mradi ule wa *Agri–connect*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 697

**Uhitaji wa gari la wagonjwa Kituo cha Afya Mlola – Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mlola Wilayani Lushoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji ya kuwa na magari ya wagonjwa kwenye Vituo vya Afya na Hospitali ili kurahisisha huduma za rufaa kwa wagonjwa. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 35.1 kwa ajili ya ununuzi wa magari 316 ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, magari haya yameanza kupokelewa kwa awamu na yatagawiwa katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ambayo itapata magari mawili kwa ajili ya huduma za rufaa za wagonjwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ni lini itapeleka fedha kujenga Vituo vya Afya katika Kata ya Kwayi pamoja na Kata ya Makanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Kituo cha Afya Gare kimezungukwa na kata mbili ambazo hazina vituo vya afya. Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kupeleka gari la wagonjwa ili kurahisha huduma kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza hili kuhusu ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kwayi na Makanya, tutakaa na Mheshimiwa Shekilindi kuona katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Vituo vya Afya katika Halmashauri yao na tuhakikishe fedha hizi zinakwenda katika walau kituo cha afya kimojawapo, kwa sababu ni mpango wa Serikali wa kujenga vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati nchini kote ikiwemo Kwayi na Makanya.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la gari ya wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Gare. Mheshimiwa Mbunge ni shahidi kwamba muda siyo mrefu kituo hiki cha afya kimetoka kukamilika kwa maana kilipelekewa fedha na tayari kimeshakamilika. Sasa kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imenunua magari 316 kwa ajili ya kila Halmashauri kupata walau magari mawili ya wagonjwa. Sasa magari haya mawili yatayoelekea kule Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto waelekeze moja katika Kituo hiki cha Afya cha Gare. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umesema magari mawili kila Halmashauri, Halmashauri zingine ndogo sana kuzipelekea magari mawili (moja, moja) peleka kila mahali. Halafu yale yanayobaki tazameni yale Majimbo ambayo ni makubwa (Halmashauri ni kubwa sana) zipewe hata matatu, kwingine liende moja, ama mengine yanaweza kuwa madogo, lakini watu wanaohudumiwa ni wengi. Kwa hiyo hilo ni wazo kama nyinyi mmeamua mawili, mawili, kafanyeni hesabu vizuri maana kuna Halmashauri hapa ndogo kwa kweli, ndogo kwa maana eneo la jiografia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa magari ya wagonjwa yaliyoagizwa na Serikali yanakuja kwa awamu, je, Serikali haioni umuhimu kwa awamu ya kwanza kuanza na Hospitali ya Mji Handeni kwa sababu haina gari la wagonjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, magari haya yanakuja kwa awamu kama ambovyo nimesema awali na kila Halmashauri ilikuwa tumepanga kupeleka magari mawili na gari lingine la tatu kwa ajili ya *monitoring and evaluation* katika Halmashauri hizi.

Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri ambao umeutoa wa kuangalia Halmashauri zile ambazo zitakuwa zina eneo dogo lakini lile gari la *monitoring and evaluation,* bado litakwenda kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma za afya zinasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali la Mheshimiwa Kwagilwa, tutakaa naye na kuona katika awamu hii ya kwanza, Hospitali ya Mji pale Handeni inaweza kupata gari pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 698

**Soko la samaki Mbamba Bay kuanza kutumika**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza: -

Je, lini soko la samaki Mbamba Bay litaanza kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba *Bay* unafanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ulianza mwezi Mei 2021 na kukamilka mwezi Machi, 2022. Katika awamu ya kwanza Serikali ilijenga jengo kuu ambalo lina vizimba au meza za kuuzia samaki. Kwa sasa, Serikali inaanza awamu ya pili ya ujenzi wa soko hilo ambao unahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji safi, maji taka pamoja na choo. Aidha, zabuni ya ujenzi huo imeshatangazwa na kufunguliwa Tarehe 23 Mei, 2023. Kazi ya uchambuzi na tathmini ya nyaraka za zabuni inaendelea ili kumpata mzabuni wa kuanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua umuhimu wa soko hilo na litaanza kutumika tu mara tu baada ya ujenzi wa miundombinu hiyo kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wazee wa Wilaya ya Nyasa walipokutana tarehe 5 Machi, 2023, waliniagiza na walisema kwamba wanaona Wilaya ya Nyasa inadharaulika kwa sababu miradi yake inachelewa kupatikana na ikianza haiishi kwa wakati na hata kama ikionesha dalili ya kuisha haipewi vifaa vinavyotakiwa.

Je, Serikali haioni haya mawazo ya wazee wa Wilaya ya Nyasa yana ukweli kiasi fulani? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa pia kulikuwa kumejengwa karakana kwa ajili ya kutengeneza boti toka mwaka 2015 mpaka leo karakana hiyo haifanyi kazi iliyokusudiwa. Je, ni lini sasa na hiyo karakana itaweza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Jambo la kwanza nitambue maoni ya Mheshimiwa Mbunge ambayo yametolewa na wazee wake na nimhakikishie tu kwamba Serikali haidharau wananchi wa Nyasa wala wananchi katika maeneo yoyote yale. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo maana tumemuelezea kwanza katika jibu la msingi, kuhakikisha kwamba soko hilo linafunguliwa na ndiyo maana zabuni imeshafunguliwa. Tunamaliza tu mchakato atakwenda atajenga na baada ya kujenga tutalifungua soko hilo ili liweze kuhudumia wananchi wa Jimbo la Nyasa kupitia Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, suala la karakana na lenyewe basi tumelipokea, mimi mwenyewe binafsi nitafanya hiyo jitihada binafsi ya kuhakikisha inafunguliwa kwa wakati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ningependa kufahamu ni lini Serikali mtapeleka fedha kumalizia ujenzi wa soko la Samaki Kata ya Mkinga, toka mmeahidi mwaka jana hakuna kitu kinaendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunatambua kuhusu mahitaji ya Soko la Mkinga na tuliahidi katika bajeti. Changamoto ambayo ilikuwepo ni kwamba fedha zilikuwa hazijatoka lakini jambo hilo liko katika mpango na nafikiri Wizara ya Fedha itakapokuwa imeleta fedha kwa wakati huu, tutazileta kwa wakati na kuhakikisha soko hilo linajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibiu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Furaha Matondo.

Na. 699

**Kujenga kipande cha barabara Kisorya hadi Nansio**

**MHE. FURAHA N. MATONDO K.n.y. MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza: -

Je, lini kipande cha barabara cha Kisorya hadi Nansio kitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inajenga barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya – Nansio yenye urefu wa kilometa 121.9 kwa awamu. Ujenzi kwa kiwango cha lami awamu ya kwanza sehemu ya Bulamba – Kisorya kilometa 51 umekamilika. Kwa sehemu ya

Nyamuswa – Bunda – Bulamba kilometa 56.4 ujenzi umekamilika na upo kwenye kipindi cha matazamio huku Mkandarasi akimalizia kazi ndogo ndogo zilizobaki. Kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Kisorya hadi Nansio ambayo ina urefu wa kilometa 12.8 Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA M. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ukerewe ni kisiwa na kwenye bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga fedha ya kujenga barabara hiyo ya kutoka Kisorya kwenda Nansio. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Matondo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli dhamira ya Serikali ni kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba tayari tumeshajenga sehemu kubwa ya hiyo barabara. Hela iliyotengwa ilikuwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa daraja ambalo lina kilometa takribani moja, lakini kwa maombi ya wana Ukerewe na Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, wameomba badala ya kuanza daraja kwa kuwa tunavyo vivuko viwili vikubwa ambavyo vitaendela kufanya kazi na hasa baada ya kuongeza kivuko kipya ni bora tukajenga barabara ya lami kuanzia Lugenzi hadi Nansio na wakati Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anawasilisha bajeti alitoa *commitment* kwamba tutaanza kujenga mwaka ujao wa fedha barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia Nansio kuja Lugezi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyomngeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais mwaka

jana iliahidiwa kujengwa barabara kutoka Mafinga inayokwenda Madibila kupitia Sadani.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli swali hili limeulizwa jana na Mheshimiwa nakumbuka wa Mbarali na nilijibu kwamba tutaendelea kulitengeneza, lakini marekebisho tu ni kwamba, kama alivyosema wakati Mheshimiwa Rais ametembelea Mkoa wa Iringa, Wabunge wa Mkoa wa Iringa hasa Wilaya ya Mufindi waliomba barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami na Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na akatoa maelekezo na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi akiwepo, ameshatoa maelekezo, kwamba ile ahadi ya Rais ianze kutekelezwa mwaka huu. Kwa hiyo, tutaanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami kama maagizo ya Mheshimiwa Rais yalivyotolewa kuanzia huku Mafinga kwenda Mbarali, ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami kipande cha barabara kinachoanzia Ngarenanyuki hadi Oldonyo Sambu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja inachangiwa kipande na barabara yetu ya *TANROADS,* pia kuna kipande ambacho wenzetu wa *TARURA* wanakifanya. Kwa upande wetu wa *TANROADS* tayari tumeshafanya usanifu na tunachofanya

sasa hivi ni kuhakikisha kwamba hii barabara inapitika kwa muda wote wakati tukiendelea kutafuta fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Kokoto mpaka Mwandege ndiyo lango kuu la magari yanayotoka Kusini. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua barabara hiyo ili kupunguza msongamano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika bajeti ambayo tumeitenga mwaka ujao na kweli nakubaliana kuna changamoto kubwa sana. Pale ambapo *BRT II* inaishia mwaka ujao tunaanza kutekeleza mradi wa kujenga kilometa 3.8 kwa barabara hizo nne, lakini mpango ni kwenda mpaka Vikindu kwa ajili ya kujenga hizo barabara nne kupunguza changamoto ya msongamano wa hizo barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu Hamis Mwagao, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza na ni kwamba zimebakia siku nane leo kabla ya mwaka wa Serikali kuisha na Serikali ilikuwa imetueleza kwamba Sengerema tutafanya usanifu barabara ya Sengerema - Ngoma na Busisi - Ngoma kwa ajili ya lami kwenda Nyangh'wale na zimebakia siku nane hatujaona mkandarasi, Nini kauli ya Serikali Mheshimiwa Waziri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii kwa sababu

inaunganisha mikoa miwili wa Geita na Sengerema Mkoa wa Geita na Mkoa wa Mwanza sehemu kubwa inasimamiwa na Makao Makuu ya *TANROADS* ninataka nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Mhandisi Mshauri ameshapatikana kwa ajili ya kuanza kazi hii ya usanifu wa hii barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 700

**Kutatua changamoto ya upatikanaji wa mbolea**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto ya upatikanaji wa mbolea nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kushirikiana na sekta binafsi vikiwemo viwanda vya Minjingu *Mines and Fertilizer Limited* na *ITRACOM Fertilizers Limited* kuhakikisha uzalishaji na upatikanaji wa mbolea hapa nchini unaimarika na kupunguza utegemezi wa kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi. Kupitia mpango huo, uwekezaji unaofanywa na kiwanda cha *ITRACOM* unatarajiwa kufikia uzalishaji wa takribani tani 1,000,000 za mbolea ifikapo Desemba, 2024. Vilevile kiwanda cha mbolea cha Minjingu

kinafanya upanuzi ili kuongeza uwezo wa uzalishaji kutoka tani 100,000 hadi kufikia tani 300,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2023/2024 Serikali imepanga kuiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC)* kwa kuipatia mtaji wa takribani Shilingi Bilioni 40 utakao iwezesha kununua na kusambaza mbolea kwa wakulima. Serikali kwa kushirikiana na kampuni za mbolea na Vyama vya Ushirika imepanga kuongeza vituo vya mauzo ya mbolea nchini ili kuwezesha wakulima kupata mbolea kwa urahisi na kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsnate. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali langu la kwanza, mmesema Serikali imejipanga kuipa kampuni yetu ya *TFC* mtaji wa bilioni 40 na sasa hivi tumebakiwa na miezi mitatu tu tufike kwenye *high season* ya kuhitaji mbolea. Je, mtatumia muujiza gani kuhakikisha mmeagiza mbolea na mnaisambaza nchi nzima?

Swali langu la pili, ni kwa nini *CPB* hawataki kuwarudishia wakulima fedha, walizoahidi kuwapa mahindi wakati Serikali imezuia *CPB* isitoe mahindi, na fedha zao hamtaki kuwarudishia ni kwa nini na mnarudisha lini hizo fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nilitoa taarifa humu ndani Bungeni na naomba leo nirudie ya kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha ifikapo mwezi wa saba mbolea zote za kupandia na kukuzia ziwe zinapatikana kwa wakulima ili waanze msimu na mbolea zikiwemo.

Mheshimiwa Spika, nakata nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba *TFC* walianza maandalizi haya mapema na hivi sasa tuko katika hatua za mwisho kuanza kupokea shehena za meli ambazo tutashusha mzigo huo, pia tunayo mbolea ya kutosha kuanzia kwa wakulima katika msimu unaoanza hivi karibuni. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba jambo hilo litafanyika.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, nimesikia hoja yake ya *CPB* na wakulima, naomba nikae na Mheshimiwa Mbunge nipate hayo madai ya wakulima, mimi na *CPB* tutakaa tuone namna ya kuweza kutatua jambo hili, ili mwisho wa siku tuweze kuhakikisha kwamba wakulima wanapata haki yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na.701

**Kutumia TEHAMA kuboresha kilimo nchini**

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza: -

Je, kwa kiwango gani TEHAMA inatumika kuboresha sekta ya kilimo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ni mojawapo ya sekta zinazonufaika na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano hapa nchini. Kwa kutumia TEHAMA sekta ya kilimo imeboresha maeneo mbalimbali ya huduma zinazotolewa na Wizara kwa wakulima, wafanyabiashara na wadau mbalimbali

katika sekta na umma kwa ujumla. Baadhi ya huduma zilizoboreshwa kwa kutumia TEHAMA ni pamoja na kutoa huduma za ugani kwa wakulima, masoko ya mazao ya wakulima, kutoa mbolea ya ruzuku, kupata vibali ama leseni za kufanya biashara za mazao ya mimea na vyeti vya afya ya mimea kwa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; kwanza teknolojia hii ya habari na mawasiliano ina mchango mkubwa sana katika kuziba lile pengo la uhaba wa Maafisa Ugani wetu kwa muda mfupi na kwa eneo kubwa, sasa Wizara ina mpango gani sasa wa kuanzisha *Apps* au mifumo mbalimbali ya TEHAMA, ambayo mifumo hii itawasaidia wakulima wetu wadogo wadogo kupata taarifa kwa wakati na kwa usahihi?

Pili, Wizara sasa haioni kuna umuhimu wa kuyashawishi makampuni mbalimbali ya simu kutoa kifurushi maalum cha huduma za wakulima, ambapo sasa wakulima wetu watakuwa wanapata taarifa hizi wakiwa maeneo mbalimbali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua matumizi ya teknolojia ambapo ndiyo dunia ya leo inapoelekea, katika kurahisiha utoaji wa huduma kwa wakulima na hasa kupitia Maafisa Ugani, tunao mfumo ambao tunauita *N-Kilimo* ambao mpaka hivi sasa tumeshasajili Maafisa Ugani 9,725, ambao kazi yao kubwa ni kuhakikisha kwamba tunasambaza taarifa hizi kwa wakulima kupitia programu hii. Pia tunayo *call center* yetu ya Wizara ya Kilimo ambayo pia wakulima ambao wanapata changamoto

mbalimbali wamekuwa wakipiga simu na kupata ufafanuzi na kujibiwa baadhi ya changamoto ambazo wanakabiliaba nazo.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu rai na kuwaomba wakulima wote nchini Tanzania kuendelea kuitumia namba yetu ile ya 0733 800 200 kwa ajili ya kuweza kupata huduma mbalimbali za kilimo kupitia teknolojia hii.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ushauri tunaupokea wa kukaa na kampuni za simu kurahisisha utoaji wa huduma hizi za ugani kwa wakulima wetu. Ushauri huo tumeupokea ni mzuri, tutaona namna ya kuweza kuboresha ili wakulima wetu waweze kupata taarifa kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHW. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika taarifa yao ya Wizara ya Kilimo walisema sasa hivi wakulima watakuwa wanapimiwa udongo kupitia Maafisa Ugani kwa vishkwambi. Elimu hiyo sasa wakulima wanayo maana yake nimeona bado hawajaanza kutumia hiyo teknolojia ya kupimiwa udongo katika mashamba yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha tunapima afya ya udongo ya ikolojia zote saba nchi nzima ili wakulima wawe na taarifa sahihi za afya ya udongo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali kupitia Maafisa Ugani tumewapatia *scanners* za kwenda kupima afya ya udongo ambayo itasaidia kutoa taarifa kwa wakulima. Vilevile katika mwaka wa fedha unaokuja tutakwenda kununua *mobile lab* ambazo zitakuwa pia zinapita kwa ajili ya kuwapimia afya ya udongo wakulima. Kwa hiyo, tutakuwa tunao uwezo wa kupima

afya ya udongo kupitia maabara na kupitia katika magari pamoja na *kit* ambacho tumewapa Maafisa Ugani ambapo mkulima akipimiwa afya yake ya udongo hapo hapo akiwa shambani atapata cheti chake ambacho kitaonesha katika udongo huo kuna *nutrients* za aina gani na anahitaji nini kupanda zao gani na atumie mbolea ya namna gani, ambayo itakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wakulima wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 702

**Mafunzo kwa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi - Pwani**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza: -

Je, upi mpango wa kuwapa mafunzo Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ngazi za Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya – Pwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani ni miongoni mwa Mikoa iliyofanya vizuri katika kuanzisha majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ambapo Jukwaa la Mkoa limeanzishwa kwa mafanikio makubwa hadi kufikia wazo la kuanzisha kiwanda cha vifungashio. Wizara katika bajeti yake ya mwaka 2023/2024 imetenga kiasi cha shilingi milioni 161 kwa ajili ya kujenga uwezo wa majukwaa, ambapo Mkoa wa Pwani utakuwa miongoni mwa Mikoa iliyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naishukuru sana Serikali kutupongeza Mkoa wa Pwani kwa kufanya vizuri, lakini pia kwa kutenga kiasi cha shilingi milioni 161 kwa kuanza hayo mafunzo. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je, ni lini hasa mafunzo hayo yataanza kwa kuwa majukwaa yale yameundwa muda mrefu na tumefanya jitihada mpaka Kitongoji, Vijiji, Wilaya mpaka na Mkoa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika jibu lake la msingi amesema zimetengwa hizo fedha shilingi milioni 161 na ndani yake kutakuwa na za Mkoa wa Pwani, lakini nataka niulize, je, Serikali inaipa wajibu gani Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kupitia Katibu Tawala wa Mkoa na Halmashauri zetu za Mkoa wa Pwani katika kulea majukwaa haya ili yalete tija iliyokusudiwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, swali lake la kwanza kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, Serikali imetenga shilingi milioni 161 kwa ajili ya kuwajengea uwezo na kuwajengea uwezo wanawake ili kuinuka kiuchumi ambapo

Mkoa wa Pwani umetengewa shilingi milioni 58.5 kwa ajili ya kuendesha mafunzo hayo.

Niwaombe tu Maafisa Tawala wa Mikoa wote nchini waanze kuandaa programu hizo za mafunzo na mwaka wa fedha ukiingia mafunzo hayo yaanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, zipo taasisi mbalimbali za binafsi ambazo zinawezesha wananchi kutoa mikopo mmoja-mmoja na vikundi. Kwa hiyo, niwaombe wananchi waendelee kutumia fursa hizo kuhakikisha uchumi wao unakua, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ziko baadhi ya Halmashauri hapa nchini ambazo mapato yake sio toshelevu hivyo hawawezi kutosheleza kutoa mikopo ya asilimia 10.

Je, ni upi mkakati wa Wizara hii kuwawezesha wanawake kiuchumi kuanzia ngazi ya kitongoji na vijiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inawaagiza Maafisa Tawala wa Mikoa na Maafisa Ustawi wa Jamii waendelee kutoa elimu kuhakikisha wananchi wote wanapata elimu, ili kuweza kujiinua kiuchumi na kuhakikisha wanakuwa vizuri katika maisha yao na maendeleo yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watu wengi hawafahamu uwepo wa Sheria ya Manunuzi ya asilimia 30 kwa makundi maalum. Sasa je, Serikali ina mkakati gani kueneza uelewa juu ya uwepo wa sheria hii ya asilimia 30 ya manunuzi kwa makundi maalum ambayo ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu? Ahsante.

**SPIKA:** Hili ni la Wizara ya Fedha nafikiri, ama? Sio la Wizara ya Fedha hili?

Hebu, *Chief Whip,* hili ni la Wizara ya Fedha au Maendeleo ya Jamii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, lina-*cut across* kwenye sekta hizi zote.

**SPIKA:** Ahaa, basi ahsante.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, labda kwa kuwa linakwenda kwenye sekta zote ninaomba tu niseme kwamba kwa sababu Serikali inafahamu umuhimu wa makundi hayo tutajipanga ndani ya Serikali ili sekta zote zihakikishe zinasimamia jambo hili na makundi hayo maalum ambayo yamekwisha kutamkwa kwenye sheria hiyo waweze kunufaika. Hiyo ni fursa muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Ahsante sana.

Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Grace Tendega.

Na. 703

**Uhitaji wa msaada wa kisaikolojia kwa watu waliopata ukatili wa kijinsia**

**MHE. GRACE V. TENDEGA K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia msaada wa kisaikolojia watu waliopitia ukatili wa kijinsia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha vituo 22 vya huduma ya mkono kwa mkono *(One Stop Centres)* kwa ajili ya hospitali za mikoa 13 ikiwemo Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza, Arusha, Tabora, Morogoro, Kigoma, Dodoma na Simiyu kwa ajili ya kuwahudumia waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Vituo hivyo hutoa huduma za kipolisi, ushauri nasaha na huduma za afya. Lengo la Serikali ni kuwa na kituo angalau kimoja kwa kila Mkoa. Vilevile kuna nyumba salama 11 nchini na Madawati ya Jinsia katika vituo vyote vya polisi na magereza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza nishukuru majibu yake ni mazuri sana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, nina matarajio kwamba sasa kila Mkoa utapata kituo hiki cha *One Stop Center.* Swali langu, ni lini vituo hivi vitaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Maafisa Ustawi wa Jamii ndio wanaotoa huduma za kisaikolojia; nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mnaajiri Maafisa Ustawi wa Jamii wa kutosha ili waweze kutoa huduma hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuratibu uanzishaji wa vituo vya mkono kwa mkono hadi kufikia lengo la kuwa na angalau kituo kimoja kwa kila Mkoa. Hii ni kwa sababu ya kuwasaidia wananchi wetu pale wanapopata matatizo au changamoto ili waweze kwenda mahali ambapo watafanikiwa na kutatuliwa matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali itaendelea kuwaajiri Maafisa Ustawi wa Jamii kila tunapopata kibali ili waweze kusambazwa nchi nzima na kuhakikisha matatizo yote yanaondoka kwa wananchi na kupata elimu ambayo itawasaidia ili wasiathirike na msongo wa mawazo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa hivi vitendo vya ukatili wa kijinsia vimekuwa vikiongezeka nchini, na tumetambua huo mkakati wa Serikali kuhakikisha vituo na kuajiri ustawi wa jamii, lakini nataka nijue sasa mkakati kabisa wa kuhakikisha kwamba tunaondoa kabisa huu ukatili wa kijinsia. Mkakati gani ambao Serikali inao kuhakikisha kwamba, yani kunakuwa na *zero* ukatili wa kijinsia Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa kuna vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto hapa nchini. Jukumu letu ni kuhakikisha wanawake na watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili kuwapatia huduma muhimu ikiwemo ushauri nasaha ili wasiathirike kiakili pale wanapopata vitendo vya ukatili, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhakikisha jamii nzima inashirikiana katika jambo hili la kutokomeza ukatili wa watoto, wanawake na makundi maalum nchini, lakini nadhani Bunge lako tukufu linafahamu kwamba Serikali inao mpango mkakati wa kitaifa wa kutokomeza unyanyasaji wa makundi haya maalum ambao ni jumuishi kwa sekta zote, na kila Wizara imeshirikishwa katika kuhakikisha mkakati huo maarufu kwa MTAKUWA unafanikiwa na unazaa matunda ya kuhakikisha Taifa hili la Tanzania linakuwa mstari wa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tumeshuhudia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan yeye mwenyewe kwa kuzingatia matakwa ya kimataifa amekuwa mstari wa mbele kutengeneza afua ambazo zitasaidia mapambano hayo dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia katika Taifa letu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka Serikalini. Kabla hatujaendelea na ratiba yetu, nilete matangazo tuliyonayo siku ya leo hapa Bungeni.

Tangazo la kwanza ni la wageni walioko hapa Bungeni; tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali na nitawatambulisha kama ifuatavyo:-

Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Juma Aweso ambaye ni Waziri wa Maji, huyu ni Balozi wa Maji kutoka Mkoa wa Tanga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na hii ni familia yake kutoka Mjini Magharibi, Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa David Silinde ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hawa ni walimu wa Sekondari ya Jakaya Kikwete kutoka Tunduma, Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na hiki ni kikundi cha wafuga nyuki kutoka Kata ya Dabalo, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 65 wa Mheshimiwa Taska Mbogo ambao ni Makatibu wa UWT Kata na Wenyeviti wa UWT Kata kutoka Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi, wakiongozwa na Katibu wa UWT Mkoa wa Katavi, Ndugu Jenifer Chinguile, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni watoto wake wakiongozwa na mke wake Ndugu Ukundi John Sillo, karibuni sana. *(Makofi)*

Mke wake ndio yupi?

*(Hapa Ndg. Ukundi John Sillo Mke wa Mhe. Daniel B. Sillo Alisimama)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana na karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 31 wa Mheshimiwa Tarimba Abbas ambao ni Jumuiya ya Wazazi na UWT kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ambaye ni mtoto wake kutoka Kusini Unguja, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu kutoka *Storm FM Radio* ya Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo kutoka Mbagala, Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mariam Kisangi ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni wafanyakazi wa *Hotel Fifty-Six* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Charles Kajege ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni makada wa CCM kutoka Chamwino, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni Jumuiya ya Wazazi kutoka Wilaya ya Ilala, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Wilaya ya Urambo, Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo kutoka Jijini Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Mussa Sima kutoka Singida Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 70 na walimu 10 kutoka Shule ya *Sheikhat Hissa Islamic Seminary* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 na walimu 14 kutoka Shule ya Awali na Msingi ya *Stone of Help* iliyopo Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge na watumishi kwamba zoezi la kugawa sadaka iliyoletwa na Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Mbarali, Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed bado linaendelea, na wale ambao bado hawajachukua sadaka hiyo wanaombwa wakachukue kuanzia saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo maelezo hapa kuhusu Tuzo ya Uandaaji Bora wa Hesabu kwa mwaka 2021.

Waheshimiwa Mawaziri mnaozungumza tusikilizane kidogo.

Maelezo ya Spika kuhusu Tuzo ya Uandaaji Bora wa Hesabu kwa mwaka 2021 ambayo Bunge limeipata.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kutumia fursa hii kuwataarifu kuwa Ofisi yetu ya Bunge ilipata tuzo ya mshindi wa tatu wa Taarifa Bora ya Hesabu za mwaka 2021. *(Makofi)*

Tuzo hii ambayo nitawaonesha muda si mrefu imeandikwa, *Third Winner for the Best Presented Financial Statements Awards for the Year 2021* ambayo ilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi *(The National Board of Accountants and Auditors – NBAA)* wakati wa maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuzo hii ya Utayarishaji Bora wa Mahesabu ambayo ofisi yetu imepata hutolewa kila mwaka na *NBAA* kwa lengo la kuhamasisha Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa, Mashirika na Kampuni Binafsi kuzingatia viwango vya kimataifa katika uandaaji wa hesabu. Kwa maana hiyo mhimili wa Bunge umeonesha mfano bora wa kusimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi katika kusimamia mali za umma kwa kuzingatia pia Bunge lina jukumu la kusimamia taasisi nyingine za umma.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kulipongeza Bunge kwa kazi hii nzuri iliyofanyika ya uandaaji bora wa hesabu, nitoe rai kwa wahasibu na wakaguzi wote nchini kuendelea kufanya kazi zao kwa ufanisi kila mwaka wa fedha ili kuondoa changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie sasa kwa kuwaonesha tuzo ambayo tumeipata, ambayo ni Tuzo ya Mshindi wa Tatu wa Taarifa Bora ya Hesabu za mwaka 2021. *(Makofi)*

*(Hapa Tuzo ya Mshindi wa Tatu wa Taarifa Bora ya Hesabu kwa mwaka 2021 ilioneshwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, tuzo yetu hii hapa. *(Makofi)*

Haya sasa niwasomee na kama nilivyosema nia yetu sio kwamba tunajidai, nia yetu ni kuwaeleza wananchi kwamba tuko vizuri kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Haya, ngoja niwasomee Waheshimiwa Wabunge; *"The National Board of Accountancy and Auditors Tanzania: this Award is given to the National Assembly Fund, Vote No. 42 as a Third Winner in the Ministries and Government Departments Category for the Best Presented Financial Statements Award for the Year 2021. Awarded on the 30th November, 2022." (Makofi)*

Kwa hiyo, tumepata tuzo hii Waheshimiwa Wabunge na nitumie fursa hii kumpongeza sana Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha mambo yanakuwa mazuri, lakini pia niwapongeze sasa watumishi wa Ofisi inayohusika na utunzaji wa mahesabu wakiongozwa na *Chief Accountant* wetu na Mkaguzi wetu wa Ndani kwa kazi nzuri wanayoifanya, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo lingine hapa linahusu kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, leo ni Alhamisi na tulimtarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu angekuwepo kwa ajili ya maswali, lakini tumeletewa taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko nje ya Dodoma kwa majukumu mengine ya kikazi na kwa hiyo, anayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni ni Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo ambaye atakuwa anakaimu nafasi hiyo mpaka Waziri Mkuu atakaporejea. *(Makofi)*

Nimeambiwa picha haijapigwa bado, kwa hiyo, ngoja picha ipigwe vizuri. Sasa sijui inapigiwa upande gani. Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Kwa kusema hayo nilimwona Mheshimiwa Mhata amesimama, Mheshimiwa Ally Mhata.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako; katika swali langu la msingi Na. 695 linalohusu lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa kwenye Kituo cha Afya cha Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali sina matatizo nayo, tatizo langu liko kwenye majibu ya nyongeza ambapo nilitaka kufahamu Serikali ilileta vifaa tiba katika kituo hiki chakavu cha muda mrefu, nikataka kufahamu je, walikuwa na lengo gani kutuletea vifaa tiba wakati kituo cha afya hakina uwezo wa kuhimili vifaa hivi. Majibu ya Naibu Waziri amemwelekeza mkurugenzi aandae bajeti ya kufanya ukarabati kituo kile cha afya.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwongozo wako; ni sahihi majibu ya Mheshimiwa Waziri kumwomba mkurugenzi au kumwelekeza mkurugenzi kuandaa bajeti ya kufanya ukarabati kituo cha afya chakavu wakati ni wajibu wa Wizara yake kuandaa bajeti na kuleta fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya?

Mheshimiwa Spika, ninataka Mwongozo wako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, jambo la dharura.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole.

## HOJA YA DHARURA

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimesimama hapa kwa Kanuni ya 54 kuomba shughuli hizi za Bunge ziahirishwe tujadili hili jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali iliweka zuio la kuzuia mahindi kuuzwa nje ya nchi. Zuio hilo limesababisha bei ya mahindi kuporomoka kwa kiasi kikubwa. Sasa hivi kote kule

Mbeya, kwangu Mbozi, debe moja la mahindi linauzwa shilingi 7,000 na bei inazidi kuteremka. Hii inavunja moyo wakulima ambao wamejitolea kulima kwa kiwango kikubwa. Matokeo yake sasa tunakwenda ambako gunia la mahindi linakwenda kuuzwa kwa shilingi 15,000.

Mheshimiwa Spika, sasa jana Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba zuio hilo ni kwa ajili ya kuhakikisha wafanyabiashara wanafuata zile taratibu, lakini wanaozuiwa ni wafanyabiashara ambao wana *BRELA***,** wana leseni, wanalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba shughuli za Bunge ziahirishwe tujadili kwa kina tuone namna gani ya kuishauri Serikali kuokoa hii bei ya mahindi ambayo inaporomoka, na kuwanusuru wakulima wetu ambao wataingia kwenye umaskini mkubwa kiasi kwamba watahitaji kuuza magunia kumi kununua mfuko mmoja wa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona, lakini sijampa nafasi bado ya kutoa hoja.

Nianze na hoja ya Mheshimiwa Ally Mhata kuhusu majibu yaliyotolewa na ameomba mwongozo kupitia Kanuni yetu ya 76 akieleza kwamba swali alilokuwa ameuliza, swali lake la msingi amesema majibu ambayo Serikali imeyatoa hana shida nayo. Amepata tu changamoto kwenye majibu ya swali la nyongeza, ambalo yeye ameuliza kuhusu Serikali kununua vifaa kupeleka kwenye kituo cha afya ambacho hakina uwezo wa kuhimili wingi na ukubwa pengine, wa hivyo vifaa kwa sababu ni kituo cha muda mrefu, kina uchakavu na hivyo hakina utoshelevu wa maeneo ya kuweka vifaa hivyo.

Sasa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu hapa ameeleza kwamba vifaa hivyo, na yeye amekubali Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kama vikipelekwa sehemu nyingine, basi wafanye utaratibu huko kwenye halmashauri kwamba wafanye ukarabati wa kile kituo cha afya halafu utaratibu mwingine ufanyike kwa sababu Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vingine, kwa hivyo ukarabati ule ukikamilika vifaa vingine vitapelekwa.

Hoja ya Mheshimiwa Mhata, kwa sababu majibu hayo yaliambatana na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri anamwagiza mkurugenzi kufanya ukarabati wa hicho kituo. Sasa nimemsikia pia wakati akitoa hayo majibu, amesema halmashauri itenge fedha kwa ajili ya ukarabati. Lakini sasa kwenye kutenga fedha pale maana yake sasa hivi mchakato wa bajeti umeshaisha, sijui watatengea wapi hizo fedha.

Kwa hivyo nadhani hofu ya Mheshimiwa Mhata ni kwamba mkurugenzi akiagizwa saa hizi kwamba atenge fedha ni kwamba atenge mapato ya ndani, atengee kwenye kona gani? Maana sasa hivi mchakato wa bajeti kwenye halmashauri umeshapita, na huku Bungeni ndiyo tuko saa hizi kwenye mchakato wa mwisho kabisa kukamilisha hili jambo.

Mheshimiwa Mhata nimekuelewa sawasawa hofu yako? Sawa, amenijibu kwa ishara kwamba ndivyo nilivyomuelewa.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, nitakupa dakika moja ili pale anapotengea bajeti kwa kipindi hiki ni wapi, ama hayo maelekezo yako yalikuwa maalum kwamba pesa zitatoka eneo gani ili Mheshimiwa Mhata ajue kile kituo cha afya alichoulizia kitakarabatiwa, na vifaa vile kwa sababu wananchi wameviona, ndiyo hoja yake, anataka viende pale. Kwa hiyo nitakupa nafasi.

Lakini nimalize hili la Mheshimiwa George Mwenisongole ambaye amesimama hapa akitaka Bunge lijadili hoja ambayo yeye ameiita ya dharura, na amesimama kwa Kanuni ya 54 akitaka Bunge tuahirishe shughuli tunazozifanya ili tujadili jambo ambalo amelisema ni la dharura.

Waheshimiwa Wabunge jambo alilolieleza, ameeleza ni kuhusu bei ya mahindi ya wakulima, kwamba inaendelea kuporomoka kwa sababu ya katazo ambalo Serikali imelitoa. Jambo hili lilijitokeza wakati wa michango hapa jana nafikiri, na ikatolewa taarifa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo akisema kwamba hakuna katazo la kuuza mahindi nje, isipokuwa wameweka utaratibu kwamba lazima ufuatwe. Huo utaratibu ukifuatwa basi wananchi wanaruhusiwa kuuza mahindi nje.

Sasa sijajua huo utaratibu ni upi ambao unatafsirika kwamba ni zuio. Maana neno zuio limetumika sana, kwa hiyo, sijui kama ni utaratibu uliowekwa ndiyo unaitwa zuio au ni kwa namna ipi wananchi wanaona wanazuiwa. Na Wabunge nimewaona humu ndani mmesimama, maana yake na ninyi mnakubaliana kwamba pengine hoja ya Mheshimiwa aliyoisema ni kwamba kuna katazo fulani.

Sasa kwa sababu Serikali iko hapa Bungeni, kabla sijaitoa hiyo hoja kama ni ya dharura ama siyo ya dharura, niipe nafasi; hilo katazo lipo? Kama lipo wao watoe maelezo hapa, kwa sababu katazo linatolewa na Serikali. Na kama hilo katazo halipo, basi wao watoe huo utaratibu ambao wananchi wanaruhusiwa kwenda kuuza nje, hasa wale ambao, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, kwamba wamefuata taratibu zote, wanalipa kodi na wanavyo vibali. Ni kwa namna gani hilo katazo linaokena bado lipo na bei inakuwa chini.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, dakika moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, niliposema kwamba namwelekeza mkurugenzi wa halmashauri atafute fedha, atenge fedha, wao wana *own source* na vilevile kama ilikuwa ni kipaumbele chao na wanaona kuna vifaa tiba Serikali Kuu imepeleka vipya na kituo ni chakavu, ilitakiwa waweke kwenye vipaumbele vyao wakati wanapanga bajeti yao na kuileta Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, bado tuna nafasi katika *mid-year review,* wanaweza wakaiweka kama kipaumbele na tukaona ni namna gani tunatafuta fedha hiyo kwa ajili ya kuweza kupeleka kukarabati Kituo hiki cha Afya cha Nanyumbu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameshaeleza hofu yake hapa ya halmashauri yake kuweza kumudu huo ukarabati, na ndio maana wameshindwa, ndiyo maana wakahamishia vifaa sehemu nyingine, nafikiri Mheshimiwa Waziri uonenane na Mheshimiwa Mhata mkae muone hizo hoja za Mheshimiwa Mhata halafu Serikali Kuu, kwa maana ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, muone eneo gani mnaweza kusaidia kwenye hilo eneo la Mheshimiwa Mhata, hasa ukizingatia mnajenga vituo vingi sana nchini. Kwa hiyo, sioni namna gani TAMISEMI itashindwa kukarabati kituo hicho cha afya ili muweze kumsaidia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake waweze kupata huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ufafanuzi dakika moja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Cha kwanza niseme hakuna mfanyabiashara yeyote aliyefuata utaratibu uliowekwa ambaye kazuiliwa kupata *export permit*. Hata jana kama Wizara tumetoa *export permits* za zaidi ya tani 20,000 za mahindi; tumetoa *export permits* za zaidi ya tani 15 za unga wa mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulichokataza kama Serikali ni mtu kutoka nje ya nchi kwenda shambani kupakia mazao, kwenda *border* kumlipa dalali shilingi 800,000 kuvushiwa mazao kwenda nje; hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tulichokataza ni mfanyabiashara yeyote kufanya biashara ya mazao bila leseni ya biashara, bila kuwa na *TIN Certificate,* bila kuwa na *tax clearance* na bila kuomba *phytosanitary certificate* kwa ajili ya *export* ya mazao. Hili ni jambo la pili tulilolikataza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili limekuwa tatizo. Unakumbuka Bunge hili lilizungumzia Watanzania waliozuiliwa Zambia; nasema hivi; Watanzania tumekuwa na *culture* ya kutaka kuifanya sekta hii ijiendeshe kiholela. Hatuwezi kuruhusu. Kama Bunge lako Tukufu linataka tuendeshe hili jambo kinyume na utaratibu, tulete sheria, tufute *Food Security Act,* tufute sheria inayotaka kuwa na leseni, tufute sheria ya kumtaka mfanyabiashara kuwa na *TIN*.

Mheshimiwa Spika, la tatu; bei elekezi ya Serikali ya mahindi ni shilingi 800 kwa Sumbawanga Mjini, shilingi 800 kwa Mbeya Mjini, shilingi 800 kwa Njombe Mjini, shilingi 600 katika wilaya zilizoko pembezoni. Ndiyo bei tunayonunulia, na Serikali imeipatia *NFRA* bilioni 320 na wameshaanza kufungua vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwatake wakulima wa nchi nzima, hatujazuia *export* bali tunachokitafuta ni ku-*formalize* mfumo wa ununuzi na uuzaji. Kama *foreigner* anataka kununua mahindi ya Watanzania, aje ndani ya nchi asajili kampuni kwa mujibu wa sheria, ama anunue mazao kupitia kampuni za Watanzania, aingie nao mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la nne, tunachokitafuta ni kitu kimoja; hatuwezi ku-*export* zaidi ya tani 500,000 mpaka 700,000 fedha hizo hazionekani kwenye mfumo wa uchumi wa nchi. *It is disadvantageous. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe wakulima, niwaombe Watanzania, unataka kufanya biashara ya mazao, tumekupa *rooms* mbili; pale *border* yupo afisa wa Wizara ya Kilimo ambaye ana-*provide phytosanitary certificate*. Unapotoka wilayani – na niwaambie madereva wote, anayekupakilia mzigo wa mahindi, mchele, maharage, anapokupa zile karatasi za malipo za halmashauri mwambie akupe *copy* ya leseni ya biashara yake na *copy* ya *TIN* ili unapofika kwenye geti uweze kuonesha, watu wasi-*take advantage,* tunawaomba Watanzania, ni mfumo wa ku-*formalize* na kuongeza *tax base* kwenye *economy*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama hatutaki kufanya namna hii tukubaliane humu ndani.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Kabla hujakaa; wewe umesema bei elekezi ni shilingi 800; hii shilingi 800 inatafsiriwa vipi kwenye ile niliyoambiwa debe sijui ni shilingi ngapi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni hivi…

**SPIKA:** Yaani ili nijue hiyo bei elekezi ndiyo inaifanya bei ya mahindi iwe chini…

**WAZIRI WA KILIMO:** Hapana.

**SPIKA:** …au bei elekezi inaifanya bei ya mahindi iwe ya kawaida? Kwa sababu huku nimesikia 15,000, wewe umesema 800, kwa kilo?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, *yes*. 800 kwa kilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ulisema 15,000 kwa debe?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi debe ni shilingi 7,000 mpaka 8,000.

**SPIKA:** Debe ni kilo ngapi?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, kilo 20.

**SPIKA:** Kwa hiyo hapa kwa bei elekezi maana yake debe ni shilingi ngapi?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, gunia ni shilingi 48,000. Lakini kwa bei ya Waziri ni shilingi 80,000, kitu ambacho siyo uhalisia wa kule.

**SPIKA:** Sawa, nilitaka tu kuelewa bei elekezi inamaanisha nini. Kwa sababu hoja ambayo ilitaka kujadiliwa hapa ndani ni

hoja kwamba mahindi yameshuka bei, ndiyo hoja iliyopo. Kama hivyo ndivyo, hii ndiyo bei elekezi, 800 kwa kilo; si ndiyo?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kidogo *clarity;* 800 kwa kilo katika makao makuu ya mikoa, bei ya juu, bei ya chini ni shilingi 600 ambayo gunia ni shilingi 60,000 kwenye *peripheral areas,* ndiyo bei ambazo Serikali imetoa. Tumeshatoa matangazo, na hata kesho yatatoka matangazo kwenye magazeti yote ili kuonesha msingi wa bei elekezi ya Serikali.

**SPIKA:** Sawa, sasa…

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo moja tu, samahani, nakuomba, kama mtu anaamua kuuza bidhaa yake chini ya bei elekezi ya Serikali, hayo ni maamuzi yake. Nasema, ndiyo ukweli. Bei ya Serikali ni shilingi 800, ndiyo bei tunayonunulia sisi. Bei elekezi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge tuelewane jambo moja; Mheshimiwa George Mwenisongole alivyokuwa anaileta hoja yake hiyo ya dharura, alikuwa anaizungumzia kwenye muktadha wa bei ya mahindi kushuka sana na wakulima kuathirika.

Serikali inasema imewapatia pesa *NFRA* kununua mahindi kwenye hayo makao makuu ambayo yametajwa ya ile mikoa inayolima mahindi, kwamba kule wakienda *NFRA* kuuza mahindi maana yake pesa watazikuta zipo, wapeleke mahindi wakauze huko *NFRA* ambako bei ni kubwa. Mheshimiwa Waziri niko sawasawa? *(Makofi)*

Kama hiyo ndivyo sisi Waheshimiwa Wabunge, kama hayo ndiyo maneno ya kuwaambia wakulima wetu, wale ambao sasa mahindi yao wanasema tunauza kwa bei rahisi waambiwe msiuze huko, pelekeni *NFRA* kwa sababu pesa kule zipo, ili wakauze mahindi yao kule. *(Makofi)*

Sasa watakapopeleka kule kama wasipozikuta pesa ndiyo hoja irudi hapa Bungeni kwamba Mheshimiwa wamepeleka

mahindi *NFRA* na hawajalipwa pesa zao. Ndiyo hoja ije hapa. Kwa sababu kama bei kubwa ipo *NFRA* halafu anakwenda kununua mtu wa bei ya chini, sidhani kama ni hoja tunayoweza kuijadili hapa kama hoja ya dharura.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane nitawapa nafasi kwa sababu bado tuko hapa Dodoma; leo ni Alhamisi, wiki ijayo tupo na kesho pia tupo. Leo hii waambieni watu wenu wakauze mahindi wapi, *NFRA* ambako bei ni kubwa. Kukiwa na changamoto mtaileta hiyo hoja hapa ndiyo tutaweza sasa kuijadili katika ngazi hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nimesimama, sasa mnapotaka kuzungumza na mimi ni mpaka nikiwa nimekupa nafasi.

Sasa kwa kuwa nimesimama na hayo ndiyo maelekezo niliyowapa; Wabunge ambao mna wakulima kwenye majimbo yenu wapeni majibu ya Serikali, kwamba mahindi *NFRA* yananunuliwa kwa shilingi 800 mpaka 600 kulingana na eneo sasa ambalo hiyo *NFRA* ofisi ipo. Kama kule wakienda wakikuta hayanunuliwi hayo mahindi yao, ndiyo hoja iletewe hapa Bungeni tuijadili.

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kusema hayo, ataingia Mwenyekiti kwa ajili ya kuendelea na ratiba yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**22 JUNI, 2023**

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, wewe ni Mbunge mzoefu, usijaribu Kiti, naomba utulie kwanza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Najaribu vipi? *It's my right*. Ni haki yangu.

**MWENYEKITI:** Usikijaribu Kiti Mheshimiwa Matiko.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Jerry William Silaa, wakati huo Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na Mheshimiwa Ndaisaba wanajiandaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyopo mezani ya bajeti ya Serikali ya trilioni 44.38. Kwanza nianze kwa pongezi kwa bajeti hii ambayo imeenda kutoa majibu kwenye maeneo mengi…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, Mbunge mwenzetu anachangia.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Serikali kwa kuja na bajeti hii. vilevile naomba niungane na

wenzangu kuipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa ya uchumi. Uchumi wa nchi yetu umepanda kutoka dola bilioni 69.9 mpaka dola bilioni 85.4. Mapato ya Serikali yamezidi kukua na hii imepelekea nchi yetu kupata *rating* za juu kwa kampuni zinazoheshimika duniani za *Fitch Writing* na *Moody's Investors Service*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu, kampuni kama hizi ni sawa na timu zetu zinavyopata faraja, zinapopata *rating* ya *FIFA* ama *rating* ya *CAF*. Huku duniani huwezi kufanya mwenyewe ukajipa viwango mwenyewe, kwa hiyo kwa *rating* hizi za kampuni hizi yanayoheshimika duniani nchi yetu imeongezeka viwango vya kukopesheka nani pongeze kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, uwezo mkubwa wa Serikali katika ukusanyaji wa mapato umeiwezesha Serikali kuwa na uwezo mkubwa wa kutekeleza miradi ya kimkakati na miradi mikubwa. Kwa mfano Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere tumeoneshwa hapa inatekelezwa kwa asilimia 86 na inakaribia kukamilika, ujenzi wa *SGR* unaendelea bila kukoma vipande vyote vina wakandarasi, Daraja la Kigongo – Busisi liko katika hatua nzuri na litakamilika kwa muda uliopangwa, *grid* za umeme zinaendelea kusambazwa nchi nzima. Ni kazi kubwa kwenye miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya kati pia. Sisi kule Dar es Salaam kuna Bwawa la Kidunda ambalo litasambaza maji Dar es Salaam ambao inaenda ku-*complement* ile miradi ya maji usambazaji wa maji ambayo hata kwenye Jimbo la Ukonga ipo. Upo mradi wa mwendokasi awamu ya tatu Gongo la Mboto - Kariakoo. Jimbo la Ukonga ni wanufaika na unajengwa kwa kasi kubwa. Serikali pia haijasimamisha hata mradi mmoja ile miradi midogo, madarasa yanajengwa, vituo vya afya vinajengwa, zahanati zinajengwa na hii ni pongezi kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niongelee maeneo machache. Kwanza nikuendelea kuishauri Serikali kuongeza wigo mpana wa ukusanyaji wa kodi. Tumeoneshwa hapa kwenye hotuba, nchi hii watu wenye *TIN* ni watu milioi 4.45, na hizi ni *TIN*

zinazo-*include* zile leseni na wale wanaolipa *PAYE* kwenye mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIN* za biashara zimekomea milioni 1.641 na tumeambiwa hapa katika hizi *TIN* za biashara asilimia 80 ya makusanyo inatoka kwenye *TIN* asilimia 20; yaani watu kama laki nne ndio wanatuendeshea nchi kwenye makusanyo haya ya takribani trilioni 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali iendelee kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na mifumo hii, nimemsikia Mbunge mmoja hapa nadhani kwenye mjadala wa bajeti ya Wizara ya Fedha, aliongelea mfano wa Estonia. Estonia ni nchi ambayo imeweza kuwa na *central ledger* ambayo shughuli zote za kiuchumi na kijamii ziko kwenye eneo moja. Hii inasaidia Serikali kuweza ku-*monitor* shughuli za wananchi ili kuweza kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlimsikia hapa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, leo mtu ana-*export* mahindi lakini hasomeki sehemu yoyote. Lakini leo mfanyakazi mwenye *threshold* inayozidi 270,000 na kwenye mapendekezo yao 370,000 analipa *PAYE* kwenye mshahara wake. Leo kuna mtu anasafirisha mahindi tani kwa tani halipi kodi. Leo kuna mtu ana mifugo maelfu kwa maelfu halipi kodi. Mimi nadhani Serikali iendelee kuboresha mifumo lakini iendelee kwenye kulenga kuwa na *central ledger,* maana kila mtu anaandika mfumo wake; na ndiyo inakuja hoja ya mifumo ya kusomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Bashe amekuwa na mfumo wake anagawa pembejeo, lakini mfumo ule hauwezi kwenda kumsoma ni mkulima yupi amepata pembejeo kiasi gani na leo mahindi yake ameuza wapi na anaingiza kiasi gani kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ipo mifumo mingine kwa mfano Mfumo wa *ETS*. Kila mtu anakubaliana na mimi na takwimu zipo, kwamba tangu ufungwe *ETS* makusanyo ya kodi yameongezeka, zile *exercise duty* zinazotozwa kwenye biashara

zinazozalishwa nchini zimeongezeka. Na *SICPA* ni moja ya kampuni *reputable* duniani ambayo si tu inafanya mifumo ya kodi lakini pia imeaminika kwenye *printing* hasa ya vitu kama noti au fedha kwenye nchi mbalimbali na inafanya kazi kwenye nchi nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutakapokuwa na mifumo ya kisasa, na maeneo mengine Wizara ya Fedha ama Serikali isione tabu; Mheshimiwa Rais alishawahi kusema, nadhani alipokuwa akipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka jana, kwenye maeneo ambayo tunakwama sisi ndani tusipate tabu kutafuta utaalam wa nje kwa sababu yako maeneo yanahitaji ubobezi. Mimi naamini tukiwa na mifumo bora zaidi makusanyo yataongezeka kama tulivyoona kwa mfano wa *ETS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko eneo ambalo mimi nitaomba kutoa ushauri kwa Serikali, na ninadhani kama sitopata majibu ya msingi tutakutana kwenye *Finance Bill.* Serikali inapendekeza kufuta kodi ya *VAT* kwenye *gaming odds* na *gaming software.* Iliwahi kuwekwa huko nyuma kwenye *Section 64 ya Value Added Tax Act Cap.149* ya 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia *gaming odds* maana yake ni unazungumzia michezo yote ya kubahatisha. Bidhaa pekee inauzwa ni *gaming odds*. Serikali inapotaka kuchukua *gaming odds* ikaisamehe *VAT,* na ukizingatia *gaming odds* ina michezo mingi ya kubahatisha ni kampuni za kimataifa ambayo Serikali na Bunge hili liliweka ile *Section 64* ili kampuni zile zipate *representative* hapa nchini waende wakalipe *VAT;* na ndiyo kodi pekee inakusanywa kwenye eneo hili. Ukisha iondoa, ukachukua *gaming odds* ukaipeleka kwenye jedwali la kusamehewa, ambao kule kumejaa kilimo, mifugo na maeneo mengine ya uzalishaji, maana yake unaenda kujikuta kwenye shughuli hii ya michezo ya kubahatisha kwenye kampuni za nje hatutakusanya hata shilingi moja kwa sababu wale wanaofanya michezo hiyo ya kimataifa ni *non-resident* kwenye *tax base* yetu. Kwa hiyo, mimi ningependa kusema wazi kabisa siliungi mkono na ninadhani nitapata majibu ama tutakutana kwenye *finance bill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa uchache kabisa, siku ya jumamosi tarehe 17 tulikuwa pale *Mlimani City*, Mheshimiwa Rais alipokea Hundi ya shilingi bilioni 45.5 kutoka benki ya *NMB*. Huwezi kuzungumzia benki ya *NMB* bila kuzungumzia walipa kodi wakubwa, benki hii kwa mwaka wa fedha huu walitoa gawio, wamelipa kodi shilingi bilioni 453.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukaizungumzia benki ya *NMB* bila kuzungumzia mkakati wa Serikali ulioanza kwenye awamu ya tatu ya ubinafsishaji. Tuliwahi kuuza hisa zetu *Label bank* mwaka 2004. Jambo hili lilikuwa na kelele kubwa; bodi ya *NMB* iligoma, ilipelekea Serikali kuvunja bodi hiyo ya Wakurugenzi ya *NMB*. Lakini tangu uwekezaji ule ufanyike benki imezidi kuboreka, mifumo imeimarika na gawio limeongezeka. Tangu gawio la shilingi bilioni nne mwaka 2009 mpaka gawio la shilingi bilioni 45.9. Maana yake nini; Serikali hailipi mishahara *NMB*, Serikali hailipi umeme *NMB*, Serikali imeenda kupata gawio la bilioni 45.5 na kodi ya bilioni 453.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendeleza nchi hii bila kushirikiana na sekta binafsi, na mimi niombe Serikali, tulipitisha hapa Azimio la *IGA* ya bandari yetu ya Tanzania, kelele zimekuwa ni nyingi. Nishukuru Serikali imeendelea kutoa elimu, na elimu kubwa ni kwamba *IGA* sio mkataba wa utekelezaji na yeyote anayeenda nje ya hapo ana nia yake ovu maana wa kuelewa ameshaanza kuelewa. *IGA* ni makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai juu ya uwekezaji utakaoenda kufanyika kwenye bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ya kwenda kutekeleza miradi *(Host Government Agreement)* na zile *concession agreement* bado hazijaingiwa na *concern* zote za wananchi Serikali iliahidi hapa Bungeni na inaendelea kuahidi, na juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema, watazi-*consider* kwenye kuingia mikataba yenye maslahi na Taifa. Mimi naamini kabisa ufanisi wa bandari ukiongezeka na takwimu zipo uchumi wa Taifa utakua, forodha itaongezeka, kilimo kitachachuka, sekta zote za uchumi zitaenda kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaiomba Serikali, kama vile Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa alivyokubali kupigiwa kelele mwaka ule 2004, leo tunapokea Hundi pale *Mlimani City* jina lake halikutajwa hata mara tatu. Niombe Serikali ikubali ushauri, isikilize wananchi lakini wakati mwingine isikubali kuyumbishwa na watu wenye nia zao za kuitaka nchi yetu isiendelee kiuchumi; ikubaliane na hizo hoja za msingi za kuendeleza Taifa tuwe na uwekezaji na kushirikisha sekta binafsi kwenye maeneo ambayo wenzetu wamebobea tupate uendeshaji mzuri wa bandari. Miaka ijayo tutakuja hapa kupongeza na wakati wote nawajua binadamu hata wale walioshiriki jambo hilo hawatatajwa, sifa zitakwenda kwa wale watakaokuwepo wakati huo lakini ndiyo kazi ya viongozi kuweza kusimamia uongozi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mwisho, niombe Serikali iendelee kushirikiana na sekta binafsi, lakini kama nilivyosema iendelee kuboresha mifumo ya nchi yetu. Mifumo hii ikiwa bora kero zote tunazozisikia hata zikiwemo hizi za mahindi zilizotajwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Mwenisongole na kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo zitafika wakati zitakwisha na kila mtu atachangia katika uchumi wa Taifa lake kwa kadri anavyochochea kwenye uchumi wa Taifa lake. Isiwezekane kukuta mfanyakazi analipa kodi kwenye mshara wake kwenye *threshold* ndogo ya laki mbili na elfu sabini analipa kodi lakini kuna mtu mwingine anafanya biashara kubwa zaidi na hasomeki kwenye uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerry William Silaa kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula aweze kuchangia.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kwenye hoja zilizoko mbele yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uhai ili tuweze kulitumikia Taifa letu. Nianze kwa kusema

kwamba naunga mkono hoja, naunga mkono bajeti yetu. Bajeti nzuri inayoendelea kutoa matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoliongoza Taifga letu kuweza kupata maendeleo ya kiuchumi. Wote tunafahamu kwamba bajeti iliyoko mbele yetu, tunazungumzia bajeti ya shilingi trilioni 44.4, ni bnajeti kubwa na ni bajeti inayoenda kugusa maisha ya Watanzania. Lakini kinachofurahisha zaidi ni kwamba takribani shilingi trilioni 30.2 zitatokana na mapato ya ndani ambayo yataweza kusaidia kuendesha bajeti hii, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile, naipongeza Serikali kwa jitihada inazozifanya katika kuvutia uwekezaji katika nchi yetu. Taarifa zinatuonesha kwamba kuanzia mwezi wa pili mwaka huu *TIC* imeweza kuidhinisha miradi 162 yenye thamani ya dola milioni 1,833 na miradi hii inakwenda kuzalisha ajira ya takribani 25,900. Hongera sana Serikali kwa jitihada hizi tunazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia kitabu cha Mpango wa Hali ya Uchumi nikawa naangalia takwimu zilizoko pale ndani; takwimu zile zimenifariji. Wote tunafahamu kwamba ulimwengu sasa unapitia kwenye mdololo wa kiuchumi lakini licha ya kuwepo kwa mdololo wa kiuchumi bado kwenye nchji yetu tumeweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka huu kilikuwa ni asilimia 4.7 ukilinganisha na asilimia 4.9 ya mwaka jana. Sasa unaweza kuona kwamba kuna kushuka kidogo. Lakini tukizingatia athari za kiuchumi zinazotokana na vita ya kule Ukraine na matatizo ya mafuta katika ulimwengu lazima tuseme kama Taifa tumefanya vizuri sana kuhakikisha kwamba tuna-*maintain* ukuaji wa uchumi wa kiwango hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jambo linalofurahisha ni jinsi ambavyo Serikali imekuwa na uwekezaji wa kimkakati kwenye miradi ya kimkakati. Wote tumeona uwekezaji mkubwa

umefanyika kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, reli, sekta ya maji pamoja na kwenye sekta ya elimu. Uwekezaji huu ndio umetuhakikishia tumekuwa na ukuaji huu unaoridhisha, Serikali hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo tunapaswa kuliangalia kwa umakini ni ukuaji huu wa uchumi. Ukiuangalia kwa kina unaona kwamba sekta zilizochangia ukuaji huu sekta inayoongoza ni sekta ya burudani kwa asilimia 19, sekta inayofuata ni madini kwa asilimia 10.9, sekta nyingine ni bima asilimia 9.2, malazi na chakula asilimia tisa. Lakini sekta inayogusa Watanzania walio wengi, sekta ya kilimo, ukuaji wake umeshuka na hapa kama Taifa lazima tuongeze maarifa tuone tunatokaje kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta hii umeshuka kutoka asilimia 3.9 ya mwaka 2021 mpaka asilimia 3.3 mwaka 2022. Kitabu cha Hali ya Uchumi kinatuambia, mchango wa sekta hii kwenye *GDP* umeshuka kutoka asilimia 26.8 mpaka asilimia 26.2. Lakini *alarming* katika sekta hizi ni kwenye eneo la sekta ya uvuvi, hapa ndipo nilipo na maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta ya uvuvi umeshuka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2021 mpaka asilimia 1.9. Lakini mchango wa sekta hii kwenye *GDP* umedumaa, upo kwenye asilimia 1.8. Hii haiwezi kuwa sawa kwa sababu *potential* iliyopo kwenye sekta ya uvuvi ni kubwa, sekta hii hatujaitumia ipasavyo. Lazima tuongeze maarifa ya jinsi ambavyo kama Taifa tunaweza kunufaika zaidi na sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kwenye ufugaji wa samaki, kwa mwaka huu tumevuna tani 25,000 zilizotuingizia bilioni 170. Lakini tunazungumzia mabwawa ya kufuga samaki kwenye nchi hii, na ukubwa wake wote, tuna mabwawa 31,000. Vilevile tuna vizimba 780 vya kufugia samaki. Ongezeko la vizimba 307 kwa mwaka mzima, hii haiwezi kuwa sawa. Mheshimiwa Waziri tuongeze maarifa hatujatumia rasilimali yetu ipasavyo kwenye kufuga samaki kwenye ukanda wa Bahari; ni lazima tuongeze maarifa ili tunufaike. Kama wenzetu wanavyonufaika kama

wenzetu wanavyonufaika kwenye *blue economy* lazima na sisi tujielekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nililoliangalia ni kiwango cha shughuli za uzalishaji kwenye kiwanda. Ukiangalia takwimu za hali ya uchumi zinaonesha kwamba kiwango kilishuka kutoka asilimia 4.2 ya mwaka 2021, na sababu ziko wazi, Vita ya Ukraine, kuongezeka kwa gharama za mafuta pamoja na kuongezeka kwa pembejeo za uzalishaji mali. Hapa sasa lazima tujiulize, kama uzalishaji wetu kwenye viwanda ulishuka, *measures* tunazoziweka kwa mwaka huu wa fedha zinatuhakikishia kwamba tutapandisha? au zitasababisha kuwa na ushukaji mkubwa kwenye uzalishaji kwenye viwanda vyetu. Hili lazima tuliangalie kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa wamekuwa wakipiga kelele kwamba tumeweka tozo kubwa kwenye saruji, viwango vyetu vile vinaonekana ni vikubwa. Sasa tujiulize, kama tumeweka kodi kubwa kwenye saruji, je, wananchi wetu watamudu kutumia saruji zile? Kama hawatamudu, Je, mchango tunaoutegemea kutoka kwenye viwanda hivi kwenye pato letu la Taifa utakuaje? Utaathirika au utabaki vile vile? Maeneo haya ni vizuri tukayaangalia kwa umakini ili tuweze kutoka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nawapongeza kwa jinsi ambavyo wamekuwa wasikivu na kadhia ile ya biashara kule Kariakoo na mpaka tunazungumzia kupandisha kiwango cha *VAT* kwa *turn over* ile ya kutoka milioni 100 mpaka milioni 200 na kuendelea. Hapa lazima tuwe makini sana. Tumekuwa na ukuaji wa viwanda vidogo vidogo katika nchi hii na vimeleta msisimko kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa, wawekezaji wengi kwenye viwanda hivi mtaji wao huo unalenga hapo kwenye milioni 100. Sasa tunapowatoa kwenye eneo hilo tunawapeleka kwenye *turn over* ya milioni 200, lakini tukumbuke kwamba, kwa sababu hawa uwezo wao ni mdogo wamekuwa wakinunua *raw materials* kwenye viwanda ambavyo vyenyewe viko kwenye mfumo wa

*VAT*. Kwa hiyo, *raw materials* watakazonunua itakuwa ni ghali, lakini wao hawapo kwenye mfumo wa *VAT*. Kwa hiyo, hawatakuwa na uwezo wa ku–*recover* kile kiwango cha *VAT* walichokitumia kutokana na kununua *raw materials.* Hapa naona kuna mgogoro, tunaweza kukuta tunaua ukuaji wa hivi viwanda vidogo. Mheshimiwa Waziri waliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka siku zilizopita kulikuwa na utaratibu wa kuruhusu wafanyabiashara wanaotaka kuingia kwenye mfumo wa *VAT,* wakaruhusiwa kwa mpango maalum. Wizara waliangalie hili ili hawa wawekezaji kwenye hivi viwanda vidogo vidogo wanaolazimika kununua *raw material* kwenye viwanda ambavyo viko kwenye mfumo wa kulipia *VAT* wasije wakaathirika na waweze ku–*recover* fedha hizi wanazozitumia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, wakati huo Mheshimiwa Esther Matiko anajiandaa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia bajeti yetu ya trilioni 44 ya mwaka huu. Kwanza, nianze kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake mzuri na kwa kuja na bajeti ambayo inakwenda kutatua matatizo ya Watanzania wengi. Tunampenda Rais wetu, maono yake na dhamira yake ya kuondoa matatizo kwa Watanzania inaonekana wazi na tunamuunga mkono Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, pamoja na Mheshimiwa Hamad Chande, kwa uongozi wao mzuri

wa Wizara ya Fedha na Mipango. Hakika Wizara hii imepata viongozi wenye maono, kazi zao zinaonekana na sisi Wabunge na Watanzania tunawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee vile vile kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara, walioniona mwaka ule wa 2020 wakaamua kunileta Bungeni kwa dhati kabisa ili niweze kuwatetea, kuwatumikia, kulinda masilahi yao na kwa kweli kazi hiyo naendelea kuifanya. Kwa mara nyingine niendelee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara kwa kuweza kuniamini na kazi yao naendelea kuifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na maeneo manne ambayo nakwenda kuchangia. Eneo la kwanza niende kwenye miundombinu na vifaa vya zimamoto hapa nchini. Tanzania ni miongoni mwa mataifa ambayo yamekuwa na Jeshi la Zimamoto ambalo halina vifaa kwa ajili ya kuzimia moto. Yapo maeneo ambayo imewahi kutokea majanga ya moto, Watanzania wanakimbia wanasimama uwanjani wanashuhudia namna ambavyo mali zao zinavyoteketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo la Ngara, kuna wakati tulipata majanga kama hayo, tulilazimika kwenda kuazima helkopita ya kuzima moto kwenye kanchi kadogo. Kwa kweli jambo lile lilituumiza Watanzania na lilitufedhehesha, kwa sababu kama Taifa tuliona kuna haja ya kufanya uwekezaji mkubwa kwenye kuliwezesha Jeshi letu la Zimamoto ili liweze kupambana na majanga ya moto yanapotokea nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hii tumeiona dhamira kubwa ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwasaidia Watanzania ambapo ametenga dola milioni 100 kuiwezesha Wizara ya Mambo ya Ndani iweze kununua vifaa vya kuzimia moto, kama helkopta na magari ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaomba Wizara ya Fedha na Mipango, kaka yangu Mwigulu aende akakope hizi dola milioni 100, atafute mikopo ya masharti nafuu, walete magari

na mimi Ngara kwa kweli naomba niwe wa kwanza kupata gari hili. Maana nimeendelea kuwatetea na nimeendelea kulisemea hili na sasa naona mwelekeo ni mzuri. Tumetenga dola milioni 100 kwa ajili ya kwenda kununua mitambo hii ya kuzimia moto hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili huenda Watanzania wengi hawajalielewa, iko hivi; hakuna mwekezaji wa aina yeyote atakubali kuleta fedha nyingi kuwekeza kwenye nchi ambapo ile miundombinu yake ikipata moto itaungua na kuisha na hakuna vifaa vya kuweza kuzima moto huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huu unakwenda kuongeza *confidence* kwa wawekezaji hapa nchi ambao wataleta mitaji yao, mali zao na mitambo yao na endapo itatokea majanga ya moto tutaweza kuyazima. Hongera sana kwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuliona hili na pongezi nyingine zimwendee Waziri wa Mambo ya Ndani, kaka yangu Hamad Masauni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kwenye kodi ya asilimia mbili ambayo imeletwa kwa ajili ya wachimbaji wa madini. Kodi ya asilimia mbili ku–*introduce* kwa mara ya kwanza kwa ajili ya wachimbaji wa madini nchini ni kubwa mno, ambayo badala ya kwenda kujenga inakwenda kubomoa na pengine wachimbaji wa madini nchini wanaweza kuanza kutorosha madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili eneo la kodi za madini kwanza tuna ada ya ukaguzi ambayo inatozwa tozo ya asilimia moja. Wakati huo huo kuna mrabaha, huu mrabaha ni asilimia sita. Vilevile kuna *service levy, 0.3 percent,* wakati huo huo kwenye kila halmashauri kuna tozo, ushuru mbalimbali wa Mwaro, karasha, viroba na kadhalika. Hii nayo iko *estimated* kama asilimia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kodi hizo ambazo jumla yake ni asilimia 8.3, sasa hivi yamekuja mapendekezo ya kuongeza kodi ya mapato ya asilimia mbili. *Introduction* ya kodi

ya mapato ya asilimia mbili kwa mara ya kwanza ni kubwa. Kwa unyenyekevu mkubwa Mheshimiwa Mwigulu naomba a-*note* hiyo, nimwombe kabisa badala ya kutuletea kodi hii ya mapato ya asilimia mbili, watuwekee asilimia moja. Watujaribu kwanza wachimbaji wa madini tuone kama inatekelezeka hii asilimia moja kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakileta asilimia mbili watu wataona hii asilimia mbili ni kubwa na matokeo yake watu wataanza kupitisha madini kwa njia za panya, watu watajificha. Jamani hivi kweli waliona wapi tuna-*introduce* kodi ya mapato kwa mara ya kwanza tunadumbukiza asilimia mbili yote hiyo? Jumla inakuwa ni asilimia 10.3, *it's a lot*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kabisa kwenye eneo hili, iwe ni asilimia moja pekee itatutosheleza, tui–*test* kwanza kwa mwaka wa kwanza. Mwakani ikienda vizuri waongeze hiyo nyingine iwe asilimia mbili na hapo mambo yatakwenda sawasawa. Naomba eneo hili kwa kweli lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri wa Madini pamoja na Mheshimiwa Rais wamelitendea kazi eneo hili la madini. Mazingira ya uwekezaji kwenye eneo la madini sasa hivi yamenyooka na yako sawasawa. Madini sasa yanachimwa kwenye maeneo ya *TFS* kwa kufuata sheria za nchi, kwa kulipia misistu, kulipia ada ya kukaa kwenye lile eneo na sasa nimeona kuna *initiative* ambayo tumeendelea kuizungumzia ya kumwomba Mheshimiwa Rais aridhie baadhi ya maeneo ambayo yako kwenye *TANAPA* yamegwe yarudishwe kwenye *TFS* ili nchi yetu iweze kuchimba madini kwenye maeneo hayo ili *tax* iendelee kukusanywa kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumwomba Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aridhie yale maeneo mengine ambayo hata sungura hakuna pengine kuna nyoka na ndege, maeneo hayo ayalete hapa Bungeni tuweze kuyaondoa kwenye *TANAPA* yaingie *TFS,* ili Watanzania wachimbe madini waweze kufaidika ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni eneo hili la kuruhusu kuuza mazao nje ya nchi ambalo kwa kweli limeendelea kuongelewa tangu jana na Wabunge wengi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametoa ufafanuzi. Iko hivi, yako makampuni ambayo yameomba vibali vya kusafirisha mahindi, maharage na mazao mengine nje ya nchi. Vilevile makampuni haya yana vibali vyote vinavyowaruhusu kufanya biashara hii kuanzia kusajiliwa *BRELA,* kuwa na *TIN* na vibali vingine ambavyo Waziri wa kilimo amevielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa hakuna sababu ya kusubiri, wanasubiri nini? Nawaomba hawa ambao tayari wana vigezo vyote wapewe vibali. Kama mtu ameomba tani 1000 kama shida ni ku–*restrict,* basi wampe hata tani 200 waaachane na 1000, kwa sababu hatuwezi kusimamisha maisha ya Watanzania, lazima waendelee kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kwenye Jimbo langu la Ngara, jana nimewambia wafanyabiashara wote wanitumie zile nyaraka zao, wote wamesajiliwa na wana leseni. Vile vile, kwa bahati nzuri nimemtumia Waziri wa Kilimo. Nimemtumia Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, nimemtumia Dkt. Kessy ambaye ndiye anayeratibu vibali. Niombe wafanyabiashara wangu wa Jimbo la Ngara, sisi Ngara hatuna njaa, tunalima mara mbili kwa mwaka na mazao ambayo tulishavuna msimu wa kwanza bado yako majumbani. Wanatucheleweshа kufanya biashara kwa sababu kama njaa ziko katikati ya nchi, Wizara waje kununua kwetu, tuwape mazao. Niwaombe Wizara ya Kilimo, makampuni yote ambayo yamekidhi vigezo wawaruhusu waanze kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni makampuni ambayo hayana vigezo na hapa naomba Watanzania wamwelewe Waziri wa Kilimo. Sisi ni Taifa huru, haiwezekani mtu akatoka nchi jirani anaingia Tanzania na gari lake au lori lake, anakwenda kwa wakulima, anaaanza kukusanya mazao, anapakia mzigo anaondoka na anakwenda anawalipa madalali anavusha mzigo, anatoka nje ya nchi bila kulipa kodi haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania kwenye eneo hili tumemwelewa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, aendelee kuwabana, lakini wale Watanzania ambao wameshakidhi vigezo, Waziri wa Kilimo awaruhusu waweze kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi lingine la *sorrow proprietors,* ni Watanzania ambao wameendelea kufanya biashara hiyo bila kuwa na makampuni au kusajiliwa *BRELA*. Naomba hawa nao waweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisaba, kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, wakati huo Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu wanajiandaa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa fursa ya kuchangia pamoja na kwamba siko vizuri kiafya, lakini nitajitahidi kuchangia kwa kadri nitakavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nitakwenda kuainisha kwa nini natoa pongezi zangu kwa mwanamama huyu ambaye ni Rais wa kwanza wa kike Tanzania. Kwanza kabisa, sote tunajua mazingira yaliyotokea Tanzania ambapo tulipotelewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Hayati Magufuli na akawa ameacha miradi mingi ya kimkakati ambapo wengi wetu walibeza labda nafikiri kwa sababu ya jinsia yake. Hata hivyo, mama ameweza kuendeleza miradi hii kwa ufanisi mkubwa sana pamoja na kwamba kuna kuyumba kwa uchumi duniani lakini Mama ameweza kuhakikisha kwamba miradi yote inaenda na kwa ufanisi mkubwa na haya ni maendeleo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, sote tutakubaliana kwamba Mama amehakikisha kwamba analeta demokrasia

nchini. Ameweka uhuru wa mtu kujieleza iwe anatoa mawazo chanya au mawazo hasi, bado kila Mtanzania yuko huru kuweza kutoa mawazo yake. Tumeona hata sisi wa vyama vya upinzani tumepewa nafasi hata ya kuweza kufanya mikutano ya hadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, kwa mara ya kwanza Rais ambaye kwa wenzetu ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ameweza kuhudhuria Kongamano la Kitaifa la BAWACHA, la chama pinzani na wakati huo ilikuwa ni siku ya Kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani akaweza kuacha Chama chake akaenda. Kwa kweli hii inajenga *confidence,* sio tu kwa vyama vya upinzani lakini pia hata kwa wawekezaji. Vile vile, hata kwa mataifa mengine tumeona uhusiano umekuwa ni chanya sana. Kwa hiyo hii pia inaweza kujenga *confidence* na watu kuja kuendelea kuwekeza Tanzania na hivyo kuweza kuona maendeleo yanatamalaki. Kwa hiyo, nimeona lazima nimpe *credit* hii Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipitia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kwa kweli naiunga mkono na naiomba Serikali iweze kuchukua mapendekezo yote ambayo yameainishwa kwenye taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti. Siwezi kuyasema yote kwa sababu muda ni mchache, lakini tumeona yameainishwa kwamba hata utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023 ambapo tulitenga fedha trilioni 15.1 mpaka kufikia mwezi wa nne ambayo ni *quarter* ya tatu tayari zilikuwa zimeenda shilingi trilioni 11.5. Ina maana kwa fedha zilizotolewa kwenda kwenye matumizi ya maendeleo mpaka tunakwenda kumalizia ni rai yangu itakuwa pia imefikia kwenye zaidi ya asilimia 80 au 90 kwa sababu sasa hivi ni asilimia 76.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tukija ku–*discuss* hapa wakati wa bajeti unakuta hata asilimia 50 ya

utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo haujafikia. Kwa hiyo, hii ni *credit* ya kuona kwamba Rais ana dhamira ya dhati ya ku-*push* maendeleo kwa wananchi. Pia unaweza ukaona hata kuna miradi mbalimbali ya kimkakati imeelekezwa kwenye elimu, afya, maji ambayo kwa kweli ni *tangible* na unaweza ukaona. Hata ukikaa ukawa unashawishi Watanzania watoe kodi wanatoa wakiona kuna vitu vinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaweza wakakaa kama wanafanya *analysis* ya kina waka–*compare* utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka huu na miaka mingine ya nyuma, *then* watumie kama *basis* ya kuweza kushawishi Watanzania. Kwa kweli hii hata wale ambao wako *responsible* kuhakikisha kwamba wanatangaza yale mema yaliyofanyika *you are not doing your job well*. Wakifanya vizuri na kuainisha watajenga *confidence* kwa Watanzania waweze kulipa kodi, waweze kwenda kununua vitu au bidhaa na kuhakikisha kwamba *they pay* na kuomba risiti kwa sababu wanaona *service delivering* zinavyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hata kwenye Sekta ya Afya, sasa hivi niko kwenye Kamati ya *PAC,* nimetembelea miradi tumekwenda Mtwara na kwingineko, unaona hizi hospitali za rufaa na vifaa vya kisasa ambavyo vimewekwa. Ukienda unaona kabisa kuna hospitali za mikoa zimejengwa, hospitali za wilaya zimekarabatiwa. Kwa hiyo, *for the first time* baada ya miaka sita tumeona ajira zimetolewa kwenye utumishi wa afya ingawa bado ni kidogo sana elfu nane mia tisa na kitu, *it's a credit, so we need to compliment this* na kushawishi Watanzania waendelee kutoa kodi kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pia kwenye sekta ya elimu *the same thing applied* tunaona *VETA* kila wilaya zinajengwa. Haya ni maendeleo, ukiwekeza kwenye elimu ndio unaweza kwenye uchumi wa Taifa letu. Tumeona shule za sekondari za wanawake za sayansi. Tumeona pia kuna miradi mingi ya shule inajengwa huko na imepunguza hata adha ya wananchi kuchanga. Sasa haya yote ukieleza mwananchi ataona kweli nikinunua kitu kwa shilingi elfu kumi natakiwa nipewe risiti yangu ili ile kodi iende ikaendeleze maendeleo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, watendaji wa Serikalini na Mawaziri, *sell out these things* ambazo zinafanyika ili watusaidie Watanzania waweze kutoa kodi. Hii kodi ambayo tunakusanya sasa hivi na tunajisifia *TRA it is just a peanuts* nawaambia. Tukiwekeza na tukaondoa mianya yote ambayo inapotea kwa *TRA,* watu wakalipa kodi kwa asilimia zote, tutapata hata trilioni 60. *This is the second time I am saying this in this House*. Malipo yanayopatikana kupitia *TRA it's just a peanut*. Tuelimishe umma, tuzibe mianya ya utakatishaji wa fedha. Tuhakikishe kila Mtanzania au kila mtu anayefanya kazi Tanzania analipa kodi kwa uhalisia, tutampunguzia hata *burden* Mheshimiwa Rais kwenda kuomba nje. Tutapata fedha ndani ya nchi, tutawekeza kimkakati na tutaleta maendeleo *and this is what we are seeking for.*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye maji na umeme, mimi mpaka kule kijijini kwa Mzee Matiko tuna umeme na tuna maji. Ila sasa nitoe *warning,* zile takwimu wanazozitoa sasa hivi kwa mfano, wakisema maji vijijini asilimia 77 na mjini asilimia 88, ni kweli yamefika kwenye *center.* Sasa ni wajibu wa Serikali kwenda kuwekeza kuhakikisha kwamba wanasambaza maji, mtandao wake unafika kwa wananchi wote kwenye mitaa na vijiji vyote. *Equally* wanasambaza umeme unafika kwenye vitongoji na mitaa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kwa Mkoa wa Mara, ukipitia *statistics* inakwambia vijiji vyote vimepata umeme, lakini kuna vitongoji bado havijapata na wananchi hawana umeme. Kwa hiyo, tunafikaje hapa? Ni kwa kuhakikisha kodi zinapatikana kwa kina ili miradi hii iweze kusukumwa na wananchi waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nihame kwa sababu muda ni mchache sana niende kwenye Magereza. Kuna siku niliongea hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha akaniita mimi ni balozi wa hawa Maaskari na kwa kweli nitaendelea kuwatetea. Askari wetu

wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Mimi ni shahidi kwa sababu nimewahi kuishi huko, walinipeleka nikaishi huko. Kwa hiyo, nikawa naona vitu vingine ambavyo nimeviona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Askari Magereza wametumikia nchi zaidi ya miaka 26 na narudia hii tena na hata Mheshimiwa Rais alisema, unakuta Mtu anastaafu yuko kwenye *Staff Surgent* ni kwa sababu ya mazingira ambayo sio rafiki ya kuwahakikishia hawa Watanzania wanaojitoa wanapandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna Askari Magereza anakaa zaidi ya miaka mitano wakati utaratibu unasema kila baada ya miaka mitatu wapandishwe cheo lakini unakuta anakaa zaidi ya miaka mitano hajapandishwa cheo bado yuko kwenye *Staff Surgent,* ameshatumikia zaidi ya miaka 26 anamaliza katika cheo hicho, kwa hiyo, tunaomba sana mhakikishe kwamba hao Askari Magereza wanapandishwa na Maaskari wengine wote wapandishwe vyeo kulingana na inavyotakiwa. Maaskari ikitokea mfungwa amekimbia anapigwa faini ya kutopandishwa cheo miaka mitatu, halafu anakatwa nusu mshahara mbaya zaidi huo mshahara unaokatwa unapelekwa sijui kwenye mfuko maalum wa Kamishna wa Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hii hela anayokatwa ya mshahara wake unaenda kwenye mfuko maalum wa Kamishna wa Magereza inakuwa *accounted* vipi? Naomba wakati Mheshimiwa Waziri unakuja hapa utueleze inakuwa *accounted* vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanadai madeni kwa miaka mingi hawajalipwa, tunaomba walipwe madeni yao, pia muwatoe utumishi muwapeleke kwenye *consolidated fund* kama wengine, yaani hao Magereza mnawaonea sana, hata mishahara yao ni tofauti na Majeshi mengine ambayo yako kwenye Idara hiyohiyo ya Mambo ya Ndani, muweze ku-*revisit* muwatie moyo. Hawa watu wanakaa na wale watu tunaowapeleka kama Magaidi, hawa watu wanakaa na watu wa tabia mbalimbali lakini wanaangalia *at a high risk,*

msipoangalia vizuri ndiyo wanaweza kuongeza vishawishi vya kufanya mambo mengine ambayo hayatakiwi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kuweza kupandisha mapato tumeona upotevu. Mwenzetu alisema hapa kwamba waweze kutoa motisha, hizi *EFD* zinatolewa alisema waweze kukaa kwenye mambo ya simu, mimi nilikuwa na-*suggest* kama tutaweza tunaona hii kwa mfano ukipata risiti unakuta kuna wakati mwingine umewekewa *token* pale, labda siku nyingine ukienda ukalipa unakuta una laki moja na milioni moja na milioni mbili watu watakuwa wanashawishika kuomba risiti wakijua wanaweza wakabahatika wakapata hiyo *token* ambayo unakuta imeandikwa kwenye risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine naomba sana soko la kimkakati la Lemagwi liweze kujengwa kule Tarime ambalo litasaidia, leo tumeona malori mengi yamerundikana kule Sirari, hili soko likijengwa na Mheshimiwa Bashe aliahidi hapa kwamba masoko ya kimkakati ambayo yako pembezoni kwenye maeneo yote yaweze kujengwa, litasaidia kuweza kuuza mazao yetu pale watu wa Kenya watakuja upande wa pili ina *multiply effect,* uchumi utabaki Tanzania. Tunaomba sana mnipe majibu hili soko linaenda kukamilika lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni uwanja wa ndege katika kukuza utalii wetu. Mheshimiwa Rais ametangaza *Royal Tour* na tumeona kwamba Utalii walau umeongezeka lakini bado tuko chini sana, siwezi kupita takwimu nadhani muda umeenda. Kama vile tu baada ya *Royal Tour* ya Rais, utalii umeongezeka zaidi ya asilimia 190 kwa ndani na kwa watalii wa nje zaidi ya asilimia Hamsini na kitu na mapato yame-*trip* yameenda zaidi ya asilimia tisini na kitu huko, tunaomba muwekeze kuhakikisha kwamba kwanza mnavitambua vivutio vya utalii, mnavitangaza, mnaweka vivutio vya kikodi. Tanzania tulitakiwa tuwe na *turn out* ya kuchangia, yaani utalii uchangie kwenye Pato la Taifa kwa fedha nyingi sana, pia utatangaza vivutio vingi. Utalii ungekuwa ni moja ya kitu cha kutuingizia fedha za kigeni, tukiwekeza dola moja

kwenye utalii tutavuna zaidi ya dola kumi na hatuta *regret,* tukifanya hivi tutarnda kuongeza mapato ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeangalia kwenye kingine.. *ooh my god!* cha kumalizia sasa maana naona hata karatasi zangu nimezi-*arrange* zimeenda ndivyo sivyo.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi subiri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kujengewa uwanga wa ndege Mugumu uweze kukuza utalii lakini pia kuhakikisha kwamba barabara zinazopita kwenye mbuga zetu zile ambazo zinapita kuunganisha Mkoa na Mkoa ziweze kujengwa hata kwa lami nyepesi tuangalie na wenzetu wanafanyaje, ile barabara iliyopo pale siyo rafiki hata kwa utalii kuwa *attracted.* Kwa hiyo, tunaomba sana tukifanya haya mambo na tukatoa fedha za kutosha kwenye Mamlaka zote ambazo ziko chini ya Maliasili na Utalii tunaenda kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni fedha kuweza kupanga ardhi yetu. Ni aibu kwa kweli kwa Taifa letu kuona kwamba baada ya uhuru sasa hivi kwamba vijiji 2,600 tu ndiyo vimepimwa, zaidi ya vijiji 12,000 havijapimwa, tukipima ardhi yetu tutakuwa na mpango mzuri wa kujua mifugo inafugwa wapi, kilimo ni wapi, uvuvi ni wapi na tukiwekeza kwenye uvuvi nilikuwa nimesahau, naomba dakika mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika mbili tu. Sasa hivi eti sekta ya uvuvi inachangia trilioni 1.8 kwenye Pato la Taifa. Uvuvi ambapo tuna bahari, tuna maziwa, nilitaka kuyataja hapa lakini tu muda umeenda, tunachangia asilimia 1.8 kwa Pato la Taifa ambapo kwa mwaka uliopita tunasema ilileta zaidi ya trilioni tatu. Tukiwekeza kwa kina kwa vifaa vya kisasa uvuvi utaenda kuleta zaidi ya trilioni saba trilioni kumi na tutakuwa hatuna hata bajeti tegemezi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Nilimwita Mheshimiwa Palamagamba Kabudi na wakati huo Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, anajiandaa.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim, kwa ruzuku ya uhai na afya ambayo imeniwezesha kuja kutoa mchango wangu. Aidha, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango na mimi nianze kwanza kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti lakini kwa kasi kubwa ya maendeleo ambayo tunayaona katika nchi yetu, ikiwa ni pamoja na kuendeleza miradi ya kielelezo na miradi mikubwa lakini pia ustawi wa wananchi unazidi kukua katika nyanja zote chini ya uongozi wake mahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati kabisa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Katibu Mkuu Dkt. Dr. Natu El-Maamry Mwamba na Naibu Makatibu Wakuu kwa bajeti hii mwanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba katika bajeti hii Jimbo la Kilosa katika miradi mikubwa tumewekwa, ikiwa ni pamoja na kujenga barabara ya kutoka Kilosa kwenda Mikumi pia kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa daraja kubwa la Mto Mkondoa. Ni imani yangu kwamba fedha hii itapatikana katika mwaka huu wa fedha na ni miradi hiyo kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia kuhusu umuhimu wa sekta ya nyuki na hasa katika mazao yake ikwemo asali katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kuipatia nchi yetu fedha za kigeni. Tanzania ni nchi ya pili kwa kuzalisha asali nyingi katika Bara la Afrika, nchi ya kwanza ni Ethiopia, Tanzania ni ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndiye *supplie*r mkubwa wa asali na mazao ya asali kama vile Nta kwenye soko la Umoja wa Ulaya kutoka Afrika *(European union)*. Inakadiriwa kuwa

Tanzania inauza nje wastani wa tani 770 za asali na tani 283 za Nta kwa mwaka. Aidha, inakadiriwa kuwa sekta ya ufugaji nyuki na mauzo yake yanaleta wastani wa dola za Kimarekani 5,182,126 kwa mwaka katika miaka minane iliyopita kila mwaka hizo fedha ziliingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inaajiri na kuhusisha takribani watu milioni mbili waishio vijijini katika maeneo mbalimbali hususani Tabora, Singida, Katavi, Morogoro kule Kilosa. Mfano kule Singida kuna Kijiji cha Nyuki na Jiji la Nyuki. Pia Kilosa Kata za Maguha na meneo Unone katika Kata ya Ludewa wote wanafanya shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ina uwezo mkubwa wa kukua na kuongeza mapato ya nchi kwa kuuza asali na nta na mazao mengine nje ya nchi. Tunaweza tukauza vumbi yaani *pollen,* tunaweza tunaweza tukauza *royal jelly* yaani maziwa ya nyuki. Hata hivyo, sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi hasa inapokuja katika kuuza asali na nta nje ya nchi. Kikwazo kikubwa au changamoto kubwa ni urasimu mkubwa na fomu nyingi na nyaraka nyingi ambazo wale wanaouza asali nje ya nchi wanatakiwa kuzijaza na kila unapojaza iwe ni nyaraka au ni fomu lazima wanatozwa, wanalipa tozo. Kwa hiyo, eneo hili pia lina tozo nyingi takribani 30 katika hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba wanaweza kuuza asali nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania wanajaza fomu 31 ukilinganisha na nyaraka sita Rwanda, matokeo yake asali yetu nyingi msimu huu wa kurina asali ukifika maeneo kama Itigi, utakuta malori mengi yanakusanya asali inakwenda Kenya na ikifika Kenya itauzwa nje kwa jina la Kenya, moja ya sababu kubwa ni urasimu huu na tozo nyingi ambazo zimewekwa katika sekta hii hasa kwa wale ambao wanataka kuuza asali yao nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mtu anayetaka kusafirisha asali nje anatakiwa aende kwenye taasisi nyingi na akienda kwenye taasisi hizo mifumo yao haisomani. Kwa hiyo, anajikuta taarifa ambazo ametoa kwenye Taasisi moja inabidi taarifa hizohizo

azirudie kwenye Taasisi nyingine. Anatakiwa aende kwa Wakala wa Misitu *(TFS)*, anatakiwa aende *TCCIA* apate *Certificate of Origin*, anatakiwa aende *Veterinary* ili ahakikishiwe kwamba nyuki waliotoa hiyo asali walikuwa ni salama, anatakiwa aende Tanzania *Atomic Energy Commission,* anatakiwa aende *TASAC* anatakiwa aende *TRA,* anatakiwa aende *TBS,* anatakiwa aende *TPA* na hao wote mifumo yao haisomani na matokeo yake tunapoteza ufanisi wa kupeleka asali nyingi nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyohuyo anayepeleka asali nje anajikuta anatakiwa kupata aina hiyohiyo ya cheti au ruhusu au *payment* kutoka sehemu mbili tofauti lakini juu ya jambo hilohilo. Kwa mfano, anatakiwa aende *veterinary* ili apewe *sanitary certificate* ya kutoa ushahidi kwamba nyuki aliyetoa asali hiyo alikuwa salama, halafu anatakiwa aende Wakala wa Misitu ili apate *sanitary certificate* ya kuonesha kwamba asali hiyo ni salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza fomu hizi zipitiwe upya tukilinganisha na za wenzetu nchi ya Rwanda, Kenya na Uganda ili tuwe na ufanisi na tija zaidi katika kupeleka mazao haya ya asali. Mimi nina uhakikia kabisa tukiboresha mifumo yetu, tukitoa hamasa kwa watu mbalimbali na sekta binafsi kununua, kuchakata na kuuza asali nje, tunao uwezo kwa mwaka kuingiza dola milioni 20 kutokana na asali na mazao ya asali kama nta na *royal jelly*. Wote tunafahamu kabisa *royal jelly* ina bei kubwa sana na faida kubwa tuliyonayo sisi maeneo yetu ambayo tunafuga nyuki maeneo haya mengi hayana mazao yanayotumia viuatilifu au mbolea, maana yake asali hii ni *organic* na ina uwezo wa kuwa na bei kubwa katika masoko ya Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu Mheshimiwa Waziri tupitie tena zile fomu kutoka 30 tuzipunguze ikiwezekana zifike tisa kama ilivyo kwa Rwanda. Pia tupunguze tozo katika sekta hii, nashauri pia tutoe fedha ya kutosha ya kuwahamasisha wafugaji wa nyuki katika maeneo mbalimbali, Tabora, Singida yote Itigi na Manyoni lakini Kilosa na maeneo mengine yoyote yale ili wananchi wetu waweze kuwa na mizinga

ya kisasa ya kufuga nyuki lakini yenye ubora na tukusanye asali hiyo na tuichakate na kuuza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili naomba kupongeza Serikali kwa hatua ya kuondoa ushuru wa bidhaa unaotozwa kwa magari yanayotumia nishati ya umeme ambayo yamo katika hotuba ya bajeti ukurasa wa 107 na 108. Kwa mujibu wa ripoti ya *Africa E-Mobility Alliance* inaonyesha kuwa Tanzania kuna *electric vehicles,* yaani kwa maana ya magari, pikipiki, bajaji skuta 5000 na sisi ndiyo tunaoongoza katika eneo hili la Afrika Mashariki kwa kuwa na hizi *electric vehicles* nyingi, pia tunazo kampuni karibuni kumi ambazo zinaagiza aina hii ya magari. Kwa hiyo, kuondoa ushuru wa bidhaa katika eneo hili utaongeza kuingizwa nchini kwa magari mengi, pikipiki nyingi na skuta nyingi ambazo zinatumia umeme badala ya mafuta na hivyo kutunza mazingira lakini pia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili Tanzania tumefika mbali na mambo haya wakati mwingine hatuyasemi, sisi ndiyo nchi pekee katika Afrika Mashariki ambayo tunayo kampuni ambayo sasa inabadili magari haya ya mafuta kuwa magari yanayotumia umeme. Kampuni hiyo ni Kampuni ya Hanspaul ipo pale Arusha na wao wanashirikiana na kampuni ya Ufaransa na Kampuni ya *Gardy Electronics,* hawa sasa wanabadili magari yanayotumia mafuta kwenda kuwa katika mfumo wa umeme na wamejenga vituo vya kuongeza umeme vinavyotumia *solar* katika sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kuwa jitihada hii ipewe musukumo ili tuweze kuanza kutengeneza magari ya umeme sisi wenyewe ndani ya nchi yetu. Tumejaliwa kuwa na madini yote ya kimkakati ambayo yanahitajika katika magari ya umeme *Nickel, Cobalt, Lithium* pamoja na *Graphite*, kwa hiyo, hatua hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia Chuo cha Ufundi cha Arusha kipewe fedha zaidi, kwa sababu ndiyo chuo ambacho kimeanza kufundisha mafundi wa kuhudumia magari haya ya umeme, kuyatenegeneza magari haya ya umeme na

wakitoka katika kuhudumia magari haya ya umeme na kuyatengeneza magari haya ya umeme waende sasa kwenye kuunda magari ya umeme, pikipiki za umeme, skuta za umeme na vitu vinavyotumia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu mara nyingi Watanzania tunafanya vitu vikubwa sana lakini ni wazito wa kuvitangaza, ni wazito wa kuvieleza. Kwa hiyo, niwapongeze sana *Hanspaul Group,* na wengine, pia Chuo cha Ufundi Arusha kuingia katika sekta hii ya magari ya umeme. Dunia ya sasa inahama kutoka kwenye magari ya mafuta kwenda kwenye magari ya umeme na magari yanayotumia Gesi asilia. Tanzania tuwe ndiyo nchi inayofanya mambo yote hayo kwa kasi kubwa sana. Nchi za jirani zinakuja kubadili magari yao ya mafuta kuwa magari ya umeme kwa ajili ya utalii na duniani zinatangazwa kwamba magari yale yametengenezwa katika nchi zao kumbe magari hayo yote yamekuja Arusha yamebadilishwa na kuwa magari ya umeme lakini dunia inafahamu kwamba magari hayo yametoka kwenye nchi hizo. Kwa hiyo, ninapendekeza tuseme kwa sauti kubwa kwamba shughuli hii inafanywa Tanzania pia tuwape hawa wanaofanya kazi hii motisha mbalimbali ikiwa ni pamoja na hii hatua ya kufuta au kuondoa huu ushuru wa bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ningependa kulizungumzia ambalo pia tuwekeze katika hilo, tuwekeze katika haki miliki ya umahususi wa kijiografia yaani *geographical indications.* Maeneo hayo tuyatumie kuuza bidhaa ambazo zinatoka katika maeneo hayo. Moja ya mazao ambayo tunaweza tukayatangaza kwa bidii kubwa sana ni Kakao. Kakao ya Kyela ina ubora mkubwa sana duniani na inatumika kuchanganya na kakao hafifu kutoka nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja na kakao hii, kakao hii inauzwa Ufaransa, ili kuonesha kwamba Kakao hii ya Tanzania ina thamani kubwa ndiyo maana wanaonyesha kwamba asilimia 75 ya kakao katika *chocolate* hii imetoka Tanzania, imetoka Tanzania kwa sababu ina ubora mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiishie tu katika hayo pia tuanze kutangaza kutumia umahususi wa kijiografia wa mazao mengine ya kilimo ili yapate bei ya juu. Kwa mfano, Kahawa ya Mbinga ndiyo kahawa inayolimwa bila kutumia mbolea ni *organic*. Kahawa ya Manyovu na hivi vyote vitatusaidia siyo tu kupata fedha ya kigeni lakini kuitangaza nchi yetu kwamba ina bidhaa za ubora wa hali juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchele wa Kyela, mchele wa Kilombero na sasa kuhusu Mvinyo wa Dodoma. Mvinyo wa Dodoma una ubora mkubwa sana duniani, ndiyo maana mvinyo wa Dodoma unachukuliwa na nchi nyingine kwenda kuongeza ubora wa mivinyo yao ambayo ni hafifu. Kwa hiyo, ni wakati sasa wa nchi yetu kuwekeza pia katika maeneo hayo ambayo yanaonekana siyo muhimu lakini duniani ni muhimu sana, hatimiliki ya mazao yote yenye umahsusi wa kijiografia yaani *geographical indicators. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja katika bajeti hii mwanana na bora sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilimuita Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu wakati huo Mheshimiwa Benardeta Mushashu, anajiandaa.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa asubuhi ya leo na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024. Nami nianzae moja kwa moja kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema, pia nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wasaidizi wake wote hususan Wizara hii ya Fedha inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Naibu Waziri Chande na Katibu Mkuu Dkt. Natu na watendaji wote kwa kuwasilisha bajeti nzuri ambayo imeonesha Serikali hii namna gani ilivyokuwa sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ya Bunge hili, tunafanya kazi kwa karibu na Wizara ya

Fedha na Taasisi mbalimbali. Tumeona mambo mengi kama tulivyoainisha kwenye taarifa yetu na nimpongeze Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Sillo kwa kuwasilisha vizuri, tumekutana na wadau mbalimbali, mapendekezo mengi yameingia kwenye bajeti ya mwaka huu na hatua mbalimbali za kikodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwa usikivu huo tulishauri iwepo Tume ya Mipango, Tume ya Mipango Sheria yake imeshapitishwa, tulishauri mapitio ya Sheria ya *PPP* imeshapita, tulishauri mifumo ya makusanyo ya mapato, Serikali imeboresha kupitia TAMISEMI imekuja na mfumo wa TAUSI, pia imekuja na Mfumo wa Manunuzi ya Umma ambayo imeboreshwa na ipo mbioni kuleta Sheria ya Manunuzi ya Umma, yote haya yanaonekana namna gani Serikali yetu ilivyo Sikivu, nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo leo tunajadili bajeti ya trilioni 44, ni kiwango cha juu kabisa tangu tumepata uhuru wa nchi yetu, lakini inaonyesha namna gani Serikali hii inajiamini kwamba itaweza kufikia kukusanya trilioni 44 na kutumia trilioni 44, na mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ninaamini uwezekano huo upo, kwa sababu kati ya trilioni 44 inatarajia mapato ya ndani kukusanya trilioni 31. Nikiangalia mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani kuanzia tu mwaka 2020/2021 ilikusanya trilioni 20 ikaja 2021/2022 trilioni 25 na mwaka huu unaoendelea wanatarajia Serikali kukusanya trilioni 27. Kwa hiyo, ni wazi trilioni 31 na hatua mbalimbali za kikodi walizopendekeza zinaweza kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba naiunga mkono Serikali inapokuja na mipango mingine ya kuongeza mapato. Ukiangalie umbile la bajeti, Serikali kwa shilingi trilioni 31 tu ya mapato ya ndani, lakini ina dhamana ya kulipa shilingi trilioni 10 mishahara tu na hii ni ongezeko la zaidi ya trilioni tatu kwenye mishahara, ina maana ajira mpya, ongezeko la mishahara na upandishaji wa madaraja. Naipongeza sana Serikali, lakini ina dhamana ya kulipa madeni shilingi trilioni 10 na sio madeni yaliyochukuliwa na pengine na Awamu ya Sita ni awamu

mbalimbali, kwa hiyo, ina dhamana hiyo. Maana yake kuna kuwa na tofauti ya shilingi trilioni 13. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naipongeza Serikali kwa mipango mbalimbali ya kuongeza mapato na hapa mahsusi niendelee kuiomba Serikali tumepitisha azimio hapa *IGA* kwa ajili ya masuala ya bandari, naomba Serikali mchukue muda haraka mje na mikataba yenyewe, muendelee kuingia mikataba ili mwekezaji yule aje bandarini ili bandari iwe na nafasi ya kuchangia kwenye pato la Taifa, kwenye mapato ya ndani ili Serikali ipunguze kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa naishukuru Serikali imepunguza kukopa kwenye vyanzo vya biashara, imejielekeza kwenye mahusiano ya kidiplomasia na ndio maana tumepata tena shilingi trilioni nane kupitia kwenye Benki ya Dunia kwenye mikopo ya masharti nafuu ambayo haina riba na haya yote ni kutokana na mahusiano ya Mheshimiwa Rais na nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimpongeze na uimarishaji wa demokrasia ndani ya nchi yetu. Nataka pia niweke rekodi sahihi Kamati ya Bajeti hakuna mahali ambako tumekuwa na mashaka na matumizi ya mikopo kwenye miradi ya maendeleo. Tulichosema ni kushauri kwamba watizame kwenye yale matumizi ambayo hayaendi kwenye *asset* pengine wapunguze matumizi yale ya kawaida ambayo ni ya msingi yajielekeze kwenye sekta za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naipongeza sana Serikali nataka niseme pamoja na mjadala unaoendelea kwamba kwa nini; kuna kiongozi namuheshimu sana, anasema kwa nini Wabunge hatukuitwa jina moja moja kupiga kura, lakini nataka nimwambie yeye amekaa humu ndani ya Bunge miaka kumi, utaratibu wa kupiga kura ya kuitwa mmoja-mmoja ni kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali, lakini masuala mengine yote tu ni kwa utaratibu wa kuhojiwa na tulihojiwa na ndio maana tulisema kura ya ndio kwa wingi na ndio maana azimio lile limepita kuipa Serikali

sasa muda wa kuendelea kuingia mikataba moja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimkumbushe Profesa Tibaijuka alipokuwa Waziri mwaka 2013 aliwasilisha mpango wa kuifanya Mji wa Kigamboni kuwa Mji wa Kigamboni mpango wa shilingi trilioni 11 ndani ya Bunge ambao haukufanikiwa na tuliupitisha kwa kura hizi za kuhojiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo aiche Serikali inayoongozwa na mwanamama mwenzie ambayo imefanya mambo mengi na yeye akiwa mwanaharakati. Kwa namna ambayo Serikali imeingia madarakani, Mheshimiwa Rais Samia na kurithi miradi mikubwa mikubwa zaidi ya shilingi trilioni 21 *SGR* zinatakiwa, zaidi ya shilingi trilioni sita kwa ajili ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, zaidi ya shilingi bilioni 700 kwa ajili ya Daraja la Busisi na mabilioni na pesa nyingi, hakuna namna yoyote, lazima tutafute vyanzo vingine vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo bandari haiwezi kuwa tunasema inauzwa kwa kusema mwekezaji atachukua gati namba *zero* mpaka saba, sisi Serikali tutabaki na gati namba nane, tisa, kumi, kumi na moja; huo sio uuzaji kwa lugha tu ya kawaida, ni lugha ya kushirikisha sekta binafsi, lakini tumeiona dhamira ya Serikali kwenye bajeti ya mwaka huu imeandaa mazingira ya kurejesha *export credit guarantee scheme,* zaidi ya shilingi bilioni 800 imetenga kwa ajili ya kuwawezesha wazalishaji wa mazao waweze kuuza nje, lakini ili kuweka fedha za ndani za kigeni nataka kusema Bunge tulitimiza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niishauri Serikali imetambua kwamba vipo vikwazo mbalimbali kupitia utekelezaji wa *blue prints* taasisi za udhibiti kila taasisi inakuja na adhabu, tozo zake kaukaguzi, kwa kuwa imegundua inakuja na mfumo wa dirisha moja la malipo ya tozo mbalimbali na hili sisi tulilipata kwenye Kamati ya Bajeti. Chama cha Wafanyabiashara Wanawake; wanawake misingi yao si mikubwa lakini kwenye taasisi zetu hizi mfano OSHA wanatoza shilingi 1,200,000 kwa

biashara mpya. Wana mafunzo kwa shilingi 300,000; wana *certificate* ya afya kila mfanyakazi shilingi 200,000; wana *booklet* sijui *material* shilingi 360,000; ukienda *TBS* tozo hizi ni nyingi kwa biashara ndogo ndogo. Serikali mmeliona namba mlisimamie kuanzia sasa kama mlivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili niipongeze kwa namna ambavyo mmefanya maboresho kwenye sekta ya utalii, kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye masuala ya uuzwaji na ukodishaji wa vifaa mbalimbali vya ndege ambavyo vinakwenda kuunga mkono kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais juu ya masuala ya *Royal Tour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba Serikali muangalie vyanzo vingine. Tuna vivutio vingi natoa mfano, kwa mfano Wilaya yetu ya Mafia kuna samaki mkubwa duniani hajapata kutokea, lakini bado hatujaona taratibu za kuweka kukuza utalii kupata vyanzo, lakini uwanja wetu wa ndege wa Mafia bado haujawekewa taa.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iiangalie ili Mafia iweze kutoa mchango mkubwa katika sekta ya utalii, lakini sambamba na hilo Serikali ilifanya vizuri kuwekeza shilingi bilioni 90 kwenye miundombinu mbalimbali kwenye sekta ya utalii. Naiomba Serikali ule mpango wa kuanzisha kampuni ya kuweza kudhibiti au kusimamia matumizi ya mitambo iliyonunuliwa kwenye mbuga zetu mbalimbali ifanye haraka ili kampuni hiyo ianze kazi, lakini kana kwamba haitoshi pia naipongeza Serikali katika masuala mazima ya marekebisho ya sheria kama balozi wa kodi, kupunguza viwango vinavyotozwa kwenye makosa ya kutotoa risiti na ya kutodai risiti ili kuhakikisha kwamba wanatii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Watanzania tuendelee kudai risiti na kutoa risiti. Kuna vyanzo vimependekezwa hapo, shilingi 100 kwenye mafuta, lakini pia shilingi 20 kwa kila kilo 20 ya mfuko wa *cement*. Yapo maneno yanasemwa yataongeza ugumu wa maisha lakini nataka niwaambie Watanzania hakuna namna ambavyo Serikali itapata shilingi trilioni 13 kupeleka

kwenye miradi ya maendeleo bila ya kodi, lakini kama tunataka tupunguziwe vyanzo mbalimbali vya kodi lazima tudai risiti na tutoe risiti na sababu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, ni dakika kumi kumi, kwa hiyo muda ukikaribia ni vizuri pia ukawasiliana na kiti kwa ajili ya kuendelea mtu mwingine. Nilimwita Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu wakati huo Mheshimiwa Salome Makamba anajiandaa.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu, Naibu Waziri Mheshimiwa Chande, Makatibu Wakuu kwa bajeti nzuri, bajeti kubwa ya shilingi trilioni 44.38 ambayo ina wagusa Watanzania wote, inaleta matumaini mapya. Kwa kweli Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Chande mnafanyakazi nzuri sana ya kumshauri Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa na mazuri ambayo yanayoendelea kufanyika ndani ya Tanzania. Tunaona kwamba uchumi unaendelea kukua na kwa kutambua kwamba Watanzania wengi ni wakulima tumeona kwa jinsi gani bajeti ya kilimo ambavyo imekuwa ikipanda kila mwaka, lakini vilevile imekuwa ni tatizo na watu wengi wamelizungumzia. Sasa hivi Serikali imekubali inaenda kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vya kati, hawa ndio wataalamu

tutakaohitaji katika viwanda vyetu, lakini hawa watoto au wanafunzi watapata stadi zitakazowawezesha waweze kujiajiri na hivyo tutakuwa tumepunguza tatizo la ajira katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya CCM kwa kuwajali watu wenye ulemavu kwa sababu nimeangalia kwenye bajeti hii ukurasa wa 10 unasema Serikali inaenda kutenga shilingi bilioni moja, iwekwe kwenye mfuko wa watu wenye ulemavu ili waweze kuweza kupata vile vifaa wanavyohitaji, Mheshimiwa Waziri bajeti ni nzuri hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda leo nitaongelea kitu kimoja tu; na nitaongelea Mkoa wa Kagera na umaskini ndani ya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera ni maskini, lakini kwa fursa zilizo Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kagera haupaswi kuwa maskini, Mkoa wa Kagera una ukubwa wa kilometa za mraba 35,686, una idadi ya watu wanakaribia milioni tatu, una mvua misimu miwili kwa mwaka, una wasomi kibao, umepakana na nchi jirani nne, lakini mkoa bado ni maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa za mwaka 2022 pato la mwananchi mmoja mmoja kwa kigezo hicho Mkoa wa Kagera ni mkoa wa mwisho katika Tanzania Bara kwa umaskini, lakini kwa miaka zaidi ya mitano *consecutively* Mkoa wa Kagera umekuwa kati ya mikoa mitano ya mwisho kichumi. Kwa hiyo, Mkoa wa Kagera ni mkoa maskini. Kwa kutumia kipimo cha umaskini wa mahitaji ya msingi *(basic needs poverty),* Mkoa wa Kagera una wastani wa asilimia 31.9 wakati wastani wa kitaifa ni asilimia 26.4 kwa maana hiyo Mkoa wa Kagera bado una hali mbaya kimaskini. Kwa kutumia kipimo cha umaskini wa chakula ambayo ni *food poverty* Mkoa wa Kagera una asilimia 12 wakati wastani wa Taifa ni asilimia nane. Kwa hiyo, inaonesha kwamba mkoa bado ni maskini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera kama nilivyotangulia kusema kwa zaidi ya miaka mitano sasa unaendelea kuwa kati ya mikoa ya mwisho mitano kwa umaskini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri Mkuu *statistics* au takwimu huwa hazidanganyi, hivyo Mkoa wa Kagera tukubali, Mkoa wa Kagera una hali mbaya, umaskini umekithiri, lakini Wabunge tumeongea sana humu, kila Mbunge wa Kagera alipoinuka alizungumza juu ya umaskini wa Mkoa wa Kagera, mimi mwenyewe nafikiri ni mara ya tatu. Ukisoma kwenye mitandao ambayo imeundwa kwa watu wa Kagera wanaokaa Tanzania na wanaokaa nje kila mtu anaguswa na kila mtu anazungumzia juu ya umaskini wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hata Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alipokuja mkoani Kagera kitu cha kwanza ambacho wazee wa Mkoa wa Kagera walimkabdidhi ni kwamba tunafanyaje, tunatokaje kwenye huu mkwamo ambapo kwa sasa hivi inaonekana kwamba mkoa wetu ni wa mwisho, ni mkoa maskini kuliko mikoa yote Tanzania Bara na yeye akatoa maagizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda Serikali mtueleze baada ya kuona mkoa ambao ulikua upo kati ya *the best three,* kati ya mikoa mitatu iliyokuwa inafanya vizuri kielimu, kati ya mikoa miatatu iliyokuwa inafanya vizuri kimaendeleo, sasa hivi umekuwa mkoa mwisho. Nina uhakika Mheshimiwa Mwigulu na wewe hili linakugusa, nina uhakikia Mheshimiwa Chande na wewe linakugusa na Waziri Mkuu na wewe na wote. Tunafanyaje? Mmeshafanya utafiti mkaleta *REPOA,* mkaleta kamati zenu hizo zinazoshauri kiuchumi katika Wizara wakaangalia tatizo ni nini ndani ya Mkoa wa Kagera? Kwa nini tunakuwa wa mwisho? Mnapopeleka hizi pesa mafungu yote miradi mnaleta, *it doesn't work* bado tunaendelea kuwa wa mwisho. Kwa hiyo ina maana kwamba tunahitaji mkakati zaidi ya hizi hela za kawaida zinazopelekwa katika Mkoa wa Kagera na kwa sababu sasa sina muda nitaongelea mambo machache tu ambayo mimi nafikiri yakifanyika yanaweza kusaidia kufungua Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza biashara ya mpakani; sisi tunapakana na Uganda, tunapakana na Kenya, tunapakana na

Rwanda, tunapakana na Burundi. Kwa kufanyabiashara tu ya mpakani ambapo ni eneo ninalofikiri Mheshimiwa Waziri wa Fedha naona kama Tanzania hatufanya vizuri kwenye kutafuta biashara ya kuendeleza biashara mipakani, lakini sisi kama Mkoa wa Kagera tunaona kwamba biashara ya mpakani ikiweza kuboreshwa inaweza ikatusaidia na kututoa katika mkwamo tuliopo.

Kwanza kabisa tunaomba tujengewe masoko, tujengewe soko pale Mtukula ambapo ni Misenyi kwenye mpaka wa Mrongo ambapo ni Kyerwa, kwenye mpaka wa Rusumo na Kabanga ambapo ni Ngara. Kwa kufanya hivyo tutafanya biashara na nchi jirani, na hii itafungua mkoa na kutakuwa na mzunguko wa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika sasa unaona kwamba hata wafanyabiashara wa Tanzania wanahama wanaenda kufanyiabiashara zao upande wa pili kwenye nchi jirani badala ya kufanyia Tanzania. Ni kwa sababu sera za kule, uharaka wa kuanzisha biashara kule, sera zao za kodi zinawavutia kuliko za hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali tujiangalie upya, tuangalie sera zetu mipakani zinasemaje kusudi tuweze kuwavutia sasa wasiende upande wa pili. Serikali ya Tanzania, *National Housing* imejenga *mall* pale Mtukula, lakini ni kwa muda mrefu imeshindwa kujaa, wafanyabiashara wana-*prefer* kwenda upande wa Uganda kuliko kufanyia Tanzania. Mlituahidi kutujengea pale soko, lakini ukienda ni vumbi tupu, wakati wa mvua ni matope matupu. Nani atakuja kuwekeza? Hakuna hata *storage facilities*. Tunaomba tujengewe masoko ya uhakikia kuweza kuufungua Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, lakini Mkoa wa Kagera mnajuwa tupo pembezoni ni mbali sana na Dar es Salaam ambapo ndio malighafi nyingi zinapatikana kilometa zaidi ya 1,500. Kwa hiyo, huyu mwekezaji ambaye anaamua kuwekeza ndani ya Kagera, *cement* wakati Dar es Salaam inanunuliwa shilingi 13,000; shilingi

15000 ikija kufika Kagera imekuwa ya shilingi 23,000 na shilingi 25,000. Gharama za uzalishaji zinakuwa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali mmeshajiuliza wakati mnahamasisha viwanda vingi vianzishwe watu wawekeze kwenye viwanda, kwa nini Mkoa wa Kagera tulipata wawekezaji wachache sana? Ni kwa sababu ya gharama za uzalishaji tuko nazo mbali sana, ndio maana mwaka 2015 Mkoa wa Kagera ulikuwa na kongomano la uwekezaji, waliomba na wameleta Serikalini na hamjatujibu, tunaomba tupate upendeleo maalamu *(preferential treatment)* ya kikodi, ya kisera, ya kisheria ili kusudi tuweze ku- *compete*, tuweze kuwa na ushindani kuwa na ushindani ulio sawa na nchi zilizo jirani ambapo inaonekana sera zao zinavutia zaidi, lakini mpaka leo hamjatujibu na sisi tunaendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali mtusaidie kwa kuboresha biashara za mipakani, lakini vilevile tupate hiyo *preferential treatment* ili tuweze kushindana na kuboresha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera ni *predominantly rural* yaani maeneo mengi yamekaa kama vijiji. Kwa hiyo, kitu cha kututoa sasa ni kilimo, Mheshimiwa Bashe kitu cha kututoa kwenye umaskini Mkoa wa Kagera ni kilimo. Tunalima kilimo ambacho hakina tija, matumizi ya mbolea yako chini sana, mazao/mimea tuliyokuwa nayo ni imezeeka, kwa hiyo tunaomba Serikali waje watusaidie watupe pesa kusudi tulime kilimo ambacho kina tija, wang'oe ile mibuni na migomba ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza mwaka jana Serikali ndio imetuletea mbolea tani 2,600 yenye thamani ya shilingi bilioni 7.5 na kati ya hizo shilingi bilioni nne zote zilikuwa ni ruzuku iliyotolewa na Serikali, tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri awahamasishe Wanakagera walime kwa kutumia mbolea ili tuweze kupata kilimo chenye tija, lakini vilevile tunapopata ushuru haya mazao yote yakiuzwa kahawa ikiuzwa, kwa mfano kama

mwaka jana ushuru kutoka kwenye kahawa ilikuwa shilingi bilioni 4.5, ni kiasi gani kilirudishwa katika kuendeleza zao la kahawa? Unakuta kwa sababu Halmashauri zina mambo mengi yanayofanywa haziwezi kuendelea kurudisha hela kwenye kilimo zinaenda kwenye huduma kama afya, kama maji ni vizuri, lakini ni kiasi gani kinachorudi kuendeleza kilimo? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Wizara ya Kilimo…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yako mengi ya kuongea Waziri wa Fedha anapokuja kuhitimisha tunaomba atueleze kuna mpango gani makusudi wa kuweza kwenda kusaidia Mkoa wa Kagera, kuutoa kwenye mkwamo, waondoke kuwa mkoa wa mwisho wa umaskini ndani ya Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu. Nilimwita Mheshimiwa Salame Makamba, wakati huo Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara pamoja na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii muhimu na nitaanza hotuba yangu kwa kumnukuu Waziri wa Fedha kwenye hotuba yake ukurasa wa 72 kwa maandisha makubwa kabisa alisema; "kodi ni jambo la nchi, kodi ndio maendeleo ya nchi yetu" na mimi namuongeze kwa mwanasiasa nguli duniani alisema; "*what's the government gives it must first take away.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomaanisha ni kwamba ili Serikali iweze kukusanya kodi ni lazima itengeneze walipa kodi

wapya na sio kuongeza vyanzo vya kodi kwa walipa kodi wa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasisitiza maneno yangu hayo kwa kumpongeza Waziri wa Fedha kwenye baadhi ya maeneo ametusaidia kuchechemua na kutengeneza walipa kodi wapya hasa katika eneo la kuweka mikopo na ada bure kwa wanafunzi wa vyuo vya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli hilo ninampongeza sana kwa sababu moja kati ya changamoto kubwa katika Bunge hili tumeingia tuliokuwa tunapigania sisi tuliokuwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilikuwa ni kuwapatia mikopo hawa mafundi au *technicians* au watu wenye ujuzi wa kati kwa sababu kimsingi watu hawa ndiyo wanaajirika kwa haraka, kimsingi watu hawa ndiyo ambao fani zao zinauhitaji mkubwa kwenye dunia ya sasa hasa Tanzania hii ambayo tunaenda kwenye viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme ninaipongeza Serikali kwa upande huo lakini ninao ushauri mdogo. Kwanza wameondoa ada kwenye baadhi ya vyuo kwamba kwa wale wanafunzi ambao watachaguliwa na Serikali kwenda kwenye vyuo vya kati lakini pili wameweka *course* za vipaumbele kwa watu ambao watapewa mikopo hii na tatu wanasema kwamba wataanza kuwapa mikopo wanafunzi watakaoingia Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wanasema maendeleo yanapaswa kuwafuata watu na siyo watu kufuata maendeleo. Imekuwa ni utaratibu au desturi Watanzania tunaenda tunavamia mahali, tunajenga nyumba ndiyo Serikali inakuja tunataka tufanye upimaji, urasimishaji na nini. Hao wanafunzi walioanza vyuo vya kati kipindi cha nyuma siyo kosa lao. Serikali haikuwa na mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba watu hawa wanapata mikopo na wanapata elimu katika mazingira sawa na wale walio katika vyuo vya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme viwekwe vigezo ambavyo vitaweza kuwafaa wale wanafunzi ambao tayari wapo kwenye masomo na hawapati mikopo na viwekwe vigezo kwa wale ambao wataanza ili wote kama Watanzania waweze kunufaika na rasilimali hii ndogo ya Taifa letu ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kwa kusema kwamba Serikali lazima itoe ili iweze kuvuna. Huwezi kumkamua ng'ombe ambaye hujamlisha. Serikali imeweka nyenzo kwenye Sheria ya Manunuzi mwaka 2016 kwamba kwenye manunuzi yote yanayofanywa na Serikali itahakikisha 30% ya manunuzi hayo wanapewa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu lakini fursa hiyo imepokwa tena na Serikali kwa upande mwingine unasema hayo makampuni ambayo yatamilikiwa na wanawake au vijana au watu wenye ulemavu ili wapate kuzipata fedha hizo ni lazima waungane kwenye vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kampuni *is a legal person* yaani anatambulika yeye mwenyewe kama kampuni na ana *address* yake, ana uwezo wa kushtaki na kushtakiwa, kwa nini unamlazimisha akae kwenye vikundi? Fedha za vikundi zipo kule halmashauri na Serikali inatengenezea mpango. Huu ulikuwa ni mkakati mwingine wa Serikali kuwainua wanawake wenye mitaji midogo na ya kati na ya juu waweze kufikia kufanya biashara na Serikali na Serikali ndiyo mfanyabiashara mkubwa duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niengomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha busara itumike, marekebisho yafanyike. Kampuni lolote ambalo linamilikiwa na mwanamke kwa 51% au inamilikiwa na kijana kwa 51% au mtu mwenye ulemavu iweze kuwa na sifa kamili bila kulazimika kuungana na makundi mengine kuweza kupata hii mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye jambo lingine la muhimu sana la upandaji wa vifaa vya ujenzi. Hii imekuwa dhana na nimesema hatuwezi kuendelea kama Taifa kama tunaongeza kodi katika maeneo mbalimbali badala ya kuongeza walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna tatizo la msingi hapa. Serikali mwaka jana iliongeza kodi kwenye nondo, ikaongeza kodi kwenye mabati,Mwaka huu imeongeza kodi kwenye *cement*. Hivi mnataka tukakae kwenye nyumba za udongo? Mimi nataka kujua. Nalielewa lengo la Serikali, sekta ya *cement,* sekta ya nondo kwa maana ya chuma, ya mabati ni sehemu ambayo inabiashara kubwa sana lakini tusiwasahau Watanzania wa kawaida ambaye anatumia rasilimali hizi kujiboreshea mazingira yao ya kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mifumo yake ambayo inaweza kujua manunuzi haya yanafanyika kwa ajili ya viwanda, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na manunuzi haya yanafanyika kwa ajili ya wananchi kuboresha mazingira yao ya kuishi. Serikali imetueleza hapa juzi wanasema wenyewe wanayo *Electronic Tax Stamps* wanatumia mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuweza ku-*track*. Kwa nini Serikali isitumie mfumo huo huo wakamuongezea tu huyu mkandarasi hadidu za rejea kwamba mabati, *cement,* nondo ambazo zinatumika kwa ajili ya ujenzi wa madaraja, barabara sijui viwanda hayo yawe na *tax* yake tofauti na yale *material* yanayotumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi *cement* iuzwe leo shilingi 16,000 Dar es Salaam, Shinyanga inafika kwa shilingi 30,000. Angalia leo bati la *grade* 30 unaenda kuliongezea gharama. Mtu wa kiwanda hatumii bati la *grade* 30 lakini ikipunguziwa kodi wananchi wataacha kuezeka na nyasi kule kwangu Shinyanga. Nondo ambazo zinatumika kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ni *millimeter* 10, *millimeter* 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaweza tu kusema wale watu wanaohusika na *electronic taxation* waweke hizo *stamp.* Zile zinazotumika kwa ajili ya *domestic* ziwe na gharama zake na zinazotumika kwa ajili ya *industrial* ziwe na gharama zake waongeze kodi huko lakini huku kwa wananchi kwa ajili ya kuboresha mazingira ya wananchi, kwa ajili ya kuboresha makazi na tulishasema tangu Azimio la Arusha. Mwalimu Nyerere alisema tuna ujinga, umasikini mpaka leo

tunahangaikia kweli makazi wananchi sehemu nzuri ya kukaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuhangaika na hilo, niseme niiombe Serikali kwenye eneo la kuongeza kodi kwenye vifaa vya ujenzi tunawaumiza Watanzania wa kawaida. Tunawaumiza Watanzania wa kawaida kwa hiyo tutofautishe tuweke madaraja na vifaa vya ujenzi ikibidi vitolewe bure. Wakati tunazungumzia hapa biashara ya *cement* na bei ya *cement,* tafiti zilizofanyika za haraka haraka *cement* Tanzania inaweza kuuzwa kwa shilingi 10,000 kwa mfuko lakini sasa hivi ukienda Mwanza *cement* ni shilingi 28,000. Leo tumeongeza kodi haya umetoa kwenye kodi ya *cement* umeongeza bado unaongeza kwenye kodi ya mafuta umeongeza shilingi 100, maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *cement* kule imeshaongezewa gharama kuisafirisha mwisho wa siku anayeathirika ni mlaji. Umeshaiongezea gharama kuisafirisha kutoka Dar es Salaam ikifika Shinyanga imepanda bei zaidi msafirishaji anakwambia gharama ya mafuta imeongezeka wala haibebi gharama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana sana Serikali inayo mifumo tena mizuri ya kielektroniki ambayo inaweza ku-*trace* matumizi ya vifaa hasa vifaa vya ujenzi hivi ni kwa ajili ya *domestic* na kuboresha maisha ya Mtanzania, hivi ni kwa ajili ya maendeleo na ujenzi wa miundombinu watofautishe matumizi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niongelee kuhusu bakaa. Mheshimiwa Rais anajitahidi sana kutafuta fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Kwa sasa nahudumu kwenye Kamati ya TAMISEMI. Bakaa fedha ambazo zinabaki yaani halmashauri zipo zinazoomba fedha hazipelekewi, zipo ambazo zinaomba fedha kidogo wanapelekewa fedha zaidi, zipo ambazo zinapelekewa fedha ya kutosha haitumii mpaka mwaka wa fedha unaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, ningeiomba Serikali kwa kweli na hili liko kwenye dhana ya utawala bora na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeliona. Ningeomba Serikali kwa nia ya dhati kabisa kila mtendaji apimwe kwa kazi anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukubali tunakwenda kwenye halmashauri kukagua unakuta Mkurugenzi ana fedha kwenye *account,* miradi haitekelezwi ukimuuliza anasema eti kamati haijakaa hatujakaa kujadili na kufanya nini, mara sijui mifumo haifanyi kazi. Kila mtu apimwe kwa utekelezaji wa kazi zake na sasa hivi tunavyoelekea mwishoni mwa mwaka, tathmini ifanyike ni Mkurugenzi yupi ambaye ameshindwa kutumia fedha kwa makusudi, ni yupi anafanya kwa uzembe, wengine hawawalipi wakandarasi kwa sababu wanajua itatengeneza riba ambayo na yeye atakuwa ni mnufaika kwneye riba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali kwenye eneo hili la bakaa ni eneo ambalo limekuwa ni sumbufu sana kwenye maeneo ya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hazijengwi, mabweni hayajengwi, miradi haitekelezwi ukiuliza anakwambia mara mifumo, kamati haikukaa, sijui *force account* haifunguki. Sisi hatutaki maelezo, *it is either* ufanye kazi kwa ajili ya Watanzania au useme umeshindwa aje mwingine atusaidie kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara wakati huo Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Leah Komanya wanajiandaa.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Leo nitaanza kwa maeneo machache sana kwenye elimu kwa sababu mengi

wameyafanya. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. Mambo mengi sana yanayohusu elimu hasa ya vyuo vikuu yametekelezwa lakini niseme tu machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaja kwako katika kuchangia, Mheshimiwa Waziri wa Elimu kuna mambo fulani inabidi umuone huyu Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza niseme ukweli Waziri wa Fedha pamoja na msaidizi wake mmekuwa ni watu mnaoweza kufikika, hakuna ubaguzi ninyi ni kati ya wale Mawaziri ambao ni rahisi sana kufikika, nyie wenyewe mnajua jamani Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Fedha tumekuwa na Mawaziri ambao unaogopa hata kumkaribia lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nikupongeze kwa hilo na hasa kwa kujali makundi yote ya Wabunge wanafika kwako unawasikiliza. Wakati mwingine ndiyo hapa ndani lazima utibuliwe wewe ni Waziri wa Fedha lakini huna hasira, huna chuki wala huweki kinyongo. Endelea na hivyo *and that is leadership. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme suala la mikopo nikuombe sana sana Waziri hivi vyuo vya kati vipewe mikopo ikiwemo vyuo vya maendeleo ya jamii. Nimeona wakati Waziri wa Elimu anajibu anasema ooh, vyuo vya kati sijui *VETA* na nini tunaangalia. Tukiaza hivyo lazima kutakuwa na malalamiko. Kama tumesema vyuo vya kati vipewe mikopo ni vyuo vyote vya kati ili isilete shida. Hawa watu wataleta shida tu, tutapata tena *message* mimi nimechaguliwa chuo cha kati sijapata mkopo. Kwa hiyo, hakikisha wewe ni mjanja tafuta fedha ili kama kuongeza muweze kuongeza ili fedha hizo hata hivi vyuo vya kati vyote vipate mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije jingine naomba tu kukumbusha kwamba kwenye ile fedha ya *HEET* nimepata tetesi mnafanya *allocation.* Fedha za *HEET* ni kwa ajili ya *universities.* Mnafanya *allocation* sasa kama mnafanya hakikisheni kwamba hata Chuo cha Mwalimu Nyerere wanapata kwa sababu wana miundombinu ambayo inabidi waitengeneze lakini pia kuna *branch* yao kule Pemba. Kwa hiyo, kama mtafanya *allocation*

kwenye *HEET* fanyeni *allocation* hiyo muhakikishe hiki chuo kinapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye elimu, Waziri wa Elimu aliahidi kwamba mishahara ya Wakuu wa Vyuo itafanyiwa kazi, mpaka leo kimya. Nimuombe Mheshimiwa Mkenda aje aonane na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aonane na Mheshimiwa Simbachawene wa Utumishi mlimalize hili limechukua muda mrefu. Mkuu wa Chuo anapata mshahara sawa na *lecturer* wa kawaida, jamani inatoka wapi hiyo? Hebu tulimalize hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza huko. Nakuja kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Nashukuru kwamba walitengewa shilingi bilioni 40 Bajeti iliyopita, sasa hivi wana shilingi bilioni 71 ni vizuri ongezeko ni zuri lakini niseme bado ni kidogo mno. Hii Wizara ina madudu mengi mengi, maadili, ukatili wa kijinsia, ubakaji, ulawiti, vipigo, ukeketaji ambao unaendelea ingawa Waziri alisema eti amemfunga ngariba mmoja. Ngariba mmoja unamfunga halafu unakuja kutuambia hapa kwenye Bunge kweli? Wakati mangariba wako kibao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ulawiti unaendelea, ndoa za utototni. Kwa hiyo hii Wizara ina mambo mengi mengi. Nimuombe Waziri wa Fedha sasa nikuombe. Hizo fedha za kodi unazokusanya hizo naomba uzitenge nyingine kwa ajili ya ulinzi wa watoto. Hapa kuna fedha zinatengwa kwa ajili ya ulinzi hata sisi hapa tunalindwa, hakuna mtu anayeweza kuingia humu akatufanyia mambo yale mabaya lakini ulinzi wa watoto bado. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nakuomba halafu wewe unapenda sana watoto. Sijawahi kuona Mbunge yeyote au mwanaume yeyote wa Kitanzania anabeba mtoto mgongoni. Wewe unapenda watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ulifanyie kazi. Kwenye hizo fedha unazokusanya za kodi hakikisha tunapata ulinzi wa watoto. Mpe fedha Mheshimiwa Masauni, mpe fedha Mheshimiwa Gwajima, mpe fedha Mheshimiwa Simbachawene, fanyeni kazi kwenye ulinzi wa watoto nimesema tafuteni dawa. Tafuteni dawa kwa wanaume wabakaji wote na walawiti na fedha hizo

unaweza ukazipata. Tukifanya hivyo nakwambia mambo haya yatapungua tu. Nimeshasema mara nyingi hapa hivi mnaona tabu gani kuwa hasi hao? Na wao hawawezi kuwa hasi mpaka wewe utoe fedha ili hao Mawaziri wengine wenye hizi sekta waweze kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema jambo la ndoa za utotoni. Yaani mpaka wakati mwingine nashindwa kuelewa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Katiba alimhakikishia Mheshimiwa Spika ndani ya Bunge hili kwamba ataleta muswada hapa tukapitisha sheria. Sasa nasikia pembeni pembeni vinakuja vikundi mbalimbali eti ndoa za utotoni ziendelee. Nimesema mara nyingi jamani mtoto wa miaka 12 anaolewa anakwenda kufanya nini huko? Mbona hatuna uchungu na mabinti na haya mambo yote yanayohusu watoto wa kike, yanayohusu wanawake hayafanyiwi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wangekuwa wanakeketwa wanaume ukeketaji ungeisha, wangekuwa wanaolewa wanaume wadogo, ndoa za utotoni zingeisha lakini mambo yanayohusu wanawake kwa nini Serikali hamtaki kuifanyia kazi? Watoto wana keketwa kila siku, Serikali mpo, vyombo vya dola vipo eti mnasema hamuwezi kujua wanafanya kwa siri, nchi hii tunashindwa kulikomesha hilo? Mbona la ualbino tulilikomesha kwa sababu gani la ualibino lilikwisha? Kwa sababu waliokuwa wanaathirika ni watu wenye ualbino wanaume na watu wenye ualbino wanawake na ndiyo maana lilipungua na likaisha. Leo hii kwa sababu wanaokeketwa ni wanawake Serikali mko wapi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha toa fedha zikafanye kazi kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki hiyo ya ukeketaji wala hatutaki hiyo ya ndoa za utotoni. Mnatuletea hapa taratibu za ajabu eti watu wanasema sheria, sijui utamaduni. Mbunge gani hapa atatoa mtoto wake wa miaka 12 akaolewe? Nani atatoa mtoto wake wa miaka 10 akaolewe? Wanasema tu pembeni huko, wawalete watoto wao hapa ili wakaolewe kwa miaka hiyo 12. *That is uncouth,* inasikitisha. Wanawake tusimame ndani ya Bunge hili tukatae. Leta Muswada hapa tujadili msiufiche fiche

huko kwa kusikiliza vikundi vya watu wachache. Tamaduni zilizopitwa na wakati ziondoke ili mwanamke huyu akombolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimekupa kazi na sisi tunasimamia Serikali kwa hiyo mimi nakusimamia leo Mheshimiwa Mwigulu toa fedha, utoe fedha za kuwatunza watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga wakati huo wafuatao wanajiandaa; wa kwanza ni Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Tabasam Mwagao na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nipate kuchangia kwenye hoja hii muhimu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. Sina mashaka na nia ya Serikali ya kuweza kuboresha hali yetu ya uchumi hasa ukizingatia bajeti imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka sasa tuna shilingi bilioni 44.4 nyongeza ya 7% kutoka bajeti ya mwaka jana lakini ninashukuru kwamba kiasi kikubwa cha Bajeti hii karibu 71% inatoka kwenye mapato yetu ya ndani lakini kabla sijaendelea nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu mpendwa kabia anayefanya kazi ya kutukuka katika nchi hii kwa kutoa fedha nyingi katika miradi mbalimbali inayoendelea hata hivi juzi katika Jimbo langu la Kalenga tuliweza kusaini mkataba wa kujenga barabara mpya inayokwenda vijijini kutoka Wenda kwenda Mgama kwa shilingi bilioni 29.8 ni fedha nyingi kujengwa barabara kwenda vijijini lakini nashukuru zaidi alituongezea fedha kwa ajili ya kujenga kipande cha lami kinachokwenda kwenye Makumbusho ya Mkwawa. Kwetu sisi jambo hili ni la heshima

kubwa kwa hiyo, nipende kumshukuru kwa niaba ya Wananchi wa Kalenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pole kwa Wananchi wa Jimbo la Kalenga hasa Kata ya Maboga na Kata ya Mseke ambako wamevamiwa na simba na mpaka sasa simba zimeshakula ng'ombe zaidi ya 10. Niwape pole wote waliovamiwa lakini Serikali inafanya kazi. Tumesha shauriana na vyombo vinavyohusika na wako *site* wanajaribu kulikomesha kabisa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia hasa kwenye eneo la utalii. Eneo la utalii ni eneo muhimu sana kwenye uchumi wetu wa Taifa linachangia 25% ya pato la kigeni (fedha za nje) lakini 17.5% kwenye Pato la Taifa na Nyanda za Juu Kusini kama tunavyojua, Nyanda za Juu Kusini bado ni kama bikra katika eneo hili la utalii kwa sababu maeneo mengi hayajapata kufunguliwa na tunaamini Mpango wa Serikali wa kuanzisha ile miradi ya *regrow* Nyanda za Juu Kusini itakwenda kusaidia utalii kuweza kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, rai yangu ni kwamba niiombe Serikali sasa iweze kuharakisha mipango yake ya kujenga hii miradi ya *regrow* pale Iringa kile kituo cha utalii kiweze kujengwa kama Serikali ilivyoahidi pia na maeneo mengine ambayo yatakwenda kurahisisha watalii kuweza kwenda Nyanda za Juu Kusini ikiwa ni pamoja na kumalizika kwa ule uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapokwenda kumalizia Uwanja wa Ndege wa pale Iringa ambao unaitwa Nduli ambao hauna sifa sana kwenye Taifa hili la Tanzania; maana Nduli Iddi Amini kwetu huku tukimzungumza kwa kweli ni kichefuchefu. Ningependa, kwa ushauri wa wananchi wa Mkoa wa Iringa kwamba ule Uwanja wa Ndege wa Iringa unaoitwa Nduli sasa uitwe Mkwawa, kwa sababu Mkwawa ni jina la kitaifa katika nchi hii kwa mambo mengi ambayo yalifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumzie pia kwenye utalii. Nilikuwa nashauri kwa sababu Mbuga ya Ruaha imekuwa ikikauka mara nyingi kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu zinazoendelea katika maeneo mbalimbali, kwa hiyo ile mbuga imekuwa ikikosa maji. Sasa kuna mpango wa kujenga lile Bwawa la Lyandembela au Lugodaluchali, ambalo bwawa lile ni kubwa kama likijengwa inaonekana litakuwa na kina kirefu sana hata kuliko haya mabwawa mengine tunayojenga, kama Bwawa la Kidunda, ambalo ujazo wake unakisiwa kuwa utakuwa na mita za ujazo milioni 350. Kwa hiyo hili bwawa tukilijenga litaweza kutiririsha maji angalau mita sita kwa mwaka ambayo yataweza kutiririka kwenda katika maeneo ya Madibila kwenye yale mashamba ya mpunga. Maji mengine pia yatakwenda Mtera, Bwawa la Kihanzi na hatimaye Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali itaamua kujenga bwawa hili itakuwa ni rahisi kwanza kudhibiti ule mtiririko wa maji. Kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa Wizara ya Maji imefikiria kulijenga bwawa hili ningeweza kushauri pia hata wenzetu wa utalii katika hii miradi ya *REGROW* wafikirie namna gani wanaweza kushirikiana kwa sababu bwawa lile ni likubwa na linagharimu fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwa kuwa sasa nchi yetu inakuwa katika eneo la utalii, changamoto tuliyonayo nchi hii ni katika kutoa huduma hasa kwenye maeneo ya hoteli. Huduma zinazotolewa na hasa wafanyakazi wetu hawana ujuzi wa kutosha. Ningeomba Serikali ione namna gani tunaboresha huduma *(hospitality)* ambazo kwenye hoteli si nzuri. Sasa ukuaji wa uchumi katika maeneo haya ya utalii uendane sambamba na zile huduma ambazo tunazitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza kwenye eneo la kilimo. Tunaishukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ruzuku ya mbolea, wananchi wengi wamepata. Lakini ushauri wangu kwenye hilo, ili tuendelee kuongeza uzalishaji ambao utakula fedha nyingi kaka yangu Mwigulu ningeshauri yafuatayo. Kwenye upande wa mbolea

tuhakikishe kwamba vituo vya kusambazia mbolea tunavisogeza viwe karibu na maeneo ya wakulima lakini mbolea pia iweze kupatikana kwa wakati. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuzalisha zaidi na tutaweza kukupa fedha nyingi ili wewe uweze kutekeleza miradi mingi ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeshauri, ukiangalia kwenye Kata ya Nzihi katika Jimbo la Kalenga ndiyo kata kame kwenye Jimbo langu la Kalenga. kwa hiyo kulikuwa kuna mpango wa kujenga bwawa miaka mingi iliyopita. Tangu mwaka 2008 utafiti ulishafanyika, walishafanya angalau upembuzi kwa kiasi fulani. Kwa hiyo ningeiomba Serikali iendelee sasa na mpango wake wa kulijenga lile bwawa na kukarabati skimu mbalimbali zilizoko kwenye Jimbo la Kalenga. Tuna skimu takriban 19 ambapo tutakuhakikishia kwamba tutaongeza kilimo lakini utaweza kupata pesa nyingi kutokana na hili eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye wakulima; mwaka jana tunashukuru tulifanya usajili wa wakulima wengi, lakini wapo wakulima ambao kwa bahati mbaya hawakuweza kusajiliwa. Ningeomba Serikali iweze kuchukua hatua sasa waanze kusajili wakulima sasa ili wakulima wengi waingie katika hii fursa ya kupata mbolea za ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulishauri ni kwa upande wa ulipaji kodi. Wapo Watanzania wenzetu wengi ambao wamekuwa wakikwepa sana kodi na wakati mwingine kuisingizia *TRA*, kwamba *TRA* wamekuwa *brutal*, lakini wao wengi wanaongoza katika kukwepa kulipa kodi. Sasa kama ukikwepa kulipa kodi tutatekelezaje miradi hii mikubwa namna hiyo? Kwa hiyo mimi ningeomba Watanzania wenzangu wafanyabiashara, suala la kulipa kodi ni suala la lazima na suala la kutoa risiti za eletroniki ni suala la lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione namna gani inaweza kufanya mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa fedha iweze kusomana ili kuziba mianya ambayo inapelekea *leakages,* fedha kuvuja katika maeneo mbalimbali. Hili nalo liweze kuangaliwa, Serikali iharakishe sana mifumo yake ya ukusanyaji wa mapato ya

Serikali isomane na iwe rahisi. Hili ni jambo ambalo ni muhimu sana tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri, kwa kuwa umefanya marekebisho ya kupunguza na kuongeza kodi katika maeneo mbalimbali, ningeshauri katika eneo la majengo na eneo la ardhi hasa eneo la viwanja; huku kuna fedha nyingi sana ambayo imelala. Watu wengi hawalipi kwa sababu kama mnavyojua hali ya uchumi imeathirika sana duniani hata mfukoni namo mmepata changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kushauri kwamba, zile faini ambazo zinatolewa kwenye kodi za majengo na kwenye kodi za viwanja ziondolewe angalau kwa kipindi cha miaka miwili, na tuendelee kuhamasisha watu waweze kulipa hizi kodi. Hata kwenye majengo ya Serikali hata taasisi nyingine zinadaiwa fedha nyingi sana na hizi faini zimelimbikizwa, zipo nyingi. Tafuteni namna ya kulifanya hili. Mkifanya hivyo ninaamini mtakwenda kupokea makusanyo mengi sana na yataweza kusaidia kuingia kwenye mfumo na hizi fedha tuweze kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kama Mwenyekiti wa Mazingira ningependa kushauri, hakuna uchumi bila kutunza mazingira. Suala la mazingira katika nchi hii ni baya zaidi. Tafiti zanasema kwamba ifikapo mwaka 2030 asilimia 66 ya ardhi inayolimika, itakuwa hailimiki kwa sababu ya uharibifu wa mazingira. Ukiangalia kile kilichotokea Malawi, mmomonyoko wa ardhi na mafuriko ambao umeleta hasara ya karibu trilioni moja na milioni mia mbili, watu takriban elfu moja wamekufa ni kwa sababu mazingira yameharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nitoe rai katika eneo hili kama tunataka kuendelea kuwa na uchumi suala la uharibifu wa mazingira lichukuliwe kipaumbele na Serikali itumie nguvu zake za kisheria kuzuia ukataji wa miti na kuhimiza upandaji wa miti. Ukipita kwenye ndege hapa utakuta kwenye vilima vingi ni mawe tu ndiyo yanayoonekana. Hii inaonesha ni kiasi gani mazingira yameharibiwa. Kwa hiyo kwa hili niwaombe sana hatuna uchumi bila mazingira kwa hiyo Serikali iweke sheria kali.

Hakuna kukata mti katika mlima wowote katika nchi hii. Kama kuna watu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** …itapaswa ijengwe kwa mikataba maalum, nakushukuru sana napenda kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiswaga kwa mchango wako. tunaendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba mnaweza kuendelea kuchangia kwa njia ya maandishi na ni rahisi tu. Unakwenda kwenye dirisha la shughuli za Bunge, ukimaliza unachagua maneno mchango wa mandishi, ukimaliza unatoa mchango wako, kisha baada ya hapo unawasilisha, hapo mchango wako utakuwa umeshafika Serikalini. Tunaendelea nilimwita Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, wakati huo Mheshimiwa Tabasam anajiandaa.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kutoa maoni katika hoja iliyopo mbele yetu. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya za kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi mikubwa ya kimikakati. Naomba nimtie Mheshimiwa Rais moyo, tuko pamoja naye kazi anayoifanya inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mwigulu pamoja na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na jukumu kubwa la kutafuta fedha lilipo katika majukumu ya Wizara ya Fedha. Kazi ya kutafuta fedha ni ngumu, kazi ya kuchangisha kodi ni ngumu. Naomba niwatie moyo, tuko pamoja na ninyi, na naomba Watanzania hususan wananchi wa Jimbo la Meatu

tuielewe hii Wizara katika suala zima la ukusanyaji wa kodi, kwani fedha nyingi sana zinazoletwa katika Jimbo la Meatu zinatokana na kodi hizi tunazochangia wananchi. Zinatokana na fedha zinazotafutwa za mikopo ya masharti nafuu nje. Naomba tuiunge mkono Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Niishukuru Serikali hivi karibuni Jimbo la Meatu tumeletewa milioni 857.7 kwa ajili ya upanuzi wa shule ya wasichana Nyalanja Sekondari ambapo yatajengwa mabweni manne, matundu 18 ya vyoo pamoja na madarasa 12. Shule hii ni *high school,* kwa hiyo kuwepo kwa *high school* pia kutachangiza watoto wale wa *form one* hadi *form four* kupenda kujifunza kwa sababu kutakuwa na wasichana wengi wanaotoka sehemu tofauti za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishukuru Serikali wiki iliyopita imesaini mikataba saba ya ujenzi wa barabara za kimkakati ikiwemo barabara yetu ya Sibiti, Mwanuzi, Lalago Maswa kwa kiwango cha lami. Niombe Serikali yetu kusaini mikataba si maana yake fedha ziko mezani, maana yake Serikali iendelee kutafuta fedha. Fedha nyingi zinatakiwa kwa ajili ya hii miradi saba takribani trilioni tatu. Fedha hizi zinatokana na kodi zetu, fedha hizi zinatokana na tozo zetu tunazotozwa pamoja na mikopo ya masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru Serikali, mwishoni mwa mwezi Mei, Wizara ya Maji ilienda kusaini mradi wa kimkakati wa maji wa kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake aliahidi, kwamba angeenda kusaini mkataba, ni kweli amesaini mkataba wa bilioni 440 kwa ajili ya kutoa maji Ziwa Victoria na kuyaleta katika Wilaya za Mkoa wa Simiyu. Naamini sasa maji haya yatafika katika Wilaya ya Meatu ambayo imeathiriwa kabisa na mabadliko ya tabianchi. Nimshukuru Mheshimiwa Aweso wakati, huo alitupatia milioni 500 kama nilivyoomba wakati nachangia Wizara ya Maji kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la kati ya Mwambajimu pamoja na Lukale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe wananchi wa Jimbo la Meatu, bwawa hili litajengwa kati ya Kijiji cha Lukale na Mwambajimu ambako watu wetu hawapati maji kutokana na chumvi. Kuna ziwa Eyasi pale ambalo lina chumvi kabisa; wananchi wanasafiri mpaka siku nne kuyapata maji kwa ajili ya kunywesha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sasa kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Nishukuru Serikali kwa *program* ya mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa na Serikali kusoma kwenye vyuo vinavyotoa elimu katika fani za kipaumbele. Jambo hili ni zuri kwa watoto wanaotoka kwenye familia duni. Hii ni kwa sababu wengi walichaguliwa kwenda kwenye vyuo vya kati walishindwa kuhimili ada kwa ajili ya kulipa masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kuna fani ambazo zimeachwa. Kwa mfano katika Jimbo la Meatu wanafunzi wametoka Sekondari ya Kimali na Mwamalole, wengine wameenda chuo cha *IFM* kilichopo Bariadi, wengine wameenda vyuo vya maji. Lakini, wanafunzi hawa wamepata *division* nzuri, wamepata *division two* wamepelekwa katika hivi vyuo vya kati lakini havipo kwenye vyuo vya kipaumbele. Wanafunzi hawa wanatoka kwenye familia zenye maisha duni kwa hiyo ndoto yao inaweza ikakatishwa pale katikati kwa kukosa ile ada. Kwa macho tunaweza tukaiona ile ada ni ndogo lakini ipo jamii ambayo haiwezi kuilipa hiyo ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanafunzi walitamani waende *A-level* kwa sababu kule elimu ni bure hakuna ada angalau waliweza kubaingiza kwa kutafuta nauli wengine walikaa miaka miwili shuleni bila kurudi nyumbani ili waweze kuhitimu katika ile miaka miwili na hatimaye waende chuo kikuu ambako kuna mikopo. Kwa hiyo kwa kuwapeleka kwenye vile vyuo wanaweza kupoteza ndoto zao kwa ajili ya kukwamua zile familia zao. Niiombe Serikali iende zaidi, ipanue wigo, ione vyuo vya kati vingine kwa sababu kuna wengine wamepata *division three* wameenda *form five* wakatimiza ndoto zao, waliopata *division two* wanaenda chuo cha kati wanaweza wakapoteza ndoto zao pale katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la upatikanaji wa fedha za kigeni limekuwepo katika kipindi hiki cha hivi karibuni na Serikali imebainisha sababu za kuwepo changamoto hii lakini ninaunga maoni ya Kamati ya Bajeti yote. Imechambua, ikaona sekta kuu tatu ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa katika ongezeko la fedha za kigeni ikiwemo sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mazao ya kimkakati ambayo mojawapo lipo zao la pamba na zao la alizeti ambayo ni mazao ya kimkakati katika Mkoa wetu wa Simiyu katika Wilaya yetu ya Meatu. Mwaka jana wananchi walifurahi baada ya kuona bei ya pamba imefikia hado 2000. Wananchi wengi walijitokeza na kulima pamba hiyo, lakini mwaka huu bei yake ni 1,000, inazidi kuwanyongonyesha na kuwakatisha tamaa wananchi wetu wa Mkoa wa Simiyu hususan katika Wilaya ya Meatu. Kwa hiyo wananchi wamekuwa wakitangatanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana waliona bei ya alizeti ilipanda wengine waliacha pamba wakaenda kwenye alizeti lakini tunaona bei ya alizeti imeshuka zaidi ya asilimia 50 kwa wakulima wetu. Kwa hiyo wananchi hawajui cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto nyingine, katika yale mazao tunayoyalima bado Tembo wanakuja kuyavuruga yale mashamba yao. Tuone namna gani tunaenda kuwasaidia wakulima hawa wa pamba na alizeti. Pamoja na mwaka jana Serikali ilipeleka tani 28 za mbegu katika Wilaya ya Meatu, lakini tani 8 tu ndizo na zilinunuliwa tani 20 zilirudishwa na ASA kwa sababu zilienda kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo pia wananchi walipanda mbegu hazikuwa na tija nak ama mbegu zingekuwa zina tija pamoja na kuporomoka kwa bei zingeweza kuwasaidia zaidi. Huenda wenye viwanda wanashindwa kununua labda mbegu hazina tija, tuliangalie suala la tija katika mbegu za alizeti. Serikali iliagiza mafuta inawezekana zaidi ya upungufu uliokuwepo. Tukiangalia Serikali iliagiza mafuta ghafi ya michikichi kwa ajili ya kuja kuchakata na kwenda kuyauza nchini na

mengine kuyauza nchi ya Malawi, Rwanda, Burundi na *DRC*. Niiombe Serikali ifatilie takwimu na kuangalia, je, yale mafuta yanayochakatwa kwa ajili ya kuuzwa katika nchi nilizozitaja yanauzwa kweli? ama yanazunguka ndani ya nchi na kuleta ongezeko kubwa la mafuta na kukosesha bei ya mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la Tembo. Suala la Tembo linavuruga mashamba yetu, ya wakulima wetu mpaka wanakosa vyakula. Nimshukuru Mheshimiwa Rais mwaka huu alituletea mahindi yenye bei nafuu. Nishukuru wepesi wa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe pamoja na Naibu walitusikiliza Wabunge kwa urahisi na kuyaleta yale mahindi. Lakini bei ile ya mahindi bado ni ndogo ukilinganisha na gharama ya fidia ya ekari ya mahindi ambayo wananchi wanalipwa, na fedha hizi zinaletwa kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema inaweka mbinu ya kukabiliana na tembo, imesema inaleta *radio caller*. *Radio caller* katika hifadhi ya makao ziliwekwa lakini hazikuwa na ufanisi kwa sababu ziliweza ku-*detect* ni wapi Tembo wapo kwa kuangalia kwenye mtandao lakini walikosa vifaa vya risasi, walikosa radio kwa hiyo yaliendelea kuwa kama ni mapambo tu ilhali *radio caller* moja inatumia fedha nyingi sana za kigeni. Serikali imesema wakulima wa kando kando ya hifadhi walime mazao ambayo si rafiki kwa tembo; lakini, hakuna mazao ambayo si rafiki ya tembo. Hata pamba inavurugwa na tembo, alizeti inavurugwa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena niiombe Serikali ile habari ya kusema kwamba wananchi wamejenga katika ushoroba, na mimi niwaulize. Je, Tembo zamani walikuwa wanakula matikiti yalipandwa na nani? wanakula viazi vilipandwa na nani? kwa hiyo Serikali ikubali mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya maisha hata kwa hawa tembo ianze kukabiliana nao badala ya kuanza kusemea ushoroba, ushoroba, ushoroba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** …tumechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya kwa mchango wako. Hapa ninao wageni, naomba niwatambulishe.

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani Mbunge ambao ni familia yake kutoka Singida Kaskazini, haya. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni Wachungaji kutoka Rungwe Mkoani Mbeya, karibuni sana Watumishi wa Mungu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 70 na walimu 11 kutoka Shule ya Msingi ya Amani ya Jijini Dar es Salaam, ahsante sana na walimu wao wanaowalea wako wapi wapunge mikono? Haya ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, wakati huo Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima anajiandaa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchango wangu katika eneo hili la Bajeti Kuu ya nchi na leo kidogo niko kizalendo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ni majemedari wa kupiga kelele na kuzungumza sana maneno makali katika mitandao na kila maeneo mengi sana. Maneno haya yangekuwa yanatoboa mwili wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, leo angekuwa amejaa *bandage* mwili mzima. Kwa hiyo anachotakiwa hapa sasa hivi ni kuwa na ngozi ngumu tu na kujenga imani halafu baadaye anatoboa. Nchi inatukanwa kila kona na sababu ya nchi kutukanwa kila kona ujue watu

wamechoka, hawana pesa mifukoni. Kwa hiyo, mtu akikaa akafikiri hana cha kufikiri anaingia kwenye mtandao anaanza kutukana, sasa hili lazima Waziri alijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa bajeti huu ni kwamba wakati wanaandaa bajeti, hawa watalam wetu wawe wanaita na sisi tuliyochomwa jua sana huku mtaani tuje tuwashauri namna ya kuandaa bajeti. Kuna vitu ambavyo sisi tutawaeleza hiki weka, hiki punguza, hiki toa, lakini wakijifungia ndani wenyewe waliokaa kivulini wanakaa kwenye *AC*, magari yapo yapo kwenye *AC* na kila kitu, wakimpelekea Waziri huku, huku Waziri anaendelea kutukanwa sana. Sasa naye ana wataalam wanaomzunguka hali siyo nzuri, huku chini Mheshimiwa Waziri wa Fedha miradi mingi sana inafanyika, tembea nchi nzima mabarabara yanatengenezwa, majengo yanajengwa na kila kitu kinakwenda katika nchi hii, maendeleo yanazunguka kama tairi la gari. Nchi inakuwa kama imepata uhuru sasa hivi, kila kitu kinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote kuna jambo la kujiuliza, kwa nini kelele zinakuwepo? Huku chini kuna watu wakitoka ndani saa kumi na mbili asubuhi kwenda barabarani kutafuta pesa wanachomwa jua mpaka saa kumi na mbili jioni, anarudi na elfu tatu na elfu mbili, anapitia dagaa anakwenda kula nyumbani kwake, hawa watu wapo wengi kwenye nchi hii. Sasa Waziri alete mipango ya kupata pesa, wananchi huko wapate pesa na zenyewe zizunguke sasa kama tairi la gari, kelele zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipi kifanyike? Lazima waangalie huku chini wananchi wanatakiwa sasa wapate miradi itakayowaendesha, yatengenezwe masoko ya gharama nafuu. Haya masoko yanayokwenda kujengwa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha angekuwa ananisikiliza ananiangalia, unafahamu akianza tena kula *story* mambo yatakuwa magumu sana huku, kwa sababu kuna mambo makubwa hapa ndani anatakiwa ayasikilize…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, unaongea na kiti…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti na yeye awe ananiangalia na ananisikiliza…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam naomba ufuate utaratibu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ongea na kiti.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Sawa, ananiangalia kwenye *tv* haina neno. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza na Waziri wa Fedha ni kwamba iko miradi mingi inayokwenda na pesa nyingi zimekwama. Kuna magari mabovu, kila Halmashauri kwenye yadi zao wana magari mabovu mengi yamekaa. Haya magari yalikwenda pale kupakiwa yamesimama ni mabovu. Haya magari kwa nini yasiuzwe? Msajili wa Hazina amepita kukagua magari nchi nzima, yako kwenye ofisi zote, polisi kila mahali kwa nini hayauzwi haya magari tukapata pesa ili zirudi kwa wananchi huku chini zikafanye kazi? Kwa nini wanakuwa na vitu vibovu wamevishikilia, wanayasubili na yenyewe kwa ajili ya kuja pata urithi, nani aje apate urithi wakati sisi tuna shida leo? Yauzwe haya magari, watu tupate pesa huku za kuendesha ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pointi nyingine ninayotaka kuieleza hapa, nataka kumweleza Waziri suala la msingi sana ni suala la kilimo. Huko kwenye kilimo sasa hivi Serikali imeweza kutoa pesa kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, ruzuku ya petroli, dizeli na kila kitu, mabilioni ya shilingi. Kama tumeweza kutoa mabilioni ya shilingi kwenye ruzuku kwa nini tusitoe pesa zikanunuliwe trekta za gharama nafuu? *Massey Ferguson,* zikanunuliwa *Swaraj,* hizi trekta wakagawiwa wananchi kule, wakakopeshwa, wakapimiwa mashamba, hapa yuko Waziri wa Ardhi, wapime mashamba kwa Hati za Kimila zitumike kama dhamana, watu wapewe matrekta kule kwa ajili ya kuboresha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mitambo ya kuchimba visima, sasa kwa nini ile mitambo ya kuchimba visima kama wanaweza kutoa ruzuku kwa nini isingie tukaagiza mitambo mingi zaidi, ikapelekwa sasa Wizara ya Kilimo? Wizara ya Maji wanachimba visima vyao na Wizara ya Kilimo wakachimbe visima, tusitegemee kilimo hiki cha mvua, tulime zaidi ya mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano, nina eneo tu Sengerema, Sengerema imezungukwa na Ziwa kwa asilimia 68. Tunao vijana kule sisi Sengerema wamekaa katika makundi, leo mwaka wa tatu wanakaa wanasubiri kupewa mitambo ya *irrigation*. Waziri Jafo alisema, Waziri nanii, Waziri nani huyu? Waziri Bashe anasema kwamba anakwenda kutengeneza *irrigation* Kanda ya Ziwa. Wasilete miradi mikubwa ya bilioni nane, bilioni sita wanunue mashine za dizeli, mashine za *water pump* umeme sasa hivi upo kila kona, tufanye *irrigation,* sisi tuna uwezo wa kuzalisha na kulipa ile mikopo kwa haraka. Haya ni mambo ambayo wanatakiwa wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uwekaji wa stempu, uwekaji wa stempu wa *ETS* ni wa muhimu sana kwa manufaa ya nchi. Sasa bidhaa zinazowekwa sasa hivi yule bwana wakati anapewa kazi alikuwa na viwanda vichache. Leo viwanda vimekuwa vingi zaidi ya mia tatu, lakini kuna bidhaa nyingine bado zinatakiwa wakaweke mpaka kwenye majani ya chai, majani ya chai yanatengenezwa ya paketi wanatengeneza kila kitu, leo Mheshimiwa Waziri ameweka mpaka kwenye maji. Sisi tuna shida na kodi na hawa wanavyokuja kuweka basi kelele zipungue kwa sababu hao wenye viwanda vikubwa wanadai shilingi nane inayowekwa kule ni kubwa. Basi wakae na huyu mtu *SICPA* apunguze bei angalau shilingi tatu hivi viwanda sasa, hawa wawekezaji wetu wa ndani wakawalinde. Hakuna namna ya kulinda viwanda vya ndani isipokuwa kuvipunguzia mzigo uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekaji wa stempu uende kwenye bidhaa zetu ikiwezekana kwenye *cement*, sukari kila kinachozalishwa kwenye nchi hii kiwe kina nembo ya kwetu na hawa watu stempu zao, stempu wanaleta kutoka nje, kutoka

Uswisi kwa nini wasiweke kiwanda hicho cha kutengeneza stempu hapa hapa? Vitu vyote vikafanyika hapa hapa Dar es Salaam, kama ni Dar es Salaam au kama ni Dodoma tutakuwa tumepunguza mzigo mkubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi na ninachotaka kuomba kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, suala hili linalopigiwa kelele, hili la bandari. Suala la bandari, watupe fedha sisi Wabunge, huku tunavyozungumza twende Majimboni tukapige mikutano tuwaambie wananchi. Hakuna namna nyingine ya kwenda kueleza wananchi kutoa huu uongo, hawa watu walikuja na hoja ya kuzuiwa kufanya mikutano. Wakafunguliwa kufanya mikutano, wakaja na hoja ya Katiba mpya, Rais yeye ndiye alikuwa Makamu Mwenyekiti anaendesha hapa kiti cha Katiba mpya wakaikataa Katiba mpya na yeye ndiye alikuwa Makamu Mwenyekiti. Mwenyekiti wake amekufa, Mheshimiwa Sitta yeye akabakia, ndiyo Mwenyekiti sasa hivi wa Katiba, hilo na lenyewe limejifuta, wamehamia kupotosha kwenye bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende kule sisi tukawashughulikie, tukawaeleze wananchi ukweli kuhusiana na suala la bandari. Bandari ndiyo mlango pekee utakaokuja kututoa sisi kwenye matatizo, bandari ile inaingiza trilioni 1.6. Haiwezekani ikaingiza pesa ndogo kiasi hicho halafu tukaacha ile bandari ikaendelea kukaa pale. Walio wengi wanaopotosha pale ni waliokuwa na maslahi na ile bandari, wanandugu wa ile bandari wanapotosha, wanapewa pesa kwenye mitandao, wapotoshe kwamba bandari inauzwa, bandari inauzwa kwa lipi? Kitu kipo katika mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inahitaji tutoe elimu kwa wananchi waeleweshwe zaidi na sasa hivi hawana sehemu nyingine yeyote wanayotegemea kupiga kelele isipokuwa ni hiyo. Mheshimiwa Waziri awe na ngozi ngumu na ninachotaka kumwambia aendelee kusimamia, lakini awakumbuke wachomwa jua, hakuna namna nyingine ya kuweza kuwakumbuka wachomwa jua isipokuwa hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la mwisho ni suala la elimu. Haiwezekani tuna misitu kuanzia kule kwako, iko misitu Mafinga, Sengerema kule sisi Buyingi tuna misitu mingi, kwa nini Serikali isitoe *cubic meter* elfu kumi ikachana mbao za moja kwa nane au moja kwa kumi, wakanunua *square pipe,* tukatengeneza madawati nchi nzima? Watoto wanakalia mawe wakati tuna misitu imejaa hapa. Inakuwaje namna hii? Mheshimiwa Waziri wa Fedha angekuwa amekali mawe, angekuja kuwa Waziri Fedha? Khee! Inakuwaje namna hii lakini na Naibu Waziri wa Fedha wangekuwa wamekalia mawe wangekuja kuwa katika hali hiyo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusitengeneze madawati nchi nzima? Madarasa yaliyotengenezwa kwenye nchi yote ya Mama Samia yalikuja na madawati yake, haya madawati yaliyokuwa ya Marais wengine waliotangulia, watoto wanakalia mawe kwenye nchi hii. Kwa nini tuna misitu mikubwa namna hiyo? Mafinga iko pale imejaa, *Sao Hill* imejaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie katika jambo hili, hili jambo ni gumu. Hatuwezi kujenga madarasa mapya, yale madarasa yaliyokuwa zamani yote yana hali mbaya, hayana madawati na hatuwezi kuwa salama sisi Wabunge kama watoto wanakaa chini, tuone huruma katika jambo hilo. Najua nchi ina mambo mengi, lakini kama tumeweza kutoa ruzuku, Wizara ihakikishe watoto wanakalia madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa waniunge mkono kabisa, hoja ya madawati iwe ni hoja ya nchi, hoja ya madawati ni hoja ya nchi, madarasa ni mengi hatuna jinsi. Walimu namna ya kuwafundisha hawa Watoto, wanapata tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, namshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kunijengea jengo la *TRA*, Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Waangalie Sheria za Kodi…

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na wachangiaji nilimwita, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Mwigulu, ahsante sana, hali siyo nzuri huku hela hakuna. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pia nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa. Nianze pia kwa kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba amefanya kazi kubwa sana kwenye bajeti hii. Nimpongeze Naibu Waziri na Timu nzima ya Wizara ya Fedha, jambo kubwa ambalo wamelifanya ni makusanyo ya trilioni 2.63, ama hakika mifumo waliyoiweka ya *EFD* na *ETS* ni mifumo mizuri na mifumo ambayo inatakiwa iendelezwe na iweze kusimamiwa ili tuweze kupata mapato mengi kwa kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inaenda kujibu changamoto za Watanzania, yako maeneo ambayo nimekuwa nikiyazungumza tangu bajeti zilizopita hasa eneo la elimu na leo ninao majibu ya Serikali. Tumezungumza kuhusu wanafunzi wa vyuo vya kati kupewa mikopo, Serikali imejibu hoja hii, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo haikutosha, Serikali imeenda mbali zaidi hata kwenye eneo la afya. Tulizungumza hapa kwenye Wizara ya Afya kwamba tuna changamoto sana ya dawa na Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* inahitaji kupewa nguvu ya Serikali ili iweze kujisimamia. Mheshimiwa Waziri amekuja na majibu na ameahidi na kwamba Bohari Kuu ya Dawa sasa haitakuwa kitengo cha dawa, itakuwa ndiyo bohari ya kutoa dawa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la *NHIF,* tunajua sasa hivi *NHIF* ndiyo huduma pekee ambayo tunaitegemea sisi Watanzania ili tuweze kupata tiba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ameamua sasa awalipe *NHIF* madeni yao, hiyo itawapa nguvu na sisi atakuwa ametusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko eneo la watumishi hapa. Serikali imeeleza vizuri eneo la watumishi na imesema itawapandisha madaraja, lakini pia eneo la watumishi hili Serikali imesema itawalipa madeni yao. Maana yake inatengeneza mazingira mazuri ya watumishi kufanya kazi. Nataka nikumbushe eneo moja muhimu sana, mtumishi anayestaafu anapata changamoto kubwa sana na changamoto hii yawezekana inasababishwa na namna ya kufikisha ujumbe wa mabadiliko anapokwenda kuhakikisha anapewa mafao yake, anakutana na kitu kinaitwa kikotoo, kikotoo hiki amekuwa hakijui tangu awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikumbushe hapo na najua kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Kabla ya 2018, mtumishi alikuwa anapata asilimia 50 na asilimia 50 anaendelea kulipwa kwa kila mwezi kwa miaka kumi na tano. Mwaka 2018 ikaja asilimia 25 kwa asilimia 75, hii ilileta kelele nyingi sana ikalazima kusimamishwa na mwaka jana 2022 tukaja na *formula* ya 33 kwa 67. Hapa nampongeza Mheshimiwa Rais kwanza kuongeza kufika hiyo 33, lakini bado 33 haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali katika hili. Mtumishi huyu anakuwa hajafanya maandalizi na anakuwa hajui huko mwishoni atapata nini? Sasa kwa kuwa tunahitaji tumwandae vizuri, ni vizuri *formula* hizi aweze kuzijua mapema ili aweze kufanya maandalizi, hilo jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tumpe *option* ajaribu kuchagua na tuweke kama utakubali 50 kwa 50 ama utakubali 33 kwa 67 ili mtumishi aweze kufanya maandalizi yake ya kustaafu vizuri badala ya huu mfumo ambao tunaendelea nao tunawatumia tu Vyama vya Wafanyakazi, tunawatumia Chama

cha Waajiri. Hawa hawawafikii walengwa, walengwa hawana taarifa, walengwa hawa ambao ndiyo wanasubiri wakistaafu wapate posho yao au wapate mafao yao wanapaswa kupewa taarifa mapema. Hili nataka niiombe Serikali ikalifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida tunalima sana alizeti na alizeti ndiyo *icon* ya Mkoa wa Singida, nembo kuu kwetu ni alizeti. Mwaka juzi amekuja Waziri Mkuu amehamasisha na alifanya mkutano wa wadau wa alizeti uliyojumuisha Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Singida lakini na Mkoa wa Manyara na tukawa tumekubaliana mambo ya msingi, lakini kulifanya zao la alizeti kuwa zao la kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana, wananchi wamezalisha kwa wingi na Mheshimiwa Bashe amekuja akatupa mbegu bora, wananchi wamezalisha sana, alizeti ipo ya kutosha ila alizeti imeshuka bei. Leo gunia la alizeti ni 35,000 maana yake kwa kilo ni shilingi 500, uandaaji tu wa kilimo cha alizeti una gharama zaidi hata ya hiyo fedha ambayo sasa ukienda kwenye kilimo cha mahindi, mahindi leo gunia ni 90,000, maana yake mwananchi ata–*opt* kwenda kulima mahindi leo hawezi kulima tena alizeti. Huko tunakoelekea zao hili sasa linaenda kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Nataka kuishauri Serikali, hapa tumeweka kodi ya ushuru wa mazao asilimia 25. Huko nyuma kabla ya kuingia kwenye *Covid-19* ilikuwa asilimia 35 wakati wa *Covid-19* tuliweka *incentives* tukapunguza, sasa hii asilimia 25 bado pia ni changamoto. Nataka kuiomba Serikali turudi kwenye asilimia 35 ili kulinda hili zao letu la alizeti. Hilo jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni lazima tuweke utaratibu wa kibali, hatuwezi tu kumruhusu mtu kuagiza holela. Leo tuna upungufu wa alizeti zaidi ya tani 350,000. Sasa kama hawatalima zitaongezeka na usipotoa kibali maana yake huyu mtu anaweza kuagiza tani 500,000 zikazidi hata ule upungufu wetu, ndiyo tunaua kabisa zao hili la alizeti na mafuta haya ya

alizeti. Kwa hiyo nataka kuiomba Serikali, iweke utaratibu wa kibali na kibali kilitolewa kwa kuzingatia mazingira, kuna wakati wa mavuno huwezi kutoa kibali wakati huo, kibali kitolewe wakati sisi tunalima na kibali kitolewe kulingana na mahitaji yetu. Hilo ni jambo la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ukitoka hapa ukiwa unaelekea Singida mpaka kule Shelui kwa Mheshimiwa Mwigulu, Iramba pale njia nzima unaona mafuta yamezagaa. Nataka kuomba Serikali tuwe na soko la mafuta ya alizeti kwenye maeneo husika, ukitoka hapa ukiwa unaelekea Morogoro utaona mafuta yamezagaa, hapo hata *TBS* hawawezi kutupa kiwango cha mafuta ambayo yanauzwa pale. Hapa tunatakiwa tu–*brand* vizuri mafuta yetu ya alizeti na tuyatengenezee mazingira mazuri. Kama Waziri anaweza kutengeneza *shade* kwenye maeneo ya Dumila pale mbogamboga na matunda, kwa nini asitengeneze *shade* kwenye mafuta ya alizeti tukayapa thamani? Nataka kuiomba Serikali ifanye hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi sana kwenye eneo hili, nataka kuiomba Serikali irudi kufanya tathmini kwenye eneo la tozo, eneo la tozo la miamala tufanye tathmini tuone kwa kiwango gani mpaka sasa tumefanikiwa na tumeathirika kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nifanye rejea ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu, Profesa Benno Ndulu, aliwahi kusema mwaka 2019; kodi ya miamala ya simu ni *regressive* kwa maana kwamba alieleza naomba ninukuu kwa kiingereza; "*they do not discriminate across ability to pay.*" Hii haiwezi kutofautisha ya mtu mwenye uwezo wa juu na mwenye uwezo wa chini, wote wanakata sawa. Hili jambo la kwanza alisema. Jambo la pili, alisema; "*cause negative impact on usage and the tax base.*" inaleta matokeo hasi kwa watumiaji wa simu na walipa kodi. Jambo la tatu alisema; "*create negative effects on economic growth and job creation across the economy.*" Akasema pia inaleta matokeo hasi katika ukuaji wa uchumi na ajira. Maana yake kipato kikipungua na ajira inapungua. Sasa ni jukumu la Serikali leo kwenda kutathmini hali tuliyonayo sasa hivi katika hayo

makusanyo ambayo tunayafanya. Inawezekana tunaona tunakusanya kwa wingi lakini kumbe tunapunguza ajira kwa wingi, pia huo ukuaji wa uchumi unaenda kwa kusuasua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo yote ni ya msingi sana kuweza sisi kuyasimamia. Nataka nirudi kuipongeza Serikali, Singida Mjini tumepata mradi wa maji wa miji 28. Mradi huu ndiyo mradi mkubwa sana. Pia tumepata katika vitongoji vyetu 35 niwashukuru sana tumeweza pia kupata umeme na miradi inaendelea. Mheshimiwa Waziri nilimnukuu hapa alisema miradi yote ya Serikali ambayo iko kule akawataka viongozi walioko kule chini waweze kuisimamia na iweze kutekelezeka vizuri. Changamoto ninayoiona kuwaachia tu viongozi kusimamia bila kufanya *follow up* matokeo yake kesho tutarudi hapa kurudi kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiomba Serikali itengeneze mfumo mzuri. Mfumo ambao unafanya *follow up* ya miradi yote ambayo tumepeleka kule, iwe miradi ya ujenzi wa vituo vya afya, iwe miradi ya maji, iwe miradi ya nini tufanye *follow up* ili kuhakikisha kwamba tunapata taarifa zilizo sahihi na zinapokuja kusomwa hapa ziwe taarifa ambazo zinaleta tija na sisi turudi kuzungumzia vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mradi mwingine muhimu sana, tunauzungumza sana mradi wa *TACTIC* wa *World Bank.* Mradi huu naomba ufanyiwe kazi. Mradi huu unaenda kwa kusuasua sana. Kama fedha imetoka kwa nini fedha hii mradi usifanyike kwa Pamoja, hii habari ya *phases* inachelewesha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sima kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, wakati huo Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud anajiandaa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Anafanya kazi kubwa sana mama yetu. Tunampongeza na kumtia moyo. Tunajua kwenye uongozi kuna changamoto nyingi sana, yako mengi yanazungumzwa, mikataba kuingia hakuanza yeye walianza wengi, lakini maneno yanakuwa mengi. Mimi ninamtia moyo Mheshimiwa Rais aendelee kwa nia yake nzuri ya kutaka kuiopeleka Tanzania mahali pazuri, basi aendelee kufanya kazi na Mungu azidi kumbariki na kumpa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwenye bajeti zao, Waheshimiwa Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu wote kwa utendaji wao mzuri mpaka leo hii tunafikia mwisho wa bajeti yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoli – *handle* suala zima la Kariakoo. Nitakuwa mkosefu wa fadhila mimi Mbunge ambaye natoka Kariakoo. Kwa kweli amefanya kazi kubwa na niiombe Serikali yale madai yao wayaangalie kwa sababu miongoni mwa wafanyabiashara wa Karikakoo wengi ni wakinamama. Kwa hivyo, niwaombe muangalie akinamama wale jinsi gani wanaweza kusaidiwa ili kuondoa kero ile, wafanye biashara zao. Wana mikopo na mambo mengi tu lakini niiombe Serikali na nina imani Serikali hii sikivu itayatekeleza yale waliyoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii mchango wangu utajikita katika ukurasa wa 21, 19, 12, 23, 34, 25 na 26 kama muda utaniruhusu, hivyo nitaelekea kwenye miundombinu maji, kilimo, uvuvi na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na upande wa miundombinu napenda kuishukuru Serikali, kwa kweli hali ya Mkoa wa Dar es Salaam kwa upande wa madaraja tumefanyiwa

mambo mazuri. Tuna daraja *Tanzanite*, tuna daraja la Kijazi *Interchange,* kuna *TAZARA,* kuna Chang'ombe *VETA,* kuna Kurasini pale Uhasibu kulikuwa na kero kubwa sana. Magari yalikuwa yanajaa pale Kurasini, sasa hivi tumepata daraja, magari yanakwenda na yanaenda vizuri na tunapata muda wa kwenda kufanya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna madaraja mengine madogo tumejengewa, pale kutoka Bendera Tatu kwenda Gerezani, kuna watu hawakutarajia kama lile jambo linaweza kuwa, ukilinganisha na ile miundombinu ya reli pale chini, watu hawakutarajia. Leo hii pale ukienda utasema siyo Dar es Salaam hii ambayo tumeizoea, huwezi kujua kama hapa ni Keko. Ni jambo la kumshukluru Mungu na tunaishukuru sana Serikali na Mheshimiwa Rais wetu. Miradi ile mingi iliachwa katika awamu iliyopita lakini imeenda kwa kasi katika awamu hii, pia kuna miundombinu ya mwendokasi ya kutoka Mbagala mpaka Gerezani. Hiyo imekamilika tunashukuru sana lakini miundombinu ya kutoka Gerezani tena pia mpaka Gongo la Mboto nao watu wako *site,* wafanyakazi wako *site* na kazi inaendelea. Tunapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto kubwa. Mkoa wa Dar es Salaam hatulimi, tunachotaka kwetu ni barabara. Tunaomba Serikali mradi wa *DMDP* pamoja na kuzungumza juhudi zako Mheshimiwa Waziri tunaziona hongera sana, tunakaa na wewe, tunakaa na Wizara mbalimbali miundombinu kujua hilo, lakini tunaomba *DMDP* tu, ije Dar es Salaam. Nasema hivyo kwa sababu Dar es Salaam kama Mji tuna miji yetu. Kwenye Wilaya ya Kinondoni sehemu kama Hananasif - Kinondoni, Kinondoni - Shamba, Mwananyamala, Kijitonyama, Mwenge maeneo yale kwa sasa hayapaswi kuwa na barabara za vumbi, yale ndiyo maeneo yetu ya kujidai katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwa hiyo, tunomba Serikali iangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ilala Kata ya Mchikichini, Kata hii bado iko katika Wilaya ya Ilala na iko mjini sana, lakini ukiingia kule ndani vumbi tupu. Kwa hiyo, tunaomba sana mradi huu wa *DMDP* uje ili tuboreshe. Kwenye Jimbo la Segerea,

maeneo ya Buguruni, Segerea yenyewe na Kata ya Tabata. Haya ni maeneo ambayo ya kwetu kweli ni maeneo ambayo yana uwekezaji mkubwa na watu wana shughuli kubwa za kiuchumi tunaomba tupate lami. Ukonga yenyewe, maeneo ya Ukonga Kata ya Ukonga pale Magereza, bado ukiingia humo ndani tafrani, hakujatimia, kuna barabara ile moja inayoenda markasi sijaona barabara nyingine, ninaomba Wilaya ya Ukonga nayo pia ipatiwe barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbagala Rangi Tatu ndiyo *center* ya Mbagala isipokuwa ukiingia ndani Mbgala kwenye ile Kata ya Kibondemaji ni huruma, hakuna barabara ya lami. Tunaomba tuletewe barabara ya lami kutoka Mbagala Shule ya Rangi Tatu kuelekea Kwa Ndunguru kule bondeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa niende kwenye suala zima la nishati. Nimeona Serikali jinsi gani imeweza kuwapatia wananchi wake majiko na kuhamasisha watu kutumia mitungi ya gesi. Lakini mimi niombe kwa vile gesi asilia imeshakuja katika Mkoa wa Dar es Salaam, maeneo ya Mikocheni tayari inatumika, wameshuka mpaka Msasani, niiombe Serikali wawekeze katika gesi asilia. Gesi ile ishuike mpaka Tandale, ishuke iende Manzese, ishuke iende Ubungo, ishuke iende Temeke, ishuke iende Mbagala, ishuke iende Ukonga, ishuke iende Segerea, gesi ishuke iende maeneo ya Buguruni ambako kuna wananchi wengi Watanzania ambao wanaweza wakatumia na hali zao ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama gesi ile mtu ukiwekewa ndani kwa mwezi unaweza ukalipa 10,000 tu kama matumizi yako madogo. Ni kwamba itawapunguzia gharama Watanzania. Kwa hiyo, tunaomba sana tunajua mmetuambia miundombinu yake ya gharama lakini ni uwekezaji, gharama ile italipwa polepole kama tunavyolipa umeme na mambo mengine ina Watanzania pia watakuwa wamenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye upande wa maji. Kwenye suala zima la maji tunaipongeza Serikali, kwa kweli miundombinu ya maji inaridhisha, tumepata visima vile vya Mpera

na Kimbiji, tunapata maji. Lakini bado kuna changamoto. Wakati wa kiangazi maji Dar es Salaam inakuwa shida. Ni lazima nilitaje Bwawa la Kidunda, tukiwekewa Bwawa la Kidunda hao wananchi wanaotoka mitaa hii ya Mbezi, Kimara, Chuo Kikuu wote wale wanapata maji kutoka Ruvu. Kwa hiy,o tukichimbiwa lile bwawa pale Ruvu itakuwa halikauki. Wakati Mto Ruvu unakauka wataenda kufungulia lile bwawa wananchi wa Dar es Salaam na Mikoa ya Pwani tutapata maji kwa wakati wote. Naiomba sana Serikali waendeleze kama walivyoanza Mheshimiwa Rais amethubutu kwa jambo hili kubwa la kuweka Bwawa la Kidunda kulijenga sasa basi nawaombea heri tufanikiwe hili ili tuweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la uvuvi; Dar es Salaam imezungukwa na Bahari Kuu, Bahari ya Hindi imezunguka katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini wavuvi wetu bado. Katika maeneo ya Pemba Mnazi, tunaita Pemba Mnazi ina maana bahari (ukienda pale baharini unakuta bado wavuvi wanavua na vingalawa vidogovidogo) lakini ukienda Kimbiji unakuta kuna bahari, ukija Mji Mwema kuna Bahari, ukienda hapa Feri ndiyo kwenyewe lakini bado utakuta wavuvi wetu hawana vyombo vizuri vya kuvulia samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo niiombe Serikali na Wizara husika, waende wakawaone wavuvi wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, hata vile vianikio vya kuanikia dagaa wanaanika katika vitu visivyoeleweka na wengine wanaanika tu chini. Niombe hivi huu uwezeshwaji wa hawa wavuvi sijui wa nini, ni akina nani? Mbona kwetu hatujaona wapate hata boti za kisasa. Tunaomba sana Serikali iwasaidie wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja kwenye suala zima la afya. Kwenye afya, kweli Mkoa wa Dar es Salaam jamani tumejengewa Zahanati na Vituo vya Afya na Hospitali kubwa lakini maboresho ya Haospitali za binafsi yamefanyika ni jambo jema. Hospitali zipo na zipo kweli lakini changamoto kubwa ni Madaktari pamoja na Madaktari Bingwa. Ninashukuru mpango wa Serikali wa kuwazungusha wale Madaktari Bingwa wanatengeneza timu wanahama, leo wanaenda hospitali ya Kigamboni, kesho

wanahamia Temeke, kesho kutwa wanahamia Ubungo, keshokutwa wanahamia Amana, Mwananyamala. Hivyo ndivyo wanavyofanya lakini haitoshi ukilinganisha na idadi ya watu walioko Mkoa wa Dar es Salaam ambao sasa tunaelekea kwenye milioni sita kwa mujibu wa sensa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji huduma nyingi sana za afya na Madaktari wengi waje watutibu. Nawapongeza kwa hilo lakini naomba tupewe Madaktari na Wauguzi pia. Wauguzi wanafanya kazi kubwa kwenye hospitali zetu tunawapongeza na Madaktari wetu wote, wanafanya kazi nzuri tunawapongeza sana lakini bado tunahitaji ziada. Ziada siyo mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Mwenyezi Mungu akubariki, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud aweze kuchangia.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote napenda kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, pia napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na ndugu yetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa pamoja na juhudi zao zote wanazofanya kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na timu yake yote katika kutupambania sisi Watanzania kutatua changamoto mbalimbali zinazotukabili pamoja na bajeti nzuri hii waliotuletea, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu napenda nijielekeze kwanza kwenye sekta ya kilimo. Bajeti ya Kilimo sasa hivi imefikia bilioni 970.8. Ni safari ndefu, tumeanza mbali, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi hiyo katika

kutatua changamoto za wakulima pia kujiwekeza kwenye kilimo chenye tija kwa mwananchi mkulima lakini pia kwa faida ya Watanzania wote na Taifa letu kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana bajeti hii kwa kupunguza na kuondosha baadhi ya tozo na kodi mbalimbali kwenye sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na sekta zingine za kijamii. Napenda kuipongeza bajeti hii kuna mambo yametugusa sisi wananchi kwenye sekta zetu tunaofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu kwenye sekta hii ya kilimo. Napenda kuishauri Serikali kwanza naipongeza Serikali kwa kuongeza ruzuku kwa mbolea lakini naishauri tuendelee kujenga viwanda vingine vipya vya mbolea. Kwa zile malighafi za mbolea zinazopatikana ndani ya nchi tuendelee kujenga viwanda vyetu vya mbolea ili kukabiliana na changamoto hii, pia kukabiliana wakati itakapojitokeza majanga mengine na maafa huko duniani kwa sababu mbolea ni silaha kwenye kilimo chetu. Kwa hiyo, tukiwa na mbolea nyingi ya kutosha hapa nchini, tutaweza kutatua changamoto zetu bila kuagiza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya sukari. Bodi ya Sukari na Wizara ya kilimo imejipanga vizuri sana kuhakikisha tunakwenda kuongeza tija katika sukari lakini pia kuacha kuagiza sukari huko siku za baadae. Pamoja na hilo nia na dhamira ya Wizara ya Kilimo na Bodi ya Sukari ni kufufua Chuo cha Sukari kwa sababu sasa hivi tuna shida ya wataalam wa sukari hapa nchini, inalazimika wazalishaji kuagiza wataalam nje ya nchi. Kwa hiyo, mimi nashauri andiko lao hili lifanyiwe kazi ili kile chuo kifufuliwe na wanafunzi waanze kusoma ili tupate wataalam wetu wa sukari hapa ndani ya nchi tuepushe na tatizo la kuagiza wataalam mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu kwenye sekta ya uvuvi, nasisitiza tu uwekezaji Bahari Kuu uendelee ili tuweze kuingia kwenye sekta hii ya uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na kulifufua shirika la *TAFICO* liongezewe fedha kwa haraka ili

lianze kazi na mambo haya yaende sambamba kwenye sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazingira nashauri na mimi masuala ya nishati mbadala. Kutafutwe mbinu ya kupunguza gharama kwa mtumiaji mdogo wa chini ili kila mtumiaji mwananchi aweze kumudu gharama hizi za kutumia nishati mbadala ili kuepusha ukataji wa miti ambao unaharibu mazingira ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ajira Serikali inajipanga sana sekta mbalimbali kuhakikisha vijana wanapata ajira, lakini kwenye ajira kuna wanaopenda kilimo, wanaopenda uvuvi, wanaopenda na kazi nyingine. Lakini kuna na wengine kila mtu kwa kipaji hake na utashi wake anapenda kile ambacho anakipenda. Mimi nashauri bado tuling'ang'anie soko la ajira kwenye lugha ya Kiswahili. Sasa hivi vyuo vingi duniani vinaanzisha mitaala ya lugha hii ya Kiswahili, bado hili soko linaandamwa na nchi jirani. Tujipange kuhakikisha hili soko tunalikamata sisi Watanzania kwa sababu sisi ndiyo wenye chimbuko la Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea najikita kwenye amani na utulivu wa nchi. Bila ya amani bila utulivu wa nchi haya yote tunayoyapanga hayatatekelezeka ila nia ya Serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anaishi kwa amani na utulivu katika nchi yetu. Napenda kuwapongeza Marais wetu kwa juhudi kubwa wanayochukua kuhakikisha amani na utulivu wa nchi unakuwa sambamba na hali halisi ya maendeleo ya nchi. Wanajitoa nawapongeza kwa uvumilivu wao na ustahimilivu wao, mengi yanawakuta wanayabeba, binadamu kapewa kifua cha mbele na cha nyuma, yote wanayabeba kulingana na hali halisi inayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba viongozi wetu na wasaidizi wake ninyi Mawaziri wetu, muendelee kumpa moyo Mheshimiwa Rais, pia nasi tunaendelea kuwapa moyo ili mambo yetu ya kuwaletea wananchi wa Tanzania maendeleo yafanyike. Ninachotaka kusema baniani mbaya lakini kiatu chake dawa.

Viongozi wetu wanahangaika kutafuta miradi, kutafuta pesa kwa ajili yetu sisi Watanzania lakini sisi tunajifanya hatuoni. Naomba sasa Watanzania tuheshimu na tuthamini juhudi zetu zinazofanywa na viongozi wetu mbalimbali kwa sababu lililopo baharini lisubiri ufukweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanayofanyika kuna siku tutayaona na tutayafaidi sote, siyo hao viongozi wanayoyaleta. Sote Watanzania kila pembe tulipo, mafanikio haya tutayafaidi na tutajivunia hapo baadaye. Ndiyo maana nikasema lililoko baharini lisubirie ufukweni, tutaona na mwenye macho haambiwi tazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada ya mja kunena, uungwana ni vitendo, tenda watu wataona, majisifu weka kando, viongozi wetu wanatenda hawajisifu na tutayaona. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kuchangia jioni hapa nina matangazo mawili.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ambao ni watoto wake kutoka Kigamboni Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni kumi wa Mheshimiwa Josephat Kandege ambao ni Mwenyekiti wa CCM, Katibu wa CCM na viongozi wa CCM Wilaya ya Kalambo, karibuni sana viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi na mwakilishi wenu yupo hapa anaendelea kuchapa kazi. Mwenyekiti na Katibu wa CCM yupo wapi? Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea jioni kama nilivyosema na watakaoanza kuchangia ni hawa wafuatao; kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, pili, ni Mheshimiwa Deo Phillip Mwanyika akifuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege na orodha itaendelea kama ilivyopangwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**na**

### Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na uchangiaji. Nilimwita Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na wakati huo, wafuataو wawe wanajiandaa. Wa kwanza ni Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, halafu Mheshimiwa Jafari Wambura Chege na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia pumzi pamoja na uzima wa afya, kuja kujadili bajeti hii ambayo tunapanga maendeleo kwa ajili ya Watanzania na cha pili, nashukuru kwako wewe kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapokuwa ameudhiwa au amepata jambo ambalo linampa maudhi, basi wale wenzake

wanaompenda huwa wanamliwaza. Sasa kwa kuwa, mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunajua alipata maudhi na watu kwa kumsema vibaya hasa kwa kumbagua, kwa hiyo, nataka kumpa kijishairi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shairi hili linasema, *"Sharti uusafi moyo ukitaka kuwa mwema, uwafanyie wenzio kwa kubembeleza wema, watakuendea mbio upate kurudi nyuma. Wema uutekeleze bila ya kuweka tamaa, watu uwasikilize shida zao kusimama, kisha wema ukuponze ubaki unalalama."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba Mheshimiwa Rais alifanya wema kumtoa mtu gerezani na akafanya mengine makubwa tu, kumwachia baadhi ya rasilimali zake ambazo zilikuwa pengine zimeshafutwa, lakini bado ule wema umemponza mama, lakini hizi ni kama tasnia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 21 na 22 wa hotuba yake, katika *Paragraph* ya 146, alieleza pale mabadiliko ya Sheria ya *SDL* ambapo hii sheria inaitwa Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82. Mheshimiwa pale amefanya mabadiliko kwa kuweka 1/3 ya fedha zitakazopatikana na *Skills Development Levy* kwenda katika Wizara inayohusiana na kazi na ajira. Kwa hiyo, katika Wizara hii, kwa sababu kule kuna *program* ya kukuza ujuzi, *program* hii ya kukuza ujuzi ilikuwa iko chini, kwa maana hiyo tulikuwa tunashindwa kupata wataalamu. Kutokana na hiyo 1/3 itakuwa kubwa kwa zaidi ya mara 10. Kwa maana hiyo sasa, Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inashughulika na ajira na walemavu itapata hilo fungu kwa ajili ya kukuza ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali. Nampongeza na ninamshukuru Mheshimiwa Rais, amekwenda kukuza ajira kwa vijana wetu, anakwenda kukuza ujuzi kwa vijana wetu. Kwa nini? Tumetoka Shilingi bilioni tisa, kama tutaangalia katika *Volume IV,* kitabu kile *page* ya nne ya *Skills Development Levy* kutoka Shilingi bilioni tisa na kwenda kukaribia Shilingi bilioni

100 na kitu. Kwa hiyo, hii maana yake ni kwamba tunakwenda kujenga uwezo kwa vijana waweze kujiajiri. Pamoja na mama ametoa ajira, lakini pia vijana wanajengewa uwezo waende wakajiajiri. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali, tunakushukuru sana mama kwa kuwajali vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu. Fedha hizi, kama tunakwenda kukuza ujuzi tutengeneze *skilled labors* wa kiwango cha juu ili kuweza kumudu sasa kuingia katika Tanzania ya viwanda. Kwa sababu, mwanzo tulinadi Tanzania ya viwanda, lakini hatukuwa na watu waliokuwa na ujuzi katika sekta hizo. Kwa hiyo, tukajaribu kuangalia upande wa kukuza ujuzi ambapo tutavutia viwanda. Duniani hapa watu wote ambao ni wawekezaji wa viwanda wanatazama vitu kama mfano wa *availability of raw materials* na *skilled labor*. Sasa tukiwa na *skilled labor* ina maana tutaweza kutekeleza ile Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niishauri Serikali, kwa sababu kila sehemu wanakuza ujuzi, kila Wizara; ukitazama Wizara ya Kilimo wanayo hii *program* ya kukuza ujuzi, lakini pia Wizara ya Mambo ya Ustawi wa Jamii nao wanakuza ujuzi. Sasa tutazame katika *instrument,* ni nani ataratibu hili? Maana tukitapanya *resources* tutakuwa hatuna mratibu na tutakuwa hatuna namba ambayo tunataka kuijua kwamba hii sasa tumekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambayo ina kipato cha kati ilitakiwa iwe na *at least* asilimia 12 ya watu ambao wana ujuzi katika kazi, lakini sasa hivi tuko katika asilimia 3.6. Kwa hiyo, tunamshukuru sana mama, amewajali vijana wake. Vijana ajira zinakuja, mama ameweka Shilingi bilioni 112 katika kukuza ujuzi. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka niliongelee, Mheshimiwa Waziri amezungumza katika *paragraph* ya 151 ambayo ipo katika ukurasa wa 154 wa hotuba yake. Pale alizungumzia Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Mheshimiwa amependekeza katika 151 *LN,* kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba *(cotton)*

zinazotambulika kwa *HS Code 52.05, 52.06, 52.07,* anasema lengo ni hatua ya kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo kwa kuongeza thamani ya zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri hapa, lakini viwanda ambavyo tunavyo hapa Tanzania vinavyotengeneza hizi nyuzi za aina hii tuliyoitaja, wanatengeneza kwa ajili ya matumizi yao wenyewe na hakuna kiwanda kinachotengeneza kwa ajili ya mwenzie. Kwa maana hiyo, wanaonunua kutoka nje, huwa wananunua kwa sababu ndani hizi nyuzi hazipatikani, na viwanda vinavyotengeneza ukiwaambia labda walete *quotation,* bei yake inakuwa ni kubwa zaidi kuliko ile ya nje. Pia uwezo wa kutengeneza kibiashara, hakuna kiwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ililisikia hili ikajipanga kuwaalika wawekezaji na wawekezaji walikuja, lakini Serikali yenyewe ilishindwa kwa sababu, imeshindwa kutoa *incentives.* Walitaka *incentives,* imeshindikana. Kwa hiyo, viwanda hivi vilipokuja, vikakimbilia Uganda. Kule Uganda wananunua umeme kwa senti nne. Sisi senti 10 ya Dola. Sasa ukienda Zimbabwe wananunua kwa senti nne. Hapa ni senti kumi. Uganda wamehakikisha wanawanunulia pamba wanawawekea kwenye maghala. Kwa maana hiyo, *availability of raw materials* imehakikishwa. Sasa sisi hapa kwetu haiko hivyo. Isitoshe, tukisema kwamba tumekipandishia hiki kiwanda asilimia 25 tunaenda kuua biashara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii tulitembelea kuangalia wafanyakazi. Pana wafanyakazi 8,700, ukisema hiki kiwanda kinashindwa kufanya kazi, umeondoa ajira za watu 8,700. Isitoshe Afrika Mashariki ushuru ni asilimia 10, Kenya Halimi pamba, lakini anatumia hiyo asilimia 10, Uganda asilimia 10. Sasa sisi tunashindwa kuingia katika ushindani. Soko letu tunalotumia, tunauza *AGOA,* tunauza *South Africa* na katika nchi nyingine. Wenzetu zinapatikana bidhaa zao kwa bei rahisi na sisi kwetu zinafeli kupatikana hizi bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, tujaribu kuangalia kwa sababu siyo kosa la kiwanda, ni kosa la Serikali kuweka *incentives,* kiwanda kimeshindwa. Tuweke *incentives* katika umeme, pia tujaribu kuangalia mazingira yote ya hivi viwanda ili vitusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Naomba Mheshimiwa Waziri aje atupe majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ukisikia kengele ya kwanza, basi ile ya pili angalau ujaribu kuwasiliana na kiti kuona kama nimeashiria muda wako pengine umeisha, endapo utakuwa hujasikia kengele ya pili.

Nilimwita Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya bajeti kuu iliyoko mbele yetu, pamoja na mwenendo wa uchumi wa nchi yetu. Nianze kwa kumpongeza sana ndugu yangu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Daktari wa Uchumi; Naibu Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu wote ambao wapo katika Wizara hii na watendaji wote kwa ujumla. Kwa kweli, wameleta bajeti ambayo inatupa mwelekeo mzuri wa tunakokwenda na tunakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu unakwenda vizuri, unaonesha uhimilivu. Sekta ya benki inaonekana ina afya, lakini siyo hilo tu, mapato yetu ya ndani yamezidi kuongezeka mwaka hadi mwaka pasipo kutumia nguvu kwa utawala wa sheria wala bila mabavu wala kuwindana. Dalili inaonesha kabisa kwamba mambo haya hayaji kwa bahati mbaya, ni kwa sababu ya uongozi mahiri wa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kuwa na maono mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imekuja na msukumo mkubwa sana kwenye sekta ya binafsi. Tumeweza kuona mambo

mengi ambayo yamekuwa yakifanyika na yanayoonekana yatafanyika katika kipindi hiki cha mwaka unaokuja, yanayoashiria ni kwa namna gani Serikali sasa inaona sekta binafsi ni muhimu kwa ajili ya kukua kwa uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Sheria ya Kwanza ya *PPP* ambayo imetengenezwa kwa ajili ya kuleta sasa miradi ya sekta binafsi ya kimkakati. Tumeona hatua nyingi za kikodi, nisingependa kuzitaja hapa kwa sababu ya muda, lakini nitaje moja tu kwenye eneo la sekta ya madini ambako kwa kweli kulikuwa na ukakasi mkubwa wa kuweka vifungu ambavyo havitabiriki katika sekta ya madini ambavyo vilikuwa vinazuia kutafuta fedha pale ambapo ungeweza kutumia *shares* zako za kampuni ambayo iko hapa ndani kwa ku-*invite* wanahisa wale wale au wanahisa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Sheria ya Kodi ilikuwa inaonekana kama ni *deemed realization* na kwa hiyo, ilikuwa ina-*attract* kodi. Sasa hiyo imeondolewa na nina uhakika sekta yetu ya madini inaenda kupaa kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi ambayo yamefanyika, lakini napenda niliongee lingine moja kuhusu mambo ambayo Serikali imeamua kuyafanya kwenye uthibiti. Kwenye *BRELLA* kulikuwa na ukakasi mkubwa sana, nami nilikuwa kwenye Kamati ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara ambapo tulikuwa tumetoa maoni kwamba ni vizuri Serikali ikaangalia, kule ndipo kwenye *MSMEs* nyingi zinakuwa *registered,* lakini kwa mfumo uliokuwepo ilikuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu uchumi wake umekua, sasa tunaongelea Shilingi bilioni 85.4 na umetoka bilioni 69.9. Ni nchi ya sita na tuna nchi tano juu yetu. Kwa jinsi ninavyoona, uwekezaji unaoendelea, hali ya kutabirika inavyozidi kuwa katika nchi yetu, miradi ya mikakati, uwekezaji katika sekta ya *LNG* na rasilimali tulizonazo, bila kusita uongozi kamili, barabara, mahiri wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nadhani katika miaka michache ijayo, lazima nchi hizi tatu za juu yetu tutazipita kama tutakwenda katika mwendo tunaoendanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea sekta moja kwa undani kidogo. Sekta ambayo nadhani ingeweza kuwa na mchango mkubwa zaidi katika uchumi wetu ni sekta ya isitu. Sekta hii ni kubwa, lakini mchango wake kwenye uchumi ni mdogo sana. Sekta hii kwa nchi nyingine ni sekta inayoleta mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi nyingine, lakini sekta hii inaweza kutusaidia kuokoa fedha za kigeni. Sasa hivi pamoja na ukuaji wa uchumi hapa nchini, lakini bado tuna tatizo la kwamba *balance of payment* kidogo tuko kwenye *deficit,* kwa sababu, bado tunaagiza vitu vingi kuliko tunavyopeleka nje. Kwa hiyo, sekta hii ya misitu inaweza ikasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni sekta jumuishi, inatoa ajira nyingi sana, ina uwezo mkubwa wa kuchochea viwanda mpaka ngazi ya vijiji. Ndiyo maana lazima Wizara na Serikali iangalie hii sekta kwa makini sana, kwa sababu mwisho wa siku sekta hii ina uwezo mkubwa sana wa kuchangia mapato makubwa kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhalisia, sasa hivi ukichukua mti wa mbao unaweza ku-*recover* asilimia 30 tu peke yake. Asilimia 62 ya mazao ya misitu ni mbao. Uki-*process* mbao hizo utapata katika meta za ujazo 200,000, uta-*recover* meta za ujazo 80,000. Kwa bei ya shilingi 250,000 utapata shilingi bilioni 24. Hiyo ndiyo *value* ya *container* moja la mita za ujazo 200,000. Ukienda kwenye mazao ambayo yamehandisiwa katika magogo ya mita za ujazo hizo hizo 200,000 unaweza uka-*recover up to 80 percent* ukapeleka kwenye *MDF.* Ukisha-*recover* hiyo unapata meta za ujazo 170,000. Bei ukiwa China kwa hiyo *MDF,* ni shilingi 600,000. Maana yake ni kwamba, hizo meta za ujazo 200,000 unaweza kupata shilingi bilioni 102. Kutoka shilingi bilioni 24 kwenda shilingi bilioni 102. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukichukua hilo *container* la ujazo wa 200,000 linaweza likazalisha *pieces* 283,000. Hizo *pieces* zinaweza zikazalisha *furniture.* Kwa bei ya China, *furniture* hizo ambazo sisi tunanunua hapa shilingi milioni 10, zinauzwa shilingi 800,000. Maana yake ujazo wa hizo mbao unaweza ukapata shilingi bilioni 226. Kwa hiyo, umetoka kwenye Shilingi bilioni 24

ambayo tunapata hapa, kama tungekuwa tumeongeza *value* tungepata shilingi bilioni 102, lakini ukipeleka kwenye *furniture* unapata shilingi bilioni 226. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sekta hii inatakiwa iangaliwe. Ukiangalia *TFS* wana mashamba karibu 11. Mashamba hayo yanazalisha karibu *TCF* 1,300,000. Sasa mimi nimechukua 200,000 tu peke yake, uki-*multiply* hizo na uzalishaji wetu wa mwaka mzima wa 1,300,000 mara 200 hata *calculator* inakupa *error*. Maana yake ni *trillions of money* tunazipoteza kwa kutokufanya *value addition on a serious way* katika nchi hii. Kwa kweli, hii *forestry is gold by itself*. Inaweza ikatuzalishia kuliko hata dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama *Vietnam,* juzi juzi tu tulikuwa na uchumi sawa sawa kabisa, lakini Vietnam wameingia kwenye eneo hili la *forestry* wame-*move*, na sasa wana-*export* mazao ya misitu kwenda nchi nyingine bilioni saba walianza mwaka 1989, wamepanda wakafika bilioni 12. Sasa *target* yao ni bilioni 25 kwa misitu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema, Wizara inatakiwa iliangalie hili eneo kwa ukaribu sana. Cha kufanya kwanza ni ku-*import technology* ambazo ni rahisi, ambazo zitasaidia sisi kuingia kwenye uhandisi wa mazao ya misitu. Tunaomba sana kwa kuanzia tu watupe *zero rating* katika *importation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la madawati, mtu amelia hapa; tuna uwezo mkubwa wa madawati. Kuna vijana hapa wana uwezo mkubwa wa kutengeneza madawati 1,500 kwa siku. Tukiweza kuwa-*empower,* tunasema tutatengeneza mabilionea, mabilionea tuanze kwa kuwa-*empower* watu watu watumie *soft wood* kutengeneza madawati ya nchi nzima, inawezekana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** …*proposal* ilikuja lakini mtu mmoja akadhania kwamba watu wana maslahi binafsi, tukapoteza miaka mitano ya kutengeneza madawati, sasa tunatumia madawati ambayo kwa kweli bado tunalia kilio kikubwa katika madawati. Tuna mbao,tunahitaji *technology* tunaweza tuka-*import* halafu tukatengeneza madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Deo Mwanyika. Nilitaka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba ni dakika nane kila mmoja kutokana na idadi ya watu kuwa kubwa sana, na tunapenda kila mtu apate fursa.

Tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Jafari Chege, wakati huo Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta anajiandaa.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kukushukuru mwenyewe binafsi kwa kuridhia na kunipa nafasi na mimi niweze kutoa maoni yangu kwenye bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ilivyo ada, nianze kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kuwa nzuri anayoifanya, hasa mwenyewe kwenye jimbo langu. Hivi nimeongea na Mwenyekiti wiki hii ninaambiwa tumepokea zaidi ya milioni 570 kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hivyo, nilikuwa na milioni 470 kwa mwaka uliopita pia kwa ajili ya sekondari mpya ya kata isiyokuwa na sekondari. Naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anatushika mkono sisi wananchi wa Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa na changamoto ya maji, lakini ninavyosema sasa hivi, katika miradi ya miji 28 tumepewa zaidi ya shilingi bilioni 132 kwa ajili ya

utekelezaji wa maji na sasa tunajenga tanki la lita milioni sita kwa ajili ya kuhakikisha tunasambaza maji kwenye Wilaya yetu ya Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana pia kwa kutupa fedha kwa ajili ya ujenzi wa *VETA*. Kubwa kuliko yote, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kuingiza barabara yetu ya Mika–Utegi–Shirati–Kirongwe, kwa ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ulione hili kama fursa, kwa kuwa mama tayari sisi ametukumbuka na ameliweka kwenye bajeti, sasa iende ikatengewe fedha, itangazwe kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 56 ili angalau barabara hii kwanza inakwenda kufungua uchumi wa Wilaya ya Rorya pamoja na nchi jirani, lakini pia inakwenda kufungua uchumi wa Mkoa mzima wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi kama Serikali, kwa sababu barabara inakwenda kutuunganisha kati ya nchi na nchi, naamini kabisa mnakwenda kuvuna na kupata mapato kwa asilimia kubwa sana kupitia barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna kwanza ulivyojipambanua kwa namna ulivyokuwa unawasilisha hoja. Lakini pili, kwa namna unavyoendelea kumshauri Mheshimiwa Rais kusimamia sera zinazohusiana na sekta na Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa mambo matatu; la kwanza, nikushukuru sana kwa namna ambavyo umeweza kumshauri Mheshimiwa Rais kuridhia na kufuta ada kwa wanafunzi ambao wanasoma vyuo vya ufundi. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri hili umewasaidia sana wananchi wanyonge, hasa sisi Wabunge wa vijijini hili lilikuwa ni kimbilio kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; ni kuridhia kwenye vyuo vya kati kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi angalau waliochaguliwa kwenda maeneo hayo. Kwenye hili Mheshimiwa

Waziri ningeomba nikushauri na ulitazame na ninaamini mwishoni uweze kuliwekea majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati unatoa hotuba yako hapa ulijipambanua hadharani, wazi kabisa, na wananchi wote walikujua kwamba wewe ni mtoto wa mkulima, ni mtoto wa mfugaji, na umelelewa katika mazingira magumu sana. Wapo wananchi huko chini Mheshimiwa Waziri, kwa huu huu mkopo ambao tunakwenda kuutoa, maana yake ni kwamba tukisema tunatoa kwa badhi ya wanafunzi waliochaguliwa kwa baadhi ya kozi na kozi nyingine tusiwape mkopo, tunakwenda kutengeneza mpasuko sana huku chini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, litazame Mheshimiwa Waziri; leo mtu na jirani yake, anamtazama mtoto wa kwake anakwenda kusoma chuo fulani anapewa mikopo lakini huyu ambaye amechaguliwa na Serikali kwenda chuo fulani hapewi mkopo, lakini wote wanaishi maeneo yaleyale, wote ni wajane, wote hawana fedha na wote ni maskini kabisa wa kutupwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ulione hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimechangia hapa, na ninaamini wananchi wanakuona, na wewe umejipambanua kama *role model* wa aina ya jamii fulani wanaotoka huko, litazame hili, ikiwezekana wanafunzi wote wanaokwenda kwenye vyuo vya kati wapewe mikopo, haijalishi huyu anakwenda kusomea nini na anasomea nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ukirudi nyuma, hata huyu ambaye hakupenda asome yale masomo kwa mfano ya sayansi, ukirudi nyuma kwenye historia unaweza ukakuta si sababu yake, hakuwa yeye ndiyo chanzo cha kutokusomea sayansi. Unajua shule zetu zina changamoto nyingi sana za walimu wa sayansi kwenye baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiwatoa wale ukasema hawa kwa sababu wamechaguliwa kwenda kozi fulani kwa hiyo hawastahili kupata mkopo wanakwenda kupata wanafunzi fulani, utatutengenezea deni kubwa sana sisi Wabunge ambalo tulikuwa

tumelitua, kwa msaada huu tulikuwa tumelitua. Nilikuwa na wanafunzi zaidi ya 50 ambao walikuwa wanatarajia angalau kufika mwezi Septemba tuwachangie kwa ajili ya kwenda kulipia ada, na ada ya vyuo unaifahamu, ni zaidi ya milioni moja mpaka 1,400,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, sasa litazame; kama mzazi alikuwa anashindwa kulipa 70,000, mama yetu kwa huruma yake akaamua kuiondoa hiyo 70,000 ya ada, leo 1,400,000 huyu mzazi anakwenda kuitoa wapi? Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri utakapofanya majumuisho, ulikuwa una nia njema, lakini tukiliweka katika mazingira haya tunakwenda kuwagawa Watanzania na haitakuwa imependeza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia kwa namna ambavyo umeendelea kumshauri Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kuondoa *VAT* kwenye nyumba zinazojengwa za kibiashara zenye gharama chini ya milioni 50. Wito wangu ni nini kwenye hili; *real estate developers,* hasa *National Housing, TBA* na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inayofanya kazi ya *development* ya ujenzi wa nyumba, waitumie hii kama fursa ya ujenzi wa nyumba hizi za gharama nafuu ili waendane na malengo na dhamira yako iliyokusababisha kumshauri Mheshimiwa Rais. Ili angalau nyumba za bei nafuu zisizozidi milioni 50 zijengwe maeneo yote ya nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani niwaone Rorya wakija wanajenga nyumba milioni 25 kwa ajili ya kuwasaidia watumishi. Waende halmashauri nyingine wajenge nyumba milioni 30, nyumba milioni 35. Kwa sababu hawa *real estate developers* walikuwa wanalia kuhusiana na bei ya nyumba, na wananchi wengi walishindwa kulipia hizi nyumba kwa sababu ya ongezeko la *VAT,* na Mheshimiwa Rais ameridhia kuiondoa. Ninatamani sana hizi taasisi ziweze kujikita kutumia fursa hii kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, lingine ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Kwa mujibu wa sheria hii ambayo tunayo hapa; *The Land Use Planning Act No. 6*

ya mwaka *2007* inaipa mamlaka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, hawa ndio wanapewa mamlaka makubwa ya kupanga na kuainisha matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye mpango wako wa Tatu wa Taifa wa mwaka 2022/2023-2025/2026, anayekwenda kutafsiri ile asilimia 50 ya kuainisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ni hii Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi; anayekwenda kutafsiri Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 120, kwamba ni lazima tutakapofika 2025 vijiji viwe vimepangwa matumizi zaidi ya 4,131 ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayekwenda kutafsiri hotuba za viongozi zinazozungumzia mpango wa matumizi bora ya ardhi ni hii tume. Na ndiyo maana kwenye sheria hii hawa ni *National Planning Authority* ambao kimsingi wanatakiwa wasimamie haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe Mheshimiwa Waziri utakuwa shahidi, hawa watu wamefanya kazi kubwa sana Msomera**,** wamefanya kazi Loliondo, sasa hivi wako Bunda, wanafanya kazi Tarime. Na hawa ndiyo wanahakikisha wanapanga matumizi bora ya ardhi kwa wale wananchi waliohamishwa Ngorongoro kwenda kule Msomera**;** wamefanya kazi kubwa sana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ninachosikitika kwa mara nyingi, na nimekuwa nikilisema sana hili; ni kwa nini tume hii, moja, hatuipi meno, lakini mbili, hatuitengei fedha nyingi ili iweze kuendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, maelekezo ya Mheshimiwa Rais, lakini iendane na Mpango wako wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa. Kwa sababu inaonekana kama ni kitu ambacho hakipo na hakina umuhimu wake. Lakini ninyi ni mashahidi Mheshimiwa Waziri; kama tunataka tuondokane na migogoro nchini ni lazima tume iongezewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wengi tumekuwa tukishauri hapa, kama tatizo ni fedha na nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, mwaka jana tulichangia ukaridhia kuongeza fedha ukawapa bajeti zaidi ya bilioni 5.4. Mwaka huu naambiwa

mmeishusha, mnawapa bilini 3.7, na wakati malengo ni yaleyale, na hatujafikia dhamira ya Ilani, hatujafikia dhamira ya Mpango wa Tatu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, nikuombe, kwa sababu tuna fedha ya mkopo, ile bilioni 345 mmege zaidi ya bilioni 20, bilioni 30, muwape hawa watu ili waende wakapange watumizi bora ya ardhi nchi. Na ninaamini kabisa kwa kufanya hivyo watakuwa wanatimiza na wanaendana na malengo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Jafari Wambura Chege kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, wakati huo Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas anajiandaa.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama Bungeni siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wananchi wa Urambo kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya ya kuleta maendeleo nchini. Na wakati huohuo niwatakie kila la heri Wizara ya Fedha, ikiongozwa na Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote, kwa sababu kazi ya bajeti si mchezo, ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wananchi wa Urambo tunangojea mradi wa maji kwa hamu sana. Kwa hiyo, tunaomba bajeti hii iwezeshe mradi wa maji ya kutoka *Lake Victoria* kuja Urambo kuanza kwa sababu tumeusikia kwa muda mrefu, tunaomba sasa mradi huo uanze. Kwa hiyo, lini Serikali itaanzisha

mradi huu wa maji ili na sisi tufaidike na maji kwa sababu ya shida ya maji tuliyonayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili ni shida ya nishati. Tuna kituo cha kupoozea umeme kinachojengwa Urambo ambacho tunaamini kitatupunguzia shida ya umeme wilayani kwetu. Lini kituo cha kupoozea umeme, *TANESCO substation,* kitaanza kufanya kazi ili na sisi tupunguze matatizo ya nishati tuliyonayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo, naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ya kujenga shule, madarasa tumeona mengi, lakini pia vituo vya afya na hospitali. Ombi langu leo kwa niaba ya wananchi wa Urambo ni kwamba tuna uhaba mkubwa sana wa wafanyakazi. Tunaomba bajeti hii tutakayoipitisha, kwa njia moja au nyingine iwezeshe kupata wafanyakazi shuleni (walimu), na wafanyakazi katika vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano shule za msingi tunahitaji walimu 627. Kwa upande wa sekondari tunahitaji walimu 78 ambao tunaamini watatusaidia angalau kupunguza uhaba wa walimu. Kwa upande wa afya ndiyo kabisa tuna uhaba wa wafanyakazi 476. Tunaomba bajeti hii tutakayoipitisha ituwezeshe kupata wafanyakazi wengi zaidi ili yale matunda ya maendeleo kwa kupitia sekta hizo mbili yaweze kuzaa matunda vizuri kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara; katika mambo ambayo yanachangamsha uchumi kwa haraka sana ni ujenzi wa barabara. Na tumeshuhudia sisi watu wa Tabora baada ya hii Barabara ya Manyoni – Chaya – Tabora kukamilika, hali ya wananchi imebadilika kule ambako barabara inapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo naiomba Serikali, kwa kupitia bajeti hii, ili kuamsha maendeleo ya kiuchumi Wilayani Urambo, tunaomba barabara ya Kahama itoke Kahama iwe ya lami kwenda Ulyankulu – ni kama kilometa 50 tu – ikitoka Ulyankulu inakuja Urambo, kilometa kama, yaani hata 40 hazifiki. Halafu

ukitoka Urambo kwenda Usoke ni lami, ukitoka Urambo kwenda Tutuo ni kama kilometa 70 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukipiga hizo lami kilometa 120 tayari watu wa Kahama mnaoniangalia ninyi Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mnatoka Kahama mnakuja Ulyankulu, mnakuja Urambo, mnakwenda Tutuo, mnakwenda Sikonge, moja kwa moja mpaka Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru Waziri wa Fedha ameniona, ni kweli Kahama – Ulyankulu – Urambo – Usoke – Tutuo – Sikonge – Mbeya, ninyi Waheshimiwa Wabunge wa Shinyanga mtakuwa hampitii Tabora, mtapunguza kilometa 70, mtakuwa mnapita kwetu Urambo ninyi, mnapunguza urefu wa njia. Kwa hiyo, tunaomba hii barabara ijengwe safi sana, hata Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba anakubali kwamba barabara ni safi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni lile ambalo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameliongelea sana; suala la wafanyakazi kupata haki zao. Nina majina ya walimu hapa, ambao walipandishwa madaraja mishahara yao haikurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipostaafu sasa kwenda kufanya mahesabu ya pensheni zao imekuwa ni vigumu kwa sababu mishahara ile ilikuwa haijarekebishwa. Kwa hiyo, mtu anapanda daraja lakini mshahara haurekebishwi, anapostaafu sasa kunakuwa na mapungufu ya hela kwa sababu mshahara wake haukurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini; nasema kwa ukweli nina majina ya walimu ambao walitoa hela zao wenyewe ili kuwezesha mafao yao yaweze kufanyiwa kazi. Kwa sababu wanaambiwa mwajiri wako alikuwa hajaleta hela kwa hiyo, anafanyiwa mahesabu kwa kupitia mshahara wa kwanza kabla hajapandishwa. Sasa yeye ndio anabaki anadai Serikali kile kiasi cha fedha alichoongezewa ili afanyiwe mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali yeti sikivu wafanyakazi wanaopandishwa madaraja mishahara yao irekebishwe ili waweze kufanyiwa mahesabu vizuri pale wanapostaafu. Nina imani kabisa na Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, na nahodha wetu akiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, suala hili tunapolizungumza tunaonekna kwamba linafanyiwa kazi, lakini bado kabisa. Nina ushaidi utakapotakiwa naweza kutoa nina jina la mwalimu hapa ambaye ametoa yeye mwenyewe fedha zake ili afanyiwe mahesabu ya pensheni; inakuwa siyo haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, kwa hao naomba sana Serikali izingatie, na hasa naona kabisa Mheshimiwa Waziri alivyojipanga hii bajeti itakwenda vizuri, ili yale mapungufu ambayo tunayataja sisi Wabunge yakifanyiwa kazi basi nchi yetu itaendelea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, wakati huo Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Shabiby wanajiandaa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hali ya uchumi wa Taifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha ujao, 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kabisa moja kwa moja niseme naunga mkono hoja hii, na wala sitasubiri mpaka mwisho wa mazungumzo yangu, nataka niseme mapema. Ninatamka hivi kwa sababu kule Kinondoni, na ndugu zangu wa Kinondoni na wananchi wa Kinondoni, tunaiona bajeti hii kwamba ni bajeti ambayo ina maono na matarajio ya wana Kinondoni, kwa hali kubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, nataka nimpongeze kwanza Mheshimiwa Rais. Na mimi sichoki kumpongeza kwa

sababu haya ambayo nitakwenda kuyazungumza yanaakisi pongezi zangu kwa nini nampongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze mwananchi mwenzangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, na msaidizi wake, Mheshimiwa Hamad, hawa watu wanafanya kazi vizuri. Nawapenda kwa sababu wako *creative,* wanatuletea mambo ambayo yanamgusa Mtanzania wa kawaida kila siku. Na haya ndiyo maono ya Mheshimiwa Rais, mnayatekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini nasema nataka Watanzania maana yake leo nazungumza na Taifa hili nikitoka Bungeni, Watanzania wanisikie huko. Kwamba pale Kinondoni kuna Kata inaitwa Kinondoni, ndiyo kata ambayo inachukua jina la jimbo, lakini jina la Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata ile kwa miaka yote hii tangu tupate Uhuru haijawahi kuwa na *secondary school. You can imagine.* Yaani hebu fikiria kata iko mjini lakini *secondary school* ya Serikali haikuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshukuru Mheshimiwa Rais, mwaka 2021 tukaja na ujumbe wetu hapa kuwaona Mawaziri wa TAMISEMI kuwaeleza matatizo tuliyonayo pale Kinondoni, wakatupatia shilingi milioni 600. Tunajenga shule ambayo ni afadhali imechelewa lakini ni shule ya kisasa. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu; hatukuwa hata na zahanati au kituo cha afya pale katika kata kubwa kama ile. Leo hivi tuna kituo cha afya cha kisasa kasoro tu mtutafutie madaktari wa kutosha na wauguzi, ili kisionekane kinapwaya, kitimie kabisa kile kituo cha kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niipongeze Serikali, ingawa hapa kuna tatizo kidogo fedha ambazo Serikali imetupatia nilivyokuja kuomba fedha hapa milioni 600

zikapelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya shule ya Sekondari ya Tandale. Mwaka 2021, Mheshimiwa Waziri na Mawaziri miliopo hapa, fedha zile hazikujenga *secondary school.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tandale ni mahali ambapo pana idadi kubwa sana ya wananchi, na hata mahitaji ya elimu kwa watoto wanaokaa pale, watoto maskini. Serikali ilifanya kitu wanaita *household budget survey* kuangalia hali ya umaskini inaletwa na nini. Kaya ambazo hazina watu ambao wamekwenda shule, wamepata elimu ili iwasaidie katika maisha yao huwa wanatengeneza umaskini, hasa katika maeneo ya mjini, kwa mujibu wa bajeti hii inavyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kule tumepeleka hela kwa ajili ya kujenga *secondary school, secondary school* haijajengwa. Natamani Serikali ichunguze sababu zilizofanya *secondary school* ile isijengwe na fedha zile zikapelekwa kwenye jimbo lingine. Hili jambo linanichukiza sana, linatia doa kazi nzuri ya mama Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifanyie utafiti kwa nini *secondary school* Tandale, mahali ambapo pana *primary schools* tatu bado wanashindwa kuweza kupata *secondary school.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niipongeze Serikali kwa kumalizia Mto Ng'ombe. Sasa hivi maeneo yale ya Magomeni, Ndugumbi na Makumbusho mafuriko hayapo, mmetusaidia sana kuokoa maisha ya wananchi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunalisubiri kwa hamu ni ujenzi wa Mto Msimbazi pamoja na Daraja la Magomeni. Hivyo watu wa Kinondoni wamekaa mkao wa kula wanasubiri hayo mambo. Nataka Mheshimiwa Waziri aje tu awatoe wasiwasi kwamba mradi wa Mto Msimbazi unaendelea kama ulivyopangwa. Ninajua sasa hivi watu wanalipwa fidia, kwa wale ambao watapisha mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niipongeze tena Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusanya mapato. Serikali imeonesha kwamba ukiangalia uwiano wa kodi na Pato la Taifa imejitahidi imefikia asilimia 12.5, hongereni sana. Lakini ningependa nione kwamba Serikali yangu inakusanya angalau asilimia 15 ya Pato la Taifa kama kodi kwa sababu huo ndio uwiano ambao utatusaidia kuondokana na bajeti *deficit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi kama Lesotho wanakusanya asilimia 30.8 ya Pato la Taifa, nchi kama Namibia asilimia 28.27, Zambia wanafanya vizuri asilimia 16. Ninapenda nione tunaweza tukajifunza mambo gani kutoka kwenye nchi hizi ili tuweze kukusanya mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo nilikuwa nikiliangalia halinipi furaha, nalo linahusiana na matumizi ya *EFD*. *EFD* inatusaidia sana kukusanya *VAT, EFD* ndiyo iko kwenye *story* ya kwenda kununua bidhaa ukinunua unaambiwa una risiti…ohoo!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha Mheshimiwa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba niiambie Serikali ifanye utaratibu wa kutumia mifumo. Elimu ya dai risiti toa risiti haitusaidii. Tangu *VAT* imeanzishwa mwaka 2010 mpaka leo miaka kumi na tatu bado tunaimba wimbo huo huo na watu hawatoi risiti. Sasa ningeomba mtumie mifumo ya *stock verification* na *stock controls* ili kuweza kuondokana na shida hii ya utoaji wa risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abbas Tarimba Gulam. Nilimwita Mheshimiwa Constantine John Kanyasu wakati huo Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Venant Protas na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo wanajiandaa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mapendekezo mengi na kwa kuchukua maoni ya Waheshimiwa Wabunge; na hasa katika maeneo ambayo tuliyasema kwa hisia kubwa. Kwa hiyo nianze kwa kuunga mkono hoja lakini nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo inafanya kwenye Jimbo langu la Geita na Mkoa mzima wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu kubwa hapa ni kushauri namna ya kutafuta fedha halafu tukatumie fedha ambazo tumeziomba kwa miezi mitatu. Mimi sasa nianze na eneo la madini. Kwa mujibu wa taarifa yako eneo la madini limekuwa kwa takribani asilimia 10.6; haya ni mafanikio makubwa sana. Lakini nina mapendekezo na ushauri katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza niishauri Serikali kuwekeza zaidi kwenye maeneo ya *CYP*. *CYP* tulizonazo ambazo ni za Serikali zilijengwa kama vile za majaribio. Sasa imethibitika kwamba wachimbaji wengi wanahitaji *CYP* nyingi ili kuweza kuongeza tija. Kwa hiyo Ofisi yako, Wizara yako itoe fedha nyingi kwa sababu kwa mujibu wa takwimu za sasa wachimbaji wanachangia takribani asilimia 40 ya dhahabu ambayo inauzwa nje ya nchi. Kwa hiyo hili ni eneo ambalo tunaomba Serikali iweze kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili katika eneo hili, tuna Watanzania wenzetu na raia wa nje wengi ambao wamekuja wakachukua *PL*, wamechukua *PL* wakatokomea; wengine wana miaka kumi, wengine miaka mitano na wengine miaka 20. Kila mwaka wanachokifanya ni kulipia na kujificha. Nimetoa mapendekezo katika michango yangu huko nyuma, kwamba wengi wanafanya kama vile kutegesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije na mkakati, mifumo ituambie kwamba huyu mtu ana *PL* hii kwa takribani miaka kumi na haizalishi na iweke ukomo wa mtu kukaa na *PL* bila kuitumia. Kwa sababu kama kuna wachimbaji wadogo wanachangia kwa asilimia 40 lakini tunaruhusu mtu anakaa miaka 20 na *PL* haitumii,

hafanyi nini, wakiingia wachimbaji wadogo wanaenda kufukuzwa ni sawasawa na kusema kwamba fedha tunazo lakini tumeshindwa kuzitumia. Kwa hiyo mimi nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tubadilishe utaratibu. Wachimbaji lazima wanapochukua *PL* watoe mpango kazi na waitumie wasipo itumia Wizara ipewe mamlaka ya kubadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili nakushukuru sana kwa kufanya marekebisho ya kodi, tulikuwa na mgogoro mkubwa sana kwenye kodi. Wachimbaji kila wanapokwenda kuuza walikuwa wanabishana na *TRA*. *TRA* akiona umeuza bilioni moja anajua hii ni faida, lakini palikuwa na gharama kubwa. Nakushukuru kwa asilimia mbili ambayo umeleta. Sasa ombi langu, mimi nimefanya biashara kabla ya kuwa Mbunge; tumepitisha asilimia mbili watu wako watakapoona watu wanafanya biashara na *turn over* inakuwa kubwa watageuka tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ofisi yako na watendaji wako waheshimu mambo haya ili turuhusu wachimbaji na watu wengine waweze kutumia mifumo ya kibenki. Kwa sababu wachimbaji walikuwa hawawezi kutunza hesabu; wachimbaji kwa *nature* ya kazi yao wanafanya kazi ngumu mpaka kuja kufika kwenye kuuza mazao kabla ya kuanza kupata faida. Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo mimi nakushukuru sana hapa; lakini naomba sana isije ikabadilika baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, tunakubaliana kwamba katika nchi hii tumezungukwa na mito, maziwa na maeneo mengine mengi kwa ajili ya kilimo na mifugo. Naomba niishauri Serikali; bado hatujatumia vya kutosha uwepo wa maziwa, mito, bahari na eneo la mifugo. Nimeangalia kwenye maeneo ambayo umeyawekea msisitizo; umeonesha kwamba unakwenda kufanya tathmini na kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais. lakini ukiangalia vizuri *nature* ya *failure* ya kwenye mifugo inategemea na uwezeshaji ambao mnaupeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *ranch* saba Tanzania, ukienda pale Mwabuki utagundua kwamba hawa watu wako dhofulhali,

wako pale wana mifugo ambayo imeshakaa miaka. Ukienda hapa Kongwa utaona jinsi shamba lilivyochakaa, lakini utashangaa ukija kwenye bajeti; hawa wanamiliki takriban watumishi 2,000 nchi nzima. Ukija kwenye bajeti leo kurugenzi inayowasimamia ina fedha nyingi kuliko watu walio kwenye sekta za utafiti. Sasa utaona hapa hakuna *seriousness.* Kama tunataka kufanya mabadiliko lazima tupeleke fedha nyingi zaidi huku kwenye *ranch* ili waweze kuzalisha mitamba mingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye taarifa, wamezalisha mitamba 1,000. Mitamba 1,000 kwa nchi ya watu milioni 60 huwezi ku-*transform* ng'ombe milioni 36. Wanatakiwa wapewe fedha nyingi ili wafanye mabadiliko. Tuwatoe wafugaji kwenye mifugo hii midogo midogo ambayo ina kilo ndogo, na wanakimbizana nayo kwenye mapori na Serikali ilhali maeneo hakuna tuwapeleke kwenye kufuga mifugo ya kisasa. Jambo hili haliwezi kufanikiwa kama Wizara haitoi fedha za kutosha. Tutoe fedha za kutosha kwenye utafiti na kwenye miundombinu. Tupeleke wataalam halafu wao wasambaze hii mitamba bora kwa wafugaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwenye uvuvi. Ukiangalia vizuri tumeanza kuzungumza uvuvi kwa miaka mingi. Wewe umesema umetoa *exemption* ya tozo na *VAT* kwa wanao-*export;* lakini nasoma kwenye taarifa yako sioni wapi umehamasisha uvuvi kwa kutoa kodi kwenye *fishing gears.* Kwa sababu kinachosababisha sasa hivi tunauza kidogo ni gharama ya uwekezaji kwenye uvuvi. Ili kuongeza uzalishaji wa samaki ziwani, Ziwa Victoria au baharini unahitaji kuwa na zana za kisasa. Tunahitaji kuwa na *out body engine*, tunahitaji kuwa na boti zenye *fiber,* watu wanahitaji kuwa na *fish finders nets.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo huwezi ukaongeza uzalishaji kwa sababu utakuwa una wavuvi wadogo wadogo wanaokomea mlingotini. Tumezungumzia mkakati wa Serikali wa kuanzisha boti za uvuvi leo takriban ni mwaka wa tatu ama wa nne lakini hatujaona *productivity* yeyote inayozungumzwa hapa. Kwa hiyo maana yake ni nini? Tunaendelea kuwategemea wavuvi wadogo wadogo ambao kwenye kodi hapa ni kama vile

wamekuwa *marginalized;* Serikali haikuonesha kwamba wanatakiwa wakuzwe walelewe waweze kuwa *productive* kwenye nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunataka kuongeza uzalishaji kwenye maziwa, na hasa kwenye kilimo cha Samaki Ziwa Victoria na maeneo mengine. Dunia nzima sasa hivi wanapata samaki wengi kwenye *cages* lakini *its too expensive* ku-*invest.* Hii ni kwa sababu mwanzo utahitaji zaidi ya milioni 50. Hakuna mvuvi wa Tanzania ambaye anaweza ku-*invest* milioni 50 kwenye *cages* akaanza kupata fedha baada ya mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia. Mimi nitachangia masuala ya Bandari yetu ya Dar es Salaam lakini si kwamba nitachangia kwa sababu labda kuna sintofahamu fulani lakini nitachangia yale ambayo hata kama kusingekuwa na uwekezaji lakini haya ningeyasema kwa sababu nilishasema kwamba nitasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza nataka niseme tu na nitoe rai kwa Waheshimiwa Mawaziri wetu, kwamba haya yanayozungumzwa na wananchi kuhusu kuboresha mkataba wa utekelezaji huu unao kuja ni lazima yazingaitiwe. Lazima tuzingatie mkataba wa utekelezaji, tusiyapuuze maoni ya wananchi kwa sababu si kila mwananchi anayechangia basi anakuwa mpinzani wa Serikali, Hapana. Wako watu wazalendo ambao wanachangia kwa manufaa ya nchi. Kwa hiyo tuchukue mawazo yao mazuri yaingie kwenye hiyo mikataba ya utekelezaji, tusiwaone kwamba ni watu ambao labda wanapinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, kwenye uwekezaji kwenye bandari ndugu zangu ni kitu cha msingi sana. Kwa nini nasema hivyo? Mimi niko kwenye Kamati ya Miundombinu sasa hivi nafikiri karibia ni kipindi cha nne. Kamati ya

Miundombinu tumetembelea bandarini pale zaidi ya mara tano sita. Ukisikiliza bandari kwa watu na yale mapato unayoambiwa kwamba yanakusanywa tofauti na faida wanayoileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape mfano tu; kwa mfano mapato ya 2021/2022 ilikuwa ni shilingi trilioni 1,144 (shilingi trilioni 1.14). Matumizi ni shilingi bilioni 805, faida ni shilingi bilioni 339. Kwa hiyo ukiangalia matumizi ni asilimia 73 faida ni asilimia 27 hilo ni tatizo. Kwa nini nasema ni tatizo? Faida ni ndogo matumizi ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia hata kwenye ushushaji wa mizigo; ushushaji wa mizigo 2019/2020 tumeshusha tani milioni 17.2; 2020/2021 milioni 17.6; 2021/2022 milioni 20. Sasa nia yangu ya kuzungumza ni kama reli ya *standard gauge* tunayoijenga ina uwezo wa kubeba tani milioni 25 peke yake ambayo imezidi uwezo wa bandari, hapo bado reli ya kati tunaifanyia ukarabati, bado reli ya *TAZARA* tunaifanyia ukarabati, bado kuna malori ya nchi nzima maana yake itabidi yasimame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama reli hii moja tu ya *standard gauge* ikichukua tani milioni 25 wakati bandari uwezo wake ni milioni 20 ina maana hakuna reli hata moja itakayofanya kazi. Sasa athari yake ni nini? Athari inakuja moja; kwenye malori tunaona kama yanaharibu barabara, yanaleta matatizo lakini ndio yenye mchango mkubwa na yenye ajira nyingi kuliko sehemu yoyote kwenye hii nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lori moja likitoka hapa kwenda Rwanda au Burundi linatumia lita 2,000 za mafuta, kodi ya Serikali kila lita inachukua shilingi 1,200, kwenye 1,200 ina maana Lori likienda hapa na Burundi katika lita 2,000 ina maana kodi inachukuliwa milioni mbili na laki nne kwenye *trip* moja ya Lori. Kwa hiyo lori likienda mara nne Burundi kwa Mwezi ina maana ni 8,800,000. Na ukiangalia mfuko wa barabara, nimeona hapa Wabunge wengi mnasema hapa barabara ndizo zinafungua uchumi. Barabara zinatengenezwa na magari kwa sababu zinatengenezwa na kodi ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama bandari yetu isipofanya vizuri, tunasema tu reli ikija barabara zitapona na mfuko gani utakaotoa fedha ya kutengeneza barabara kama malori hayatapata mzigo? Cha msingi ni kuhakikisha kwamba bandari inafanya kazi ya ziada kuhakikisha kwamba treni zinafanya kazi na malori nayo yanapata mzigo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukisema usimamishe malori ina maana umeshapoteza ajira zaidi ya milioni moja, kwa sababu tayari malori yapo zaidi ya laki moja kwa hiyo kila lori moja lina Tingo, lina dereva na mafundi. Ukija malori yanakopita kuna *guest houses* kuna, mama ntilie kuna kila aina. Ina maana miji yote ya pembezoni isiyopitiwa na reli nayo itakuwa ndiyo biashara yao imekufa. Kwa hiyo cha msingi tuzingatie kuweka mikataba yetu vizuri lakini lazima tuweke uwekezaji, bila uwekezaji haitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika kupitia bandari, tutabadilisha *Ma-MD* wa bandari lakini hakuna kitu. Nataka niwaambie nchi hii wazalendo ni wachache, wapigaji ni wengi. Pale pale bandarini utakuta mashine za kushusha unaambiwa zimekufa ilhali haizijafa halafu kuna watu wenye *tender* ya kuleta *Spear* wanaingia na kagari, wakitoka unaambiwa tumetengeneza milioni 500, kumbe ile mashine haijafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna kingine ambacho tulikigundua hata zile Meli ambazo zinapaki kule nje, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi mmesema amesema kwamba *demurrage charge* ni dola 25,000 lakini zipo Meli ambazo zinalipwa *demurrage charge* mpaka dola 35,000 ambazo ni takriban milioni 95, ile kupaki tu. Kwa hiyo wakiharibu hivi vifaa wanafanya mpango na hawa watu wa bandarini, wakiharibu vile vifaa zile meli kule zinatengeneza faida huku zimesimama kwa sababu wanalipwa *charge* ya milioni 95, ya milioni 58 mpaka 60 huku meli imesimama, kwa hiyo uwekezaji kwenye bandari ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Watanzania tusiogope uwekezaji, 2014 walikuja hapa Qatar kuja kuwekeza kwenye

ndege, tukaona aaa, amekwenda sasa hivi Rwanda Air. Rwanda Air asilimia 51 ni ya Qatar, sasa hivi anajenga uwanja pale iwe *hub;* kwa hiyo maana yake Watanzania, Wakenya, watu wa Afrika Mashariki na Kati tukitaka kusafiri kwenda Ulaya, kwenda wapi twende tena tukapandie Rwanda. Kwa hiyo tusiogope, kama uwekezaji Serikali ilishashindwa, imeshindwa, tuache wawekezaji lakini wawekezaji wenye mikataba mizuri yenye manufaa na nchi wawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni masuala ya viwanda hivi vya nguo. Muda umeisha au niendelee mzee kidogo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya nguo vya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, tumia sekunde 30 kumalizia muda wako, nyongeza hiyo.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nilikuwa nataka nizungumzie vitenge sasa hii habari ya sekunde thelathini haiwezi kutosha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea nilimwita Mheshimiwa Venant Daud Protas aweze kuchangia.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mmoja wa wachangiaji katika Bajeti Kuu ya Serikali. Awali ya yote nianze kwa kuipongeza Serikali kwa bajeti hii nzuri pamoja na utekelezaji wa bajeti iliyopita, kwa sababu tunakwenda mwishoni mwa utekelezaji wa bajeti ya 2022/2023. Na Mheshimiwa Waziri nikupongeze, yako mambo yamekwenda Jimboni kwetu ni mazuri mazuri. Hii yote imesababishwa na Mheshimiwa Rais lakini na wewe mshauri wake kwa upande wa fedha, umemshauri vizuri. Sisi tuleteeni fedha kwa sababu wananchi tuliwaahidi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza haraka haraka, kwanza mimi nianze kwa kuipongeza Wizara ya Kilimo. Mwaka huu imetusaidia, wakulima wengi waliitikia mwitikio mkubwa katika kujiandisha upatikanaji wa mbolea ya ruzuku na haya yote yalichangia baada ya Mheshimiwa Rais kuweka bilioni 150 kwenye mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo lakini bado tuna changamoto; changamoto iliyopo kama tumeweza kuweka ruzuku kwenye mbolea sasa Serikali ije na mpango mkakati wa kuweka ruzuku kwenye mbegu hasa za alizeti na mahindi ili sasa ziweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mzalishaji kama umempa mbolea, halafu akaenda kuweka mbegu zisizo bora ni sawasawa na bure. Kwa hiyo, nimshukuru Mheshimiwa Waziri nilipata tani moja, kama kilo 1,000 za alizeti, tayari nimekwenda kuzigawa kule na zimeleta tija sana. Kwa hiyo, mwaka huu aniongezee wakulima watalima sana, anipe tu tani 10 nikalime peke yangu kule Igalula na watu wameitikia kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Wizara ya Kilimo kuwa imefanya kazi vizuri, lakini niipongeze Serikali imeendelea kulipa fidia kwa wanaoidai Serikali. Niiombe Wizara ya Fedha, pamoja na changamoto nyingi wanazokabiliana nazo za kifedha, lakini kuna wananchi ambao wamepisha maeneo ili kupisha miradi ya Serikali wakiwemo wananchi wa Kata ya Kizengi ambao wanajengewa mzani pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANROADS* waliwambia wasiendeleze yale mashamba, lakini hadi leo bado hawajawalipa. Ni hela ndogo ambayo haifiki hata milioni 100. Naomba Mheshimiwa Waziri, akitoka hapa akawalipe tu ili waweze kupata fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, waliopitiwa na Mradi wa *SGR*. Kuna wakazi zaidi ya 30 ambao wamepitiwa na Mradi wa *SGR* kwa kigezo cha kwamba waliifuata reli (wako ndani ya mita za reli). Sasa, wale wakazi wamekaa pale zaidi ya miaka 30

hadi miaka 40. Nilifika hapa na hoja na nimwombe Waziri, kwa sababu Wizara ya Fedha ndio inayohusika na niliongea na Waziri wa Ujenzi, akaniambia niongee na Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, niombe kama hawa hawawezi kuwalipa ardhi, basi wawalipe majengo ili waweze kupata fidia kidogo ili wakajenge nyumba kuliko kuwabomolea na wawaache. Vile vile, Serikali ya Mama Dkt. Samia haitaki kuwaonea wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye mambo ya kitaifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kujenga na kuleta maendeleo ni lazima wananchi tulipe kodi na hili Mheshimiwa Waziri amekuwa anasisitiza na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia amekuwa akisisitiza sana. Mheshimiwa Waziri, jambo ambalo tunatakiwa tulifanye, la kwanza, Waziri anatakiwa akae na *management* ya *TRA*. *Customer care* ya *TRA* sio nzuri. Leo wanalazimisha watu wakalipe kodi, lakini wanavunjwa mioyo kwa sababu ya *customer care* ya *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mwananchi anatoka zaidi ya kilometa 200 pengine zaidi ya kilometa 250, anakwenda pale *TRA* siku ya kwanza ataambiwa mfumo, siku ya pili ataambiwa anayetoa *TIN number* ana msiba, siku ya tatu anaambiwa sijui kuna kikao gani. Sasa huyu ametembea kilometa 200 anakula na analala, ndio maana watu wengi hawalipi kodi kwa sababu ya uzembe wa watumishi wa *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali waongeze watumishi wa *TRA*, lakini wawe na kauli nzuri. Hata kama kuna changamoto ya mifumo waangalie namna ya kuwasiliana na mteja aruhusiwe kwenda halafu mfumo ukikaa vizuri wawasiliane ili aweze kuja kufanya usajili na baadaye awe mlipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linakera, leo ili uweze kukadiriwa, kwanza unakadiriwa hatua ya kwanza na baadaye mnatengeneza hesabu unapeleka. Leo

wanatengeneza risiti na wanasema tudai risiti na kweli watu wanadai risiti, lakini risiti zao zinakaa wiki mbili zinafutika. Sasa baadaye akija kuniambia nimeuza mauzo ya bilioni tatu, anasema nilete risiti, risiti zenyewe zimefutika kwa zaidi ya bilioni moja. Baadaye anakuja kumpigia tena kodi mfanyabiashara kwa ile hela ambayo anasema risiti yake haijapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali wakae na wataalam, mtu akifanya manunuzi inapoingizwa *TIN number* kwenye manunuzi yake, basi iwe *reflected* moja kwa moja *TRA,* iseme tarehe fulani ulinunua kitu cha milioni 200. Kwa hiyo, hesabu inakuja moja kwa moja ili kama akileta mahesabu, alete yale matumizi ambayo aliyafanya na ambayo hayajapita kwenye *TIN number* ikiwemo *Payee* ya mishahara na matumizi mengine ya kawaida ili a-*submit* pale wamtolee hesabu zao, kuliko sasa hivi unamwambia mfanyabiashara ndani ya mwaka mzima aandae risiti zake ambapo unakuta risiti zimefutika au zimepotea, baadaye *TRA* hawaelewi wanaanza kumpigia tena kodi ambazo sio rafiki kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri mwaka 2022 alikuja hapa na bajeti nzuri sana na akasema hivi anakwenda kubana matumizi ya Serikali. Nimwambie tu sehemu ambayo anaweza kusaidia Serikali kubana matumizi ni riba za wakandarasi. Hebu waliangalie. Kwa mwaka tunapoteza zaidi ya bilioni 800 kwenda trilioni moja. Sasa hizi fedha ukizi–*calculate* tunakwenda kuwapunguzia wananchi mzigo. Kwa hiyo, riba za wakandarasi Waziri akizidhibiti vizuri na kupunguza ukiritimba ulioko kwenye Wizara yake na watumishi wake wakawa weledi wa kulipa kwa wakati, nadhani haya mambo hayatokwenda kwa namna hii inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunalalamika hapa fedha tumekosa, lakini fedha za riba zinapatikana na wanakwenda kulipa kwa wakati, lakini fedha za kwenda kwenye matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kwa nini zinachelewa? Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri ang'ang'ane hapo hapo, abane matumizi lakini abane riba zisiendelee kupatikana katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka nichangie, takwimu ya sensa ya mwaka 2022 ilionesha Watanzania tuko milioni 62, lakini majengo yako milioni 14. Leo amekuja na bajeti ambayo inakwenda kuongeza tozo kwenye vifaa vya ujenzi hasa *cement*. Sasa ukiangalia kwa Takwimu kila nyumba moja wanaishi Watanzania wa nne. Leo tunakwendaje kuwasaidia Watanzania kujenga nyumba zao kuwa nyumba bora ambazo sisi wenyewe Serikali tunatoa maelekezo? Kwa hiyo, niombe hii tozo ambayo tunakwenda kuiweka kwenye *cement* haiendi kuwasaidia wananchi wetu wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali iangalie namna bora ya kuongeza hizi tozo katika bidhaa muhimu ikiwemo chakula hebu tuangalie kuweka msamaha. Ndio maana Watanzania hapa kuna wakati huwa wanajiuliza kwa nini makampuni makubwa yanayotoka nje yanasamehewa misamaha mingi ya kodi, lakini sisi wa ndani huku tunabanwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Venant Daud Protas. Nilimwita Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, wakati huo Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ajiandae.

**MHE. DENNIS L LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti hii ya Serikali. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Rais wetu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo inafanywa na Serikali yake. Kwa kiasi kikubwa bajeti hii ni ushahidi tosha kwa Bunge lako kwamba wamechukua kikamilifu maoni na mapendekezo ya Wabunge kuhusiana na maeneo ya vipaumbele katika kuibua fursa kwa wananchi wetu na kuimarisha uchumi wetu. Kwa hiyo, tunaweza kuona haya katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mikumi nina kila sababu ya kupongeza Serikali ya Mama Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa sababu ndani ya kipindi kifupi kabisa tumeona mambo mengi ambayo yalikuwa ni kero kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi yakipata suluhu ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo hayo ilikuwa ni suala zima la jibu la uhakika kuhusiana na soko la miwa la uhakika kwa wakulima wa Bonde la Mto Luhende. Tunaona Serikali kama Mbia wa Kiwanda cha Ilovo wamewekeza bilioni 571 kupanua kiwanda kile cha sukari ambacho kinakwenda kuwa suluhu ya kudumu kwa wakulima wa zao la miwa katika bonde lile. Pia, inaenda kuwa ni suluhu ya kudumu katika suala zima la uagizaji wa sukari kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona sekta ya kilimo inachangia pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 26.2, lakini pia inaajiri Watanzania kati ya asilimia 60 na 70. Vilevile tunaona kwamba ina ukuaji usioridhisha kwa asilimia takribani tatu ukilinganisha na asilimia tano kwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii sio njema sana kwa uchumi wetu kwa sababu tuna changamoto ya naksi ya bajeti katika urali wa fedha za kigeni. Vilevile tunaona kabisa moja ya suluhu ya kudumu ya changamoto hiyo ni kuzalisha sana mazao ya kilimo ambayo ni uti wa mgogo wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tunaweza kuona asubuhi tulikuwa na mjadala kuhusiana na bei ya mahindi. Pia, naomba nirudie tena, kama tunaweza tukawekeza fedha nyingi katika uzalishaji wa chakula, tunaweza tukapunguza bei tuka-*stabilize* thamani ya fedha yetu lakini pia tunaweza tukawa na uhakika wa chakula. Kwa hiyo, tunaweza tukampelekea mwananchi uwezo wa kuweka akiba. Pia tunaweza tukajikita zaidi kwa kuwawezesha wananchi wetu katika kuzalisha mazao ya biashara kwa ajili ya Soko la Dunia, fedha za kigeni na kwa ajili ya kuimarisha thamani shilingi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza mengi, lakini naomba niunge mkono Serikali kwa wazo la kuwa na Tume ya Mipango ya Taifa. Moja ya changamoto kubwa tuliyonayo ni

kwamba, tuna bajeti nzuri sana, lakini hatuna *coordination point,* hatuna sehemu ya uratibu ambayo inaweza ikafanya taasisi zetu na Wizara zetu zikazungumza, zikawasiliana na tukawa na Tume ya Mipango ambayo kwa niaba ya Serikali inaweza ika–*coordinate* mambo yote makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Kwanza, wa Pili na wa Tatu ni jinsi gani unavyozungumzia suala zima la viwanda na biashara, lakini *linkage* ya ukuaji wa suala la viwanda na biashara, suala zima la ukuaji wa kilimo na suala zima la utengenezaji wa barabara za vijijini kuwaunganisha wakulima na masoko, bado kuna changamoto. Hapo ndipo unaona kuna umuhimu wa kuwa na Tume ya Mipango ya Taifa ambayo inaweza ika– *ddress* mahitaji ta maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji ya uchumi wetu, kulingana na malengo ya ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naamini kabisa kwa ujio wa hii *National Planning Commission* unakwenda kutuletea mipango ya muda mfupi, kati na muda mrefu tukafanya maamuzi ambayo yatakuwa na tija kwa wananchi wetu, maamuzi ambayo hayatapendelea watu kwa sababu ya *influence* yao bali mahitaji ya maeneo kulingana na umuhimu wake kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba Sekta ya Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Pia, ni wazi kwamba dunia sasa hivi iko kwenye *knowledge economy* ambayo inahitaji uwekezaji mkubwa na ambapo hatuna fedha za kuwekeza huko. Hata hivyo, tuna maeneo kama ufugaji wa mifugo, uvuvi na kilimo ambayo yanatupa *advantage* ya ku–*compete* katika uchumi wa dunia, tuyashikirie hayo. Tukipambana kuyawekea nafuu ya kodi, ushuru, lakini i*ncentive* kwa wale wote wanaojikita katika maeneo hayo, nina imani kabisa uchumi wetu unakwenda kukua ili kukidhi matarajio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ardhi na mazingira. Ni wazi kwamba ardhi yetu haiongezeki ila Watanzania wanaongezeka, lakini mtaji mkubwa katika dunia hii ni ardhi.

Tunajua kwamba eneo kubwa la Tanzania bado halijapimwa. Ni vizuri kupitia bajeti hii tupime maeneo yetu, tupange maeneo yetu, tuendeleze maeneo yetu sio kwa sababu yetu ila kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo unaweza kuona hata upangaji wa miji yetu, maeneo mengi miradi yetu inakwama kwa sababu ya kutumia fedha nyingi kulipa fidia lakini tuna vijana ambao wamesoma kwa ajili ya upangaji miji, kupima miji na kuendeleza miji. Kwa nini wanashindwa ku–*project* mahitaji ya Tanzania kwa miaka 50 ijayo? Kwa nini wenzetu wanaweza sisi tushindwe? Kuna suala la *commitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa na *commitment* na tukaiweka Tanzania ndani ya mioyo yetu, hatutakuwa sehemu ya kupiga *besenga* kwa kutengeneza mipango mikakati ya kutengeneza mazingira ya kupiga hela ya fidia ili tu ujineemeshe ama ujifaidishe wewe na familia yako. Haya tunayaona na tunayashuhudia kwa sababu wanaofanya hivi ni majirani zetu, ndugu zetu, jamaa zetu, ni lazima ifike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu, bajeti hii imeongezeka na mapato ya makusanyo yameongezeka. Ni vizuri tukatumia *technology* kwa mfano hii *electronic tax system* ili ku–*monitor* uzalishaji lakini pia uuzaji wa bidhaa zetu kutoka viwandani mpaka kwa mlaji. Vile vile tupanue wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato badala ya kutegemea vyanzo vile vile ambavyo tayari vimeshachoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukafanya haya kama tunaweza kuwekeza kwa muda mrefu. Kwa mfano, kama tutatoa *incentives* kwa watu ambao wanajenga majengo kama *National* Husing, Watumishi *Housing* lakini pia *Real Estate Developers* ambao ni *private,* wakajenga *units* nyingi na tukawawekea *tax exemption* maana yake wanaweza wakauza *properties* kwa bei nafuu, watu wakanunua kwa wingi na Serikali ikapata mapato ya uhakika badala ya kuwachomekea kodi katika vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, muda wako umekwisha.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde 30, namalizia tu. Moja ya maeneo ambayo Serikali inawea ikapata mapato ni sehemu ya utalii na kilimo. Tuna *SGR station* pale Kilosa, lakini mtalii akiingia pale kwenda Mikumi atasafiri zaidi ya kilometa 100 za vumbi. Hata hivyo tumekwishazungumzia hili mara nyingi, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hii barabara hii iwe kipaumbele sio tu kwa ajili ya kusafirisha malighafi kwenda kiwanda cha sukari, lakini pia kusafirisha watalii ili tuipe tija na thamani uwekezaji mkubwa wa reli ya mwendokasi pale Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hapa kuna tangazo kwamba, tunaomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge waliohifadhi magari eneo la kuhifadhia magari lililopo karibu na kituo cha afya, waondoe magari hayo ili eneo hilo lifanyiwe maandalizi ya shughuli za Bunge Bonanza.

Pia, tunaomba uwakumbushe Waheshimiwa Wabunge waliomaliza kujaza Dodoso lililoandaliwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu kutoa maoni ya ujenzi wa Ofisi za Jimbo, wakabidhi madodoso hayo wahudumu walioko ukumbini.

Tunaendelea. Nilimwita Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, wakati huo Mheshimiwa Pallangyo, Mheshimiwa Nyamoga na Mheshimiwa Kapufi wanajiandaa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niwe mchangiaji katika bajeti hii ya Serikali. Awali ya yote naomba pia nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha jioni ya leo kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, kama ilivyo ada nami

naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashahidi, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza bayana kwamba pato la Taifa limeongezeka kutoka bilioni 68 hadi 85, jambo hili ni la kujivunia sana. Jambo hili linajidhihirisha kwenye huduma za jamii katika maeneo tunayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashahidi, kwenye Jimbo langu la Nanyumbu, miradi mingi ya maendeleo imefanywa ndani ya miaka hii miwili na mwaka uliokwisha. Kuna miradi mikubwa ya maji; Mradi wa bilioni 3.6 kwenye Kata ya Maratani ambao kwa kweli ni mkombozi wa wananchi wa Jimbo langu. Kuna Mradi mkubwa wa bilioni 3.4 katika Kata ya Sengenya, lakini tuna mradi wa bilioni 40 wa kutoa maji katoka Mto Ruvuma kuleta katika Mji wa Mangaka. Miradi hii ya maji ilikuwa ni kero kwa wananchi na imekuja kukomboa wananchi wa jimbo langu. Namshukuru sana Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mama yetu ameonesha ukomavu, amerudisha demokrasia. Sisi ni mashahidi, leo hii Vyama vya siasa vimeruhusiwa kufanya siasa, jambo ambalo lililkuwa ni ndoto. Vile vile, amerudisha mchakato wa Katiba Mpya, kwa kweli jambo hili jambo hili linatia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya miaka hii miwili tumeona kiwango cha *investment* kilichowekezwa ndani ya nchi yetu, zaidi ya trilioni 23, karibu nusu ya bajeti yetu imeingizwa katika uchumi wetu. Ni jambo la kumshukuru sana Mama amekuwa muungwana, wafadhili na wawekezaji wamekuja kuwekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tuliona zile fedha za *Covid* ambazo kwa busara ameweza kuzitumia katika kujenga shule na miradi ya maji. Ndani ya Jimbo langu nimenufaika na hizi fedha za *Covid* karibu madarasa 68

yalijengwa. Vile vile, mradi wa maji wa bilioni moja ulijengwa ndani ya Jimbo langu na kuondoa kero hii kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pato la mtu mmoja mmoja *(per capita income)* imeongezeka kufikia dola 1,252. Kwa hiyo, kwa haya yote na mengine namshukuru sana Waziri wetu wa Fedha na Naibu wake kwa ushauri mzuri wanaoufanya kwa Mheshimiwa Rais ambayo haya yote leo tunayoyaona yanafanyika ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kidogo kwenye bajeti hii. Tumeona makadirio yetu ya kodi katika mwaka ujao wa fedha ni karibu trilioni 44.3. Makadirio haya ya kodi yanatokana na vyanzo mbalimbali, kuna *direct tax* na *indirect tax,* kwa hiyo hizi kodi ili zikusanywe lazima tuwe na watumishi waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kuna vyanzo vya kodi ambavyo kwenye ripoti ya *CAG* vilileta hoja nyingi sana, ningemwomba Mheshimiwa Waziri aangalie kama kuna uwezekano hebu tubadilishe jinsi ya kukusanya hizi kodi. Mfano, ukiangalia taarifa ya *CAG* hii kodi ya *withholding tax* imekuwa na hoja nyingi. Waajiri wanakusanya *withholding tax at source* lakini hawapeleki *TRA*. Sasa nini matokeo yake? Matokeo yake yule mtu aliyekatwa anapoenda kukadiriwa kule *TRA* inaonekana hajalipa chochote. Kwa hiyo, yule aliyekata ananufaika lakini yule aliyekatwa inakuwa ni tatizo kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwamba, kwa nini tusitumie mabenki kukusanya hizi pesa na kuzipeleka *TRA*? Mwajiri alipe kama ilivyo deni la mhusika lakini benki ndiyo ikate hizi pesa na *at the end of the day* benki anapeleka *TRA* moja kwa moja na mtu anapotaka kujua amelipa kiasi gani anaenda kwenye *website* ya *TRA* ana-*click button* anapata kiasi alichochangia katika ile *final payment* analipa ile tofauti na jambo hili tutaondoa hata kero hoja za ukaguzi ambazo miaka na miaka tunakuwa tunakutana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *direct tax* nyingine ambayo tumekutana nayo ni tumekuwa waagizaji wakubwa wa magari kutoka nje ya nchi, lakini watu wengi wameshindwa kukomboa magari yao kutokana na kodi. Sasa wakati umefika tukubaliane, mtu anapoagiza magari nje ya nchi alipe na kodi moja kwa moja. Kama kodi inajulikana ni shilingi milioni tano gari milioni 30 alipe milioni 35 moja kwa moja. Hii itasaidia sana kupunguza hizi *bonded warehouse* ambazo zinahifadhi magari miaka kumi, miaka 15 mtu hana hela ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo itatusaidia sana, kwanza itarahisisha kukusanya kodi kwa mara moja lakini pili itapunguza mzigo kwa watumishi wa *TRA*. Watumishi wa *TRA* kazi yao itakuwa inakuja tu *paper work* kuangalia hii ndiyo gari uliyoagiza? Hii ndiyo *CC number*? Hii sijui na nini na nini, *at the end of the day* maisha yanakuwa mepesi. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tutarahisisha sana na kukusanya hela kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *indirect tax,* hii pia ni kodi ambayo mwananchi anaweza akalipa bila kujihisi kwamba amelipa kodi, hiki ndiyo chanzo ambacho tukitumie zaidi na zaidi, sasa nilikuwa nimeangalia hapa hawa *ETS* wao wameingiza katika baadhi ya bidhaa ku-*stamp* bidhaa zetu, kwa ku-*stamp* imesaidia sana, kwanza inamtambulisha kwamba hii bidhaa ni ya Tanzania lakini pili inarahisisha kuondoa bidhaa feki, tatu inaweza kujua ni kiasi gani cha kodi ambacho kinaweza kukusanywa kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima tuwatumie hawa katika bidhaa mbalimbali, hebu tuongeze wigo wa bidhaa zetu. Mfano Mheshimiwa Waziri amezungumza kuongeza kodi kwenye vifaa vya ujenzi, badala ya kuongeza kodi hebu tuende kwa utaratibu huu tuone tuki-*stamp* hizi *cement* tunayozalisha je, hatuwezi kukusanya kodi nyingi kuliko kuongezea wananchi kodi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri katika maeneo hayo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho naomba tena nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli Mheshimiwa Waziri

wewe hujioni lakini umekuwa mtu laini sana, unafikika. Kulikuwa na Mawaziri hapa Waziri wa Fedha ananata huwezi kuamini kama huyu ni binadamu, lakini wewe tunakutana wewe Yanga mimi Simba tunachati unaondoka zako maisha yanaendelea, hii imerahisisha watu kukuambia mambo mengi ya msingi. Kwa hiyo, usiache tabia hiyo na wananchi wanakujua unafikika. Sasa kwa kuwa unafikika tunakuomba sasa urahisishe uwezekano wa wananchi kurahisisha maisha yao, kubali hoja zao zifanyie, kazi ndugu yangu Shabiby amesema hoja za wananchi zichukuliwe kama ni changamoto, zifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba tena nishukuru sana Serikali kwa miradi mbalimbali ambayo imeendelea kutekelezwa ndani ya Jimbo langu. Jimbo la Nanyumbu tulikuwa hatujawahi kuona barabara ya lami na taa za barabarani lakini ndani ya Mama Samia tumeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya kusema hayo najua muda siyo rafiki naunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Ally Mhata kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa na Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafsi hii nichangie hii bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2023/2024. Nianze kwanza kwa kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anawafanyia Watanzania, juhudu zake tumeziona katika kujenga Diplomasia ya Uchumi, *Royal Tour* na mambo haya yamefanya nchi yetu sasa imepanda ilikuwa Namba Sita kiuchumi Afrika, tumeondoka kwenye dola bilioni 69.9 mwaka 2021 na sasa tumefikia dola bilioni 85.4 kufika mwezi Aprili, haya ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anategemea sana wasaidizi wake wa karibu na kwa ajili hiyo nichukue nafasi hii

kumpongeza sana Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake Mheshimiwa Chande pia na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Mkuu pale Wizarani wote, hawa wanafanya kazi nzuri, ndiyo wametufikisha hapa tulipo kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na bajeti ya trilioni 44.39 fedha ambazo zinatakiwa zikusanywe na kutumika kwa mwaka huu wa fedha, sina mashaka kwamba hizo fedha zitapatikana kwa sababu nimesoma mikakati ya kuzitafuta lakini pia na mikakati ya usimamizi. Nimpongeze sana Waziri kwa kujipanga sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo za pongezi naomba nizungumze kidogo kwenye Wizara za Kisekta nikianzia kilimo. Wenzangu wamesema kwamba Kilimo kinaajiri Watanzania wengi lakini mchango wake kiuchumi bado uko chini sana. Mimi nipongeze kwa kweli juhudi za Serikali katika kukiboresha na kukiinua kwa kuongeza bajeti kutoka bilioni 294 mwaka juzi sasa tuko bilioni 970 ambazo zimependekezwa hapa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa cha kisasa, kwa maana ya mbegu bora, pembejeo lakini pia na kuhakikisha kwamba tunaachana na kilimo cha kutegemea mvua. Nirudie kusema tena kwamba kwa kweli tutafanikiwa tu kama nchi hii tutaachana na kufanya kilimo cha kukaa na kusubiri mawingu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kule Arusha Meru Tarafa za King’ori na Mbuguni kwa miaka mingi zimekuwa ndiyo kapu la chakula kwa ajili ya Jiji la Arusha na viunga vyake lakini pia hata kwa nchi za Jirani. Lakini sasa hivi Tarafa zile zimeathiriwa sana na mabaliliko ya tabianchi, na kwa hiyo nishauri Serikali ichukue hatua za haraka yajengwe mabwawa kwenye Tarafa hizo na kujenga skimu za umwagiliaji sambamba na kuendelea kutoa mbegu bora na pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani sana miaka ya 1970 kule Kisimiri Juu tulikuwa tunalima Pareto na tulikuwa na Kiwanda cha Pareto kule Arusha, yale mashamba yalifungwa na siku hizi yale mashamba wananchi wanalima bangi. Kwa hiyo, Serikali

imekuwa inahangaika sana kupambana na kilimo cha bangi kule Kisimiri Juu. Ushauri wangu kwa Serikali, tufufue Kilimo cha Pareto kule Kisimiri Juu, hali ya hewa inakubali kwa ajili ya kilimo cha Pareto nina taarifa kwamba Iringa wameanza ujenzi wa Kiwanda cha Pareto kama sijakosea, lakini kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunafufua kile kilimo cha Pareto ili wananchi waachane kilimo cha bangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Serikali imekuja na mipango mingi tu, nimshauri Waziri, kule abeleke hii *program* ya *BBT* zile familia ziunganishwe, wasaidiwe kimtaji na kuhakikisha kwamba hicho Kilimo cha Pareto kinafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mashamba ya maua ambayo yalikuwa yanaongeza sana Pato la Taifa, yalikuwa yanatuingizia fedha nyingi za kigeni. Haya mashamba yamefungwa na wananchi wafanyakazi kule wamebaki wanahangaika kutafuta ajira, lakini pia wamekuwa maskini. Nishauri pia kwamba Serikali ije na mpango wa *BBT* kwenye yale mashamba ya maua, wale watumishi waliokuwa kwenye yale mashamba waunganishwe wachanganywe na vijana, wapewe pesa kazi iendelee na maisha yawe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kupongeza Wizara ya Ujenzi kwa kuja na mpango wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam. Sasa hivi Serikali inajenga *SGR* ambayo tunahakika kabisa kwamba itakuwa na uwezo mkubwa sana wa kubeba mizigo lakini kama bandari ile isingeboreshwa ile Reli ingebakia kama *white elephant,* jambo ambalo lingekuwa si zuri kwa sababu soko la huduma za bandari kwa nchi yetu ni kubwa sana. Bandari ya Dar es Salaam ina soko kubwa sana ya kutoa huduma *landlocked counties* za Malawi, Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Uganda na wakati mwingine Msumbiji. Kwa hiyo, uboreshaji wa ile bandari ni kama ni lazima ifanyike kazi kubwa ya kuiboresha na nashukuru Mungu kwamba Serikali imeshaanza mchakato kwa kusaini mkataba wa *EGA* kati ya Tanzania na Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu nilikuwa na Waziri Mkuu juzi kule Jimboni kwangu alizungumza vizuri sana na kusema

ile kweli alinisaidia sana mimi kama Mbunge kule kwa sababu sitakuwa na kazi kubwa sasa ya kwenda kuelimisha wananchi kuhusu hilo la bandari. Alizungumza alikaa kama Mwalimu akafundisha na watu wote waliomsikiliza waliondoka pale wana amani kwamba kumbe nchi haiuzwi, bandari haiuzwi bali inafanyiwa maboresho ili iweze kufanya kazi *efficiently*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pallangyo na muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa sababu ya muda na mimi naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** nilimuita Mheshimiwa Engineer Ezra Chiwelesa wakati huo Mheshimiwa Nyamoga na Mheshimiwa Kapufi wanajiandaa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji katika hotuba hii ya bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifaya, hasa tuki-*refer* ukurasa wa 29 wa Bajeti ya Serikali, tumeona kwamba wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na vyuo vya kati vya ufundi wakitokea Kidato cha Nne wameondolewa ada, chuo cha *DIT*, Chuo cha *Arusha Tech* na *Mbeya Tech,* kwa hiyo hii inatupatia ma-*technician* na watu wengine wakati wa kuweza kusaidia hasa miradi hii mikubwa inayoendelea katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuanzisha *program* maalum ya mikopo kwa wanafunzi waliochaguliwa kwenda kusomea Vyuo vya Afya na Sayansi, Ufundi na Ualimu. Ni maendeleo makubwa kwa sababu wote Waheshimiwa Wabunge mnaelewa hali ambayo wananchi wamekuwa wanaipitia, ulikuwa ni usumbufu mkubwa sana lakini hii itatusaidia kupiga hatua mbele ili kipindi

tunapata wale wa kada ya juu na hata kada ya kati pia waweze kwenda na sisi tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya ninataka nichangie eneo moja, niki-*refer* ukurasa wa 80 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba acheni Watanzania walipwe pesa nyingi acheni Watanzania watajirike. Nataka nianze na *statement* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Viwanda Biashara, Kilimo na Mifugo na wewe ni Mwenyekiti wangu wa Kamati, tunapotaja biashara sehemu kubwa tumekuwa tuna-*refer* hasa biashara ambayo inafanywa na wazawa. Mimi leo nataka nisimame kwenye habari ya wakandarasi wanaofanya miradi ya ndani. Kwenye hotuba ya CAG 2021 nakumbuka kulikuwa na riba zilizolipwa takribani bilioni 68.7 na wakati nachangia nilisema riba nyingi zinazolipwa, zinalipwa kwa wakandarasi wa nje, kwa sababu wakandarasi wa ndani huwa hatutozi riba. *The moment* mkandarasi wa ndani ametaka kudai riba kinachofuata kesho yake anapoomba kazi hatapewa. Ni haki yake kudai, lakini wale wanaompa kazi wanaona kama anawasababishia hasara, ingawa yeye kwa upande wake anapata hasara kwa sababu mabenki yanamdai na malipo yanavyochelewa analipa *interest* kwenye mabenki lakini anapotaka kudai yeye inaonekana si haki yake. Lakini wanapodai watu wa nje tunahangaika kuwalipa zaidi kwa sababu wao hawahofii kwamba utawanyima kazi kwa sababu wana sehemu nyingine za kupata kazi ila Mtanzania hana sehemu nyingine ya kupata kazi ispokuwa humu humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba kipindi tunatangaza miradi mizuri hii ambayo inakuja na bajeti kubwa ya trilioni 44, bajeti ambayo ina miradi mingi sana ya maendeleo na tukitegemea kwamba Watanzania wanaenda kunufaika huko, na ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais pia alishasema wakandarasi wa ndani wawe *considered* kwenye kazi na kwenye malipo. Sasa tuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakumbuke vijana wenzako wa Kitanzania, watu wengi sana wamechukua mikopo

kwenye mabenki, kwa riba za juu sana asilimia 20 mpaka 22, lakini malipo ya wakandarasi wengi hayajalipwa kwa muda mrefu sana. Sasa wakandarasi wengi wanalalamika, Wabunge wengine wako humu ni wakandarasi na tuko humu tunafanya kazi hizi hali kadhalika tuna madeni makubwa tunadai hatujalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachoomba Mheshimiwa Waziri hili liangalie, kwa sababu kipindi hii miradi unaileta, wenzetu wanafilisika kwenye mabenki, hakuna benki inayouza nyumba unachofanya kila wakati unaomba *extension* ukimwambia hujalipwa na yeye anajua hujalipwa, yeye ana-*extend* lakini yeye anavyo-*extend interest* ya benki haisimami, utajiukuta mtu amefanya mradi wa bilioni moja bilioni mbili au bilioni tatu matokeo yake *interest* benki ameshalipa karibu milioni 500 hana faida tena. Kwa hiyo, tunaomba hili uliangalie ili uweze kuwasaidia wakandarasi wa ndani hatimaye waondokane na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kitu kingine ambacho Mheshimiwa Waziri nataka nishauri, kama inawezekana kuondoa adha hii inayofilisi wakandarasi wa ndani na pia kujikuta tunalipa pesa nyingi sana kwa wakandarasi wa nje kwenye *issue* ya riba. Kwa nini kusiwe na utaratibu maalum wa kuomba vibali kwako wewe kwenye Wizara ya Fedha? Mtu anapotaka kutangaza miradi mikubwa aombe kibali Wizara ya Fedha, mmhakikishie kwamba fedha ipo. Siyo Wizara inatangaza pesa halafu pesa ni mradi ambao unakuja kuomba pesa hazina, matokeo yake anapoomba pesa hazina unajikuta kwamba ile pesa kwako haipo au hujaikusanya, matokeo yake tunaanza kukulaumu wewe, kumbe na wewe hukuwa umetarifiwa wakati ile miradi inatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe kama inawezekana iwepo *procedure* maalum ya kukuomba wewe kibali, utakapo ruhusu Wizara au Taasisi kutangaza maana yake pesa una uhakika nayo ili tusitoze riba kwa wakandarasi wa nje wanaotutoza lakini hali kadhalika wakandarasi wa ndani wasiumie, hilo naomba nimalizie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unakumbuka wiki mbili zilizopita Kamati yako ya Viwanda na Biashara na Kamati ya Bajeti tulikutana kwenye eneo la Wizara ya Kilimo pale, tukiwa na Waziri Bashe na hali kadhalika Waziri wa Viwanda. *TBL* walikuwa wametukaribisha pale wakiwa wanatangaza ufunguzi wa kiwanda chao kipya cha Kilimanjaro *Breweries.* Kiwanda ambacho wamehakikisha kwamba kitatumia shayiri ya ndani kwa asilimia mia kwa ajili ya kufanya uzalishaji wa bia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza mwaka 2021 hapa ndani ya Bunge lako, tulipitisha kushusha *exercise duty* kwa bia ambayo inazalishwa kwa kutumia shayiri ya ndani kwa asilimia 20 tukashusha kutoka 765 kwa lita ikaenda 620. *TBL* wakawa *attracted* kuwekeza kama siku ile ulivyosikia pale, hali kadhalika Waziri Bashe aka-*attract* watu kuwekeza kwenye ngano. Kwa hiyo, tulichokuwa tunategemea ni kwamba *TBL* wangesaidiwa ili ngano hii ambayo wamesema inakwenda kulimwa Makete, ngano inayoenda kulimwa Babati iweze kuwanufaisha Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tunachokiona hapa, ile shayiri ya ndani huyu mtu amemaliza kuwekeza hajaanza kuzalisha anaanza mwakani imeongezeka tena *20 percent* na shayiri ya nje imeongezewa tena 20 percent, inazidi kupanda lakini kwenye kuingiza ngano kutoka nje tunaona ngano ya nje inashushwa *by 35 percent* ninaenda *25 percent,* sasa maana yake ni nini? Huyu aliyekuwa anataka azalishe kwa ngano ya ndani umempandishia halafu anayetoa nje umemshushia, tunaenda kuua hata hawa wakulima ambao juzi tuliambiwa wananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili jambo aliangalie. Unajua unapoongeza wigo hasa kwa watu wanaoweza kuzalishia kwa ndani; kinachotusaidia ni kwamba, tutengeneze ajira za Watanzania walio wengi. Sasa huyu mtu kawekeza, kamaliza hapa tena, kodi zinaongezeka, *extra duty* inaongezeka, halafu *import duty* kwenye ngano ya nje inapungua. Tutakuwa hatujengi, ila tunabomoa. Kwa hiyo, naomba hilo mweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, Mheshimiwa Waziri siku nachangia Wizara yako ya Fedha niliongea habari ya *ETS,* mimi ni mwaka wa tatu sasa unaenda niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, Mwenyekiti wetu huyu hapa anaongoza kikao hiki, hakuna siku wafanyabiashara wamekuatana na sisi bila kuongelea habari ya *ETS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, naomba kwa mara nyingine, Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi ya ku-*rectify* hili tatizo. Hatusemi yule aliyepo aondoke, kwa sababu tayari ameshawekeza muda mrefu, lakini kaa naye uone kama anaweza aka-*adjust price*. Kwa sababu leo ameenda kwenye sukari, ameenda kwenye *cement*. Ina maana tayari wigo wake wa kukuonesha kwamba mapato unayapata wapi, ni mkubwa. Angalia basi, wafanyabiashara wa ndani wasiendelee kulalamika kila wakati, inawaumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it is very bad,* wafanyabiashara wanapokuja wanategemea Bunge liwasaidie na Bunge ni la kwao, lakini wanaona Bunge haliwasaidii, wameenda kwenye Kamati ya Bajeti hawasaidiwi, wamekuja kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara hawasaidiwi, basi tulilete kwa Mheshimiwa Waziri atafute jinsi ya kuwasaidia watu hawa ili tuwe na *balanced state* ambayo itaweza kusababisha wafanyabiashara wafanye vizuri na naye akusanye kodi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri amekuwa muumini wa kusema kwamba unapokuwa na watu wachache uliowabana kwenye kodi haisadii zaidi ya kwamba wao wanaumia. Atengeneze wigo mpana. Wigo mpana ni pamoja na kuwa na hawa watu. Wasipolalamika, watawekeza zaidi, watapanua wigo wa kukusanya kodi, kuliko leo unapokuwa na walipakodi wachache huku ukiwakaba mashati mpaka damu ya mwisho wanaitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda na kwa nafasi hii, naunga mkono hoja. Nina uhakika kwamba Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni msikivu, haya ameyasikia, atayafanyia kazi, hatimaye walipakodi katika mwaka wa

2023/2024 watalipa kodi huku wakiwa wanatabasamu, hatimaye tupate mapato haya ya kufanya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *Engineer* Ezra Chiwelesa kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, wakati huo Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, anajiandaa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya ili niweze kushiriki kuchangia Bajeti kuu. Jambo la kwanza, nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Kilolo kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu na ofisi yake kwa kuwasilisha bajeti nzuri yenye mwelekeo na dira nzuri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza bajeti hii kwa sababu za msingi kabisa. Bajeti ya mwaka jana 2022 ilikuwa na Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya shule za wasichana za mikoa inayojengwa Kilolo. Nina sababu ya kupongeza. Pia kuna kilometa 33 za barabara kutoka Ipogoro mpaka Kilolo, nina sababu ya kupongeza. Vile vile tumesema juzi tu kuhusu *bypass* ya Mlima Kitonga, kilometa 10, usanifu tumeshauona kwenye bajeti ili angalau watu wasikwame pale, tuna sababu ya kupongeza. Pia hii bajeti ina miradi mingi sana kwa ajili ya Kilolo; miradi ya *VETA,* miradi ya maji, ina mabwawa na mambo mengi mbalimbali, lakini na ruzuku ya mbolea na Kilolo ina maeneo mengi ya wakulima, nina sababu ya kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, nami naamini kwamba kwa mwenendo huu nchi yetu inaenda kupata sura mpya ya maendeleo katika uongozi wake. Nami namwombea maisha marefu, Mwenyezi Mungu ambariki ili aendelee kuwatumikia Watanzania katika kipindi ambacho Mwenyezi Mungu amempa nafasi hiyo kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hoja chache ambazo ningependa kuchangia kwenye hii Bajeti Kuu. Jambo la kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kupiga marufuku maduka yasifungwe kwa sababu yoyote ile. Naomba nimwongezee kitu kimoja, naomba atakaposimama pia aagize magari yasikamatwe yanapokuwa yamebeba mizigo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi, mtu anatoka mjini, amenunua vitu vyake, amepakia kwenye gari, ile gari siyo yake, lakini aliyenunua vile vitu hajadai risiti, na yule mtu anaenda anafika, gari inakamatwa. Ile gari ikikamatwa inapelekwa *yard*. Ikipelekwa *yard,* kama ni Ijumaa ni hadi Jumatatu, na huyu mtu ni mfanyabiashara, na gari ile siyo ya yule aliyefanya kosa na aliyefanya kosa anajulikana. Kwa hiyo, huyu mwenye gari anapata hasara kubwa ya kutoendelea na biashara yake kwa sababu ya yule ambaye hakudai risiti. Kwa sababu anayenunua, haendi na mwenye gari dukani, wala hajashiriki hilo kosa la kutokudai risiti. Kwa hiyo, napendekeza kutokufunga maduka kuambatane pia na kutokukamata magari yale yaliobeba mali ili yale magari yaendelee na shughuli zake. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili linalohusiana na mambo yaliowekwa kwenye bajeti hii kuhusu kodi ni suala la faini ile ya kutokudai risiti ile ya Shilingi milioni nne hadi Shilingi milioni tatu. Ni ukweli usiopingika kwamba ile ilikuwa inatengeneza kichaka cha rushwa, kwa sababu kama mimi nina mzigo wa Shilingi 300,000/= na sikudai risiti, hata gari ikipelekwa *yard* siwezi kupata hiyo Shilingi milioni tatu wala milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pale kuna pendekezo la punguzo, lakini Mheshimiwa Waziri naomba wasaidizi wako waangalie lile punguzo vizuri ili liendane na bei ya mzigo huu ambayo sikudai risiti. Huwezi kumdai mtu ambaye hakudai risiti ya shilingi 50,000, umwambie alipe shilingi milioni tatu hadi shilingi milioni nne, kwa sababu hana na kwa hiyo, mara nyingi unafungua milango ya majadiliano tu ya rushwa ili aweze kuondoka na huo mzigo wake. Kwa hiyo, hilo pia ningeomba

niwasilishe kwa namna hiyo kwamba pia liendelee kuangaliwa ili lisiweze kuleta changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependekeza jambo moja kwenye mambo ya kodi, katika kipindi cha hivi karibuni, tulimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwani aliwaagiza *TRA* kuangalia zile kodi ambazo ni za muda mrefu zisiweze kulipwa, lakini kuna tafsiri nyingi sana kwenye hizo kodi za muda mrefu. Pale Iringa kuna mlipakodi mkubwa tu alikuwa anadaiwa kodi ya *VAT* lakini alipoenda akasema hizi zote zimeshasamehewa. Kwa sababu muda mrefu wenyewe yeye alitafsiri labda ni wiki moja, wiki mbili, wiki tatu, mwezi au mwaka. Kwa hiyo, napendekeza ofisi yenu inayo wajibu wa kutoa tafsiri ya huo muda mrefu na aina ya kodi ambazo zimepata huo msamaha ili kusitokee watu wa *TRA* kuwaonea wale ambao hawakupaswa kulipa wamesamehewa, lakini pia wale wanaotakiwa kulipa walipe bila kutumia hiyo kama kivuli cha kujitetea kutokulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda mliangalie ili mlipe tafsiri ya hiyo kauli, pia mpeleke kwa maandishi maelezo *TRA* ili wale vijana wanaosimamia hizo wasijiamulie wenyewe kwamba hii ndiyo iliyofutwa, hii haikufutwa. Kwa hiyo, hilo nafikiri ni vizuri mkaliwekea mkazo na mkaangalia katika utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kikodi, napenda kuzungumzia zaidi hii kwa sababu tunachangia bajeti na ni mapato na matumizi, ni kuhusu kuweka utaratibu mzuri kwenye mazao ya kilimo ambayo hayawezi kuwa na risiti za *EFD*. Kila kitu kimewekwa *EFD,* gari zinazobeba mchanga *EFD* na ukweli hamjasambaza hizo *EFD* kwamba magari yanayosomba michanga huko hayana *EFD* lakini na wao wanadaiwa *EFD*. Sisi tunaotoka kwenye maeneo ya kilimo tunapata shida sana kwa wakulima ambao wanataka kuuza mazao yao, kila siku ni lazima wachukue barua ya Mtendaji wa Kijiji, wapite *TRA* wachukue barua; anakuwa na barua karibu tano, kwa nini? Kwa sababu tu ajieleze kwamba yale mazao ni ya kwake ameyavuna shambani anayapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo usumbufu wa aina hiyo, utengenezeeni utaratibu ambao hausababishi hiyo kero. Pamoja na hizo barua zote, ukifika hapo Migori bado utakamatwa na hadi bei ya rushwa inajulikana, kwamba ukifika pale, ukitoa shilingi 200,000 ndiyo unapita. Kwa hiyo, sasa hii inakuwa pia ni mwanya wa rushwa ambao siyo mzuri. Kama kuna changamoto yoyote, kama ni mbao, kama ni njegere, kama ni viazi tunapopita pale ieleweke, nimetokanavyo shambani. Hata kama hukutokanavyo shambani, ukinunua kwa wakulima, umekusanya, hauna *EFD* na hawajapewa na huwezi ukawagawia wakulima wote *EFD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwekwe utaratibu mzuri ili iwe ni *routine* kwamba upo utaratibu, badala ya sasa hivi ambapo ni uamuzi wa unayemkuta getini kwamba inakuaje? Hiyo inawasumbua wakulima wetu sana, kwa sababu kila siku lazima watakupigia simu, "eeh, nipo hapa getini, leo wamenisumbua." Unaanza tena kupiga simu kwa huyo mtu ili awaruhusu. Sasa hiyo inakuwa ni kero na nafikiri ni vizuri mkiiwekea mkazo ili iweze kutatuliwa na wakulima waweze kusafirisha mazao yao bila shida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi sisemi wasilipe kodi, kama kuna kodi inatakiwa kulipwa, wekeni utaratibu mzuri wajue. Ile rushwa ambayo inatolewa pale, ile Shilingi laki mbili mbili, basi iwekeni angalau basi iwe ni Shilingi laki moja, ipungue nusu, iingie Serikalini badala ya kila siku kuacha Shilingi laki mbili pale kwa mtu. Nafikiri ile ingeweza kuwa ni suluhisho kubwa zaidi kuliko kujua kabisa kwamba nikienda pale ni lazima niwe na shilingi 200,000 na inaenda kwenye mfuko wa mtu. Hilo napenda liwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili ya mwisho, kwenye bajeti zijazo, hebu tuangalie, hiki chanzo cha hewa ya ukaa kimekaaje? Kwa sababu tunaona wawekezaji binafsi, mtu ana hekta 5,000 tu pale Kilolo anapanda miti, analipa watu hela nyingi tu anakuwanazo, huyo ni mwekezaji binafsi. Sisi Kilolo tuna hekta 52,000 za miti ya asili, hatulipwi hata buku na mtu yeyote. Sasa najiuliza, huyu amekuja amepanda hekta 5,000, analipwa hela,

analipa watu 200 wafanyakazi kwenye ardhi yetu, sisi wenye hekta 52,000 hata buku hakuna. Kwa utaratibu upi? Hiyo bado nafikiri Serikali pengine iunde kikosi kazi kifanyie kazi. Hizo nazo ni hela atakuwa anapata, na Mheshimiwa Waziri utapata hela nyingi zaidi, pengine hata kodi nyingine zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Namwita Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, wakati huo Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, wanajiandaa.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mchango wangu utakuwa katika maeneo machache, nikijielekeza katika pongezi, lakini sehemu kubwa itakuwa ni eneo la madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama ilivyo ada, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, lakini nafarijika sana, kuna huu mradi mkubwa wa *TACTIC* mara ya mwisho Serikali imetoa tangazo, naamini kwa maana ya Mji wa Mpanda, Manispaa ya Mpanda tunakwenda kunufaika na mradi huu wa *TACTIC* ambapo tangazo limetolewa. Tuko kwenye awamu ya pili, zaidi ya kilometa 15 za lami zinakwenda kutengenezwa katika Mji wa Mpanda, zaidi ya kilometa 30 kutoka Mwamkulu – Kakese - Misunkumilo, hili ni jambo jema. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenye msukumo wa kuzisukuma fedha hizi kwenda huko, usisite tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kama haitoshi, naiongelee upande wa reli. Tunayo reli yetu kwa maana ya kutoka Kaliua kwenda Mpanda. Kuna zaidi ya Shilingi bilioni 379.3 zinapelekwa huko kuimarisha reli ile. Siyo hilo tu, wanakwenda kutujengea kituo cha kupumzikia abiria cha kisasa katika stesheni yetu ya Mpanda. Mheshimiwa Waziri, katika hili, utakapofika muda wa kuzisukuma fedha huko, naomba naomba sana. Ukanda huu wa kwetu, mkitusaidia kwenye maeneo hayo tutaendelea kujikita kwenye

kusukuma kilimo mazao mbalimbali na kuyaleta kwa walaji huku. Tumebahatika, kwani maeneo yetu yana ardhi nzuri na rutuba nzuri, kwa hiyo, mnapotuletea miundombinu, nasi tunahangaika kuwaleteeni ninyi wenzetu huku ambapo wakati mwingine hali ya hewa ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, nimeona kuna ununuzi wa kandarasi za ujenzi katika maeneo ya meli tatu ikiwa ni pamoja na Ziwa Tanganyika. Naomba sana, Ziwa Tanganyika kama chanzo cha mapato kinachotuunganisha na hizo nchi ikiwa ni Kongo, Burundi au Zambia, kandarasi hii ya ununuzi wa meli kwenye ziwa hilo ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema, naomba sana fedha hizo zielekezwe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema sehemu kubwa nitajielekeza kwenye suala la madini. Naomba sana, najua Serikali inatamani kupata mapato, huko nyuma wachimbaji tuliwahi kuwa na mkutano mkubwa, tukaiomba Serikali kwamba namna pekee ya kuisaidia Serikali, ipunguze utitiri wa tozo na kodi katika eneo la madini. Nami nikueleze Waziri wa Fedha, nakuomba sana, mimi bahati nzuri ni mchimbaji, kwa hiyo, nikiyaongea haya, naongea yale ambayo wakati mwingine tumekuwa tukiyafanya muda wote. Hakuna mtu anakimbia suala la kulipa kodi na vitu vingine vya namna hiyo, lakini nilichokuwa naomba sana, kwanza hebu ziangaliwe kanda tofauti za uchimbaji. Wako wenzetu wa kanda ya mwanza, Shinyanga, wako wenzetu wa Chunya huko, uko ukanda mwingine kama huku kwetu Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukizungumzia kwa mfano dhahabu ya Mpanda, nilikuwa natamani sana, hapa kwenye taarifa yake amepongeza na kusema kuna suala zima la kuongeza thamani na kuthibiti utoroshaji wa rasilimali za madini. Naomba sana, *refinery* sikatai, ni jambo jema na ndipo hapo katika *refinery* amesema, "mtapunguza kutoka asilimia sita kwenda asilimia nne za mrabaha." Ni jambo jema, lakini nilichokuwa naomba, eneo hili pia ikumbukwe kuna mchanga unasafirishwa kwenda nje, hiyo mnayoiita makinikia, lakini kule ndani Mheshimiwa Waziri tujiulize kama sehemu ya mchanga huo

yapo madini ya dhahabu, yapo madini ya fedha, yapo madini ya shaba, Tanzania tunafeli wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa naomba sana, bado iko nafasi ya kuwa na viwanda vya uchanjuaji hapa hapa nchini, kama ambavyo tumesema *refinery* ile inayotengenezwa Mwanza; na hapa mimi nashukuru maana tunaambiwa hata dhahabu sasa hivi itaanza kununuliwa na Serikali, ni jambo jema, lakini nasema bado tuna nafasi ya kufanya uchenjuaji hapa hapa nchini. Kwa sababu kama unabebwa kama mchanga kwenye nje lakini ukumbuke huko ndani mmesema kuna shaba, kuna fedha, ni madini haya, ni chanzo cha mapato, hiki kitu ni vizuri kama kingeongezewa thamani hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi tena kuuliza, lengo ni nini? Dhahabu hii nyingi iliyopo hapa nchini, naomba sana, leo katika maeneo ya uchimbaji yawezekana hawa watu wachimbaji kwa ujumla wake, tukiwapa motisha tukawapunguzia ongezeko hilo la tozo na kodi mbalimbali, kubwa ambao Mheshimiwa Waziri atakutananalo, wachimbaji hawa kwa ujumla wao, wakihangaika ikapatikana dhahabu, kodi mbalimbali atazipata kutokana na hawa watu kufanya manunuzi katika maeneo mbalimbali. Naomba aliangalie hilo, na bahati nzuri wachimbaji inapokuja kwenye matumizi ni watumiaji wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huko ndiko ambako kama ni kwa maana ya kodi tuzipate huko. Ukumbuke dhahabu kama ilivyo, ikibaki ardhini huwezi ukaiona thamani yake. Utakuja kuiona thamani kama imetolewa ardhini ikawekwa hapa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize, zipo nchi hawana hata shimo moja la madini, iwe ni dhahabu au vinginevyo, lakini wametengeneza *refinery*. Unajiuliza wanakusudia wapate dhahabu kutoka wapi? Kwa hiyo, maana yake sisi hapa nchini tulichotakiwa kwanza ni kufungua milango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikupa mfano wa kule kwetu Mpanda, *DRC* Congo siyo mbali. Tukitengeneza mazingira rafiki hapa, ipo nafasi Mheshimiwa ya hata majirani zetu kuleta mali

hapa nyumbani kwetu. Kwa hiyo ni wewe kufungua milango Mheshimiwa. Taabu iko wapi? Nimesema kuna nchi nyingine hawana hata shimo moja la kuchimba dhahabu, lakini wametengeneza viwanda vya kusafisha dhahabu. Unajiuliza, wanapata wapi dhahabu? Sasa kudhibiti utoroshaji, ushauri wangu, eneo hili la tozo mbalimbali wewe Mheshimiwa jipange vizuri. Watu hawa wakipewa motisha kila mmoja huko aliko, hata sisi tunaofanya uchimbaji wa kienyeji huwa tunatoa motisha kwa watu wetu nikiamini wakipata motisha hawa, wataongeza kasi ya kutafuta mali na mali ikipatikana upande wa pili wa Shilingi Serikali nayo inanufaika kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba katika eneo hilo, ukumbuke wachimbaji hawa bado kuna tozo nyingine nyingi. Mfano mtu ana karasha ambalo ni kitendea kazi, anaambiwa alipie, maji alipie. Sasa tozo hizo mbalimbali ukizijumlisha, leo tunataka kwenda karibia zaidi ya asilimia kumi tozo mbalimbali zaidi ya kumi ambapo utashindwa kuiona thamani na mchango wa wachimbaji hawa ambapo naamini kwa kupitia madini ya dhahabu tuna uwezo mkubwa wa kuitoa nchi hapa ilipo ikapiga hatua mbele zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimwita Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali ambayo iko mbele yetu. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako. Lakini nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpa pongezi za dhati Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kupaisha uchumi wa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kukupongeza Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu Dkt. Mwigulu, Naibu Mheshimiwa Chande lakini watendaji wa Wizara na taasisi kupitia Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuweza kukamilisha maono yake kwa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu nianze na pongezi. Napenda nitume pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri ya Morogoro Vijijini na hususani katika Jimbo langu kwenye upande wa afya tumepokea fedha karibu shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga zahanati Gwata, Kisemo, Mgata na Rukulunge katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata vilevile fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya vifaatiba kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya na kwenye zahanati. Nimepata fedha lakini vifaa tiba vya shilingi milioni 751 kwenye halmashauri yetu kwenye Hospitali ya Wilaya. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na hata wale watu wanaosema tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais hakuna sababu yule mtu ambaye anaejua ukipata una kila sababu ya kushukuru na kupongeza. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kupongeza kwa sababu Mama anafanya kazi nzuri lakini na wewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu unafanya kazi nzuri ya kutafuta fedha kwa kumshauri Mama na kuzileta kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru vilevile kuna suala la ajira tumepokea ajira karibu watumishi 33 kwenye halmashauri yetu upande wa kada ya afya. Tuna kila sababu ya kupongeza katika hilo. Ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri na kwenye Serikali ni kwamba pamoja na kazi hii nzuri iliyofanyika kwenye upande wa afya bado tuna changamoto. Changamoto ya kwanza ni gari la wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya lakini vilevile kwenye Kituo cha Afya cha Tutume. Tungeomba Mheshimiwa Waziri katika mapitio pitio yako angalia uwezekano wa kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna changamoto za gari za hospitali kwenye idara ya afya kwa ajili ya kuweza kufuatilia shughuli za uendeshaji wa shughuli za afya lakini vilevile *generator* kwenye Hospitali ya Wilaya hatuna. Lakini vile vile kwenye vituo sita hivi ambavyo nimevizungumza hatuna *generator,* tungeomba tusaidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile majengo ya *OPD* kwenye Kituo cha Afya cha Kisemo, Kisaki pamoja na Kinongo. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri utuangalie. Nitumie nafasi hii vilevile kutoa pongezi za dhati kwenye suala la elimu. Ndani ya kipindi hiki kifupi juzi tu tumeletewa shilingi bilioni tatu ambayo itajenga Shule Maalum ya Wasichana kwenye Kata ya Bwakila Chini ambayo itaanzia *O level* hadi *A level.* Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais lakini tukupongeze wewe Waziri unayefanya kazi kwa dhati katika kufanya kazi hii. Lakini tulipata juzi tena shilingi bilioni 750 kwa ajili ya Mradi wa *Boost* katika kuendeleza shule zile ambazo zilikuwa kongwe. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri lakini vilevile kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali kwa upande wa elimu pamoja na walimu kupatikana tuendelee kupata walimu wengine. Bado tuna upungufu wa walimu kwenye maeneo hasa ya pembezoni kwenye halmashauri yetu, kata za milimani Singisa, Kisaki na kwenye maeneo mengine. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri uone jinsi gani ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwenye hili suala la kufuta ada kwenye vyuo vya ufundi. Nimetokea kwenye vyuo vya ufundi, nimeajiriwa *railway,* nilikwenda kusoma *Railway Training College* mpaka nimemaliza nilipofikia hapa. Sasa kwa kufuta ada kwenye vyuo vya ufundi ambavyo umevitaja *DIT, MUST* na *Arusha Tech* tunaenda kutengeneza wataalamu wengi ambao watakwenda kulisaidia Taifa lakini ombi langu kwako hebu tuviangalie Chuo cha *NIT* nacho tunakokwenda. Tuangalie Chuo cha Reli vilevile

tunakokwenda. Kule nako tunaweza tukasaidia sana vijana wetu wakaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye suala la kilimo niipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya kwenye kuwekeza kwenye kilimo lakini ombi langu kwa Serikali kutokana na tabianchi inavyoendelea uharibifu bado kutegemea kilimo cha mvua hatutaweza kufanikisha katika dhana ya kupata chakula kingi katika nchi kwa faida ya chakula cha ndani na cha kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tuangalie kwenye suala la uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji. Katika yale mabonde mwaka jana nimechangia kwenye Bajeti kuna mabonde pale Kilosa, kuna mabonde hapa tukitoka hapa kuna Kibaigwa, kuna suala la Mto Dumila lakini hata Ruvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie tukachimbe mabwawa, watu wafanye kilimo cha umwagiliaji ili tutoke kwenye lile lakini kwenye suala la kilimo niombe na nadhani Ndugu yangu Bashe yupo. Mwaka huu Morogoro tumebahatika kupata ufuta mwingi sana lakini umeingizwa kwenye suala la stakabadhi ghalani wakati watu hawajajiandaa lakini vile vile hata hiyo Serikali haijajiandaa. Imeleta taharuki na changamoto kubwa. Niwaombe Wizara ya Kilimo hebu kwa mwaka huu tuacheni wananchi walime ufuta wao na wauzie watu wanaowataka ili waondokane na adha ambazo wanazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala lingine Mheshimiwa Waziri nikuombe. Kuna suala la *CSR* la Bwawa la Mwalimu Nyerere. Nakumbuka nilikufuata uliniambia tumtafute Waziri mwenye dhamana hatukuweza kumpata lakini juzi wakati nachangia nilichangia majibu waliyonipa hayakutupa matumaini watu wa Rufiji na watu wa Morogoro Vijijini. Nikuombe wakati unachangia; je, sisi watu wa Morogoro Vijijini ambao na Rufiji ambao ndiyo tunafanya kazi kubwa ya uhifadhi lakini tunafanya kazi kubwa ya kuangalia huo mradi. Je, tunapata nini? Tuelewe ili twende tukapange na tukuleteeni kwamba tusaidieni hiki na hiki na hiki wananchi wetu wapate kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee vilevile kuzungumza kwenye suala la kodi. Mimi ni mfanyabiashara, siyo mkubwa sana lakini ni mfanyabiashara. Bado tuna changamoto kwenye sheria zetu za kodi. Mheshimiwa Waziri unazungumzia suala kwamba hakuna kufunga maduka, hakuna kufunga *account,* Mheshimiwa Rais alisema jambo hili. Mimi ni mhanga, mwaka huu nimefungiwa *account* bila sababu yoyote ya msingi. Niangalie na nikuombe lazima tukae na wafanyabiashara. Kaa na wafanyabiashara katika Sekta mbalimbali wa Kilimo, wafanyabiashara wa mahoteli, wafanyabiashara wakandarasi tuone jinsi gani tunaweza tukachangia wote kwa pamoja tutokaje hapa tulipo ili watu waweze kulipa kodi bila shuruti lakini kodi ambayo itaenda kuleta maendeleo makubwa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya kusema tumefunga, hao watu wa *TRA* kupitia sheria ambazo zimetunga ukifika wanakwambia hayo ni mambo ya siasa na kwa kusema mambo ya siasa kwa kauli yako Waziri maana yake wanakufedhehesha wewe. Lakini vilevile Rais akisema kwamba hili lisifanyike watu wakifanya ukienda wanakwambia ni mambo ya kisiasa vilevile tunamvunga nguvu Rais wetu lakini tunamchonganisha Rais na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kama kuna suala linawapa *mandate* watu wa *TRA* kufunga hizi maduka tuletee hapa tuangalie jinsi gani ya kuifanya tuondoe ili hizi kauli mnazozitoa ziende sambamba na hayo ambayo tunayataka kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikuombe kwenye suala la kupandisha *cement. N*aamini kabisa tutaenda kupeleka maisha magumu kwa Watanzania. Kuna maeneo mengi ya kuangalia na bahati nzuri kuna hili ambalo limezungumzwa *ETS.* Nilishauri siku za nyuma lilipoanza lilikuwa katika maeneo madogo lakini sasa hivi kama alivyotoka hata *Engineer* Chiwelesa kuzungumza limekwenda kwenye *cement* liende kwenye nondo, liende kwenye maeneo mengi tukajihakikishe kwamba kile kinachozalishwa kule je, kinafanana na kile tunachopewa? Tukiweza kujiridhisha matokeo yake nini? Tutaenda kuendelea

kukusanya kodi nyingi ambazo upo uwezekano tusiende tukaingiza gharama kwenye *cement* twende kuingiza gharama kwenye nondo ambazo tutaenda kuwatilia wananchi wetu washindwe kujenga majengo mazuri vilevile washindwe kufanya mambo mengine ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye suala la kodi nakuomba sana, nakuomba sana bado kuna changamoto. Umezungumza mwenyewe wafanyabiashara ni wachache lakini mahitaji ya Serikali ni makubwa. Bado tunaweza kwenda ndani zaidi kutafuta wafanyabiashara wengine ambao watasaidia hawa ambao wamejiandikisha ambao wana mzigo mkubwa na unawaumiza wanashindwa kwenda mbele na mwisho kama tutaendelea hivi hata hawa tuliokuwa nao milioni nne tunaweza tukawapoteza na Serikali ikaingia katika wakati mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris. Nilimwita Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu wakati huo Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani wanajiandaa. Kabla ya Ng'wasi Kamani atachangia Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie lakini nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya hasa ya kupeleka fedha nyingi kule chini kwenye *grassroot* kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie jukwaa hili na nafasi hii kipekee kabisa kuwashukuru sana Watanzania wanaolipa kodi kwenye Taifa letu. Tumeambiwa takwimu zao kwamba ni wachache sana lakini wanabeba mzigo mzima wa watu milioni 61 na sisi tuna walipakodi tumeambiwa walioandikishwa hapa milioni nne na wanaofanya vizuri wapo. Nichukue nafasi hii niwashukuru sana Watanzania mnaolipa kodi kwa ajili ya Taifa letu. Kama unaona kuna mtoto anakwenda shule, kuna hospitali

zinajengwa, kuna barabara zinajengwa ni kwa sababu yako wewe Mtanzania unayelipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hiyo nitoe wito kwa Watanzania wengine na sisi tujisikie wivu kuchangia maendeleo ya Taifa letu. *WHO* wameainisha maeneo ambayo yanaweza yakasababisha tuka-*improve* biashara au tukafanya biashara zetu zifanikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa wanasema lazima tuweke mazingira mazuri kwenye biashara. Hawa Watanzania milioni nne wanaolipa kodi hebu tuwawekee mazingira mazuri tuwaheshimu, tuone kwamba jambo wanalolifanya kwenye Taifa hili ni kubwa sana. Kwanza tunapoweka mazingira mazuri tutaweza kukuza biashara, tutakuza uwekezaji, tutakuza ajira lakini tutajiletea maendeleo ya Taifa letu na wanaendelea kusema kwamba yapo mazingira tunayotakiwa kuongelea ambayo tutatakiwa kuyaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuwe na mazingira huru ya biashara, tuwe na kanuni nzuri rafiki kwa ajili ya wafanyabiashara, tuwe na soko huria lakini tuwe na mipango ya kutafuta masoko mapya na kukuza masoko tuliyonayo. Kubwa zaidi tuwe na mipango ya kuwahakikishia wafanyabiashara mazingira mazuri ya kufanya biashara. Hapo ndipo tutakapoongeza hiyo tunasema *tax base* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea suala la kuongeza au kutanua masoko tumeshaambiwa hapa. Tumeona kazi moja tu ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya ya *Royal Tour,* namna ambavyo imeongeza fursa mpya katika soko letu la utalii ilivyotanua soko letu la utalii na kuvutia utalii. Sasa tunatamani katika hiyo hali na sekta nyingine ziige ili kuweza kupalilia kile ambacho Mheshimiwa Rais amekifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba tunataka kuweka mazingira mazuri, tuongee tu kwenye utalii. Leo watalii wameongezeka lakini watalii wakija kutalii wanapenda wapate huduma stahiki, wanapenda wale bata. Leo watalii wetu

wakiingia Tanzania hata uwezo wa kupata kubadilisha fedha za kigeni ni shida kutokana tu na kutokuwa na maduka ya fedha za kubadilisha yaani maduka ya kubadilisha fedha za kigeni hakuna. Taarifa inasema hapa mpaka Mei, 2023 tayari tuna maduka ya fedha tuliyoyasajili 11. Kule wakati kwenye semina tuliambiwa ni maduka nane yenye matawi 36. Kutoka kwenye *Bureau de Change* tulizokuwa nazo 2019, 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wazungu wakija Iringa hawana kwa kubadilisha dola ili waende wakale bata Ruaha. Sasa wale Mama aliokwenda kuwaita wanakuja, wanakuja huku wanakutana na *broke* hakuna pa kubadilisha fedha za kigeni wanarudi mwaka mwingine? Hayo ndiyo mazingira lakini kilichosababisha ni kutokuwa na kanuni rahisi za kufanya biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naona kwanza kwenye biashara hii kuna ubaguzi. Huwezi kuniambia umewapa watu leseni nane wana matawi 36 nchi nzima. Wenye *capital requirement* ya shilingi bilioni moja moja mmeanza kutubagua Watanzania kwa kuwapa fursa za kufanya biashara kwenye nchi hii watu wenye uwezo wa fedha. Tusio na uwezo wa fedha maana yake tusiwekeze wenye mitaji yetu midogo midogo. Hao mabilionea ndiyo wawekeze. *This is not right!* Lazima Watanzania wapewe fursa sawa ya kufanya biashara, huo ni ubaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujenga imani kwa wafanyabiashara ni pamoja na kauli za viongozi kuzingatiwa. Watanzania wana imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo hii kama Rais atatoa kauli au atatoa maelekezo kwa idara yoyote au Wizara yoyote ya Serikali isipozingatiwa ni kumdharau Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo Watanzania watamwamini nani? Hata Mbunge nikaenda kusema kuna mpango mzuri huu hapa, kama Rais alitoa kauli haikuzingatiwa haikufanyiwa kazi, tunapoteza imani kwa wafanyabiashara kuendelea kuwekeza.

Leo tuliambiwa kodi za miaka mitano Rais kasema miaka mitano ya nyuma, miaka sita zisichajiwe lakini hakuna lolote lililofanyika kwenye Mamlaka zetu kuhakikisha hilo halifanyiki na sana sana ukienda wanasema sisi tunasimamia sheria. Nchi hii Watanzania watamsikiliza nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Rais anapokuja anapotoa maagizo anakuwa ameshafanya *tit for tat* amejua hili linatakiwa mabadiliko ya haraka lakini haya mambo hayafanyiki ndiyo kuweka ugumu kwenye mazingira ya biashara. Watu wanashindwa kutanuka, watu wanashindwa kuwekeza kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ahadi za viongozi zitekelezwe. Mheshimiwa Waziri wa Fedha pale Iringa mwaka jana mwezi wa nane saa hizi tunakaribia mwaka mzima Mheshimiwa Rais alisema na kupitia wewe kinywa chako Mheshimiwa Waziri naongea na Mwenyekiti lakini kwa maelekezo ya Spika kwamba shilingi milioni 700 tutapewa kwa ajili ya kutengeneza mazingira ya machinga. Wale machinga wakiwezeshwa kwenye mazingira yao hayo madogo wata-*graduate* watakuwa wafanyabiashara wakubwa kuja kuungana huku kwenye shilingi milioni nne. Tukiwawekea mazingira saa hizi ya kumaliza mitaji yao na kuua mitaji yao hatutapata wafanyabiashara wengine wanao-*graduate* kuingia shilingi milioni nne. Waongeze idadi ya shilingi milioni nne ifike sita wote wanatakiwa watoke huko kwenye biashara ndogo. Kwa nini tunashindwa kuona umuhimu wa kuwatengenezea mazingira mazuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Waziri amesoma taarifa yake hapa kwamba anaziwezesha benki, *Tanzania Postal Bank* na ile benki nyingine wanazipa mitaji lakini kuna benki nchi hii Mheshimiwa Waziri ni *community banks,* benki ambazo mama ntilie wamechanga hela zao wamepata mtaji wamefungua *community bank* kama *Mkoba Bank* ya Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TRA* mmewachukulia shilingi milioni 600 kutoka kwenye *account* yao kwamba wanadaiwa kodi za miaka hiyo ya nyuma sita, saba huko. Shilingi milioni 600 za

mama ntilie wa nchi hii. Hivi Tanzania sisi huwa hatusamehewi kweli madeni huko na mataifa makubwa? Sisi tunakosa kuwasamehe mama ntilie unakwenda ku-*freeze account* yao, shilingi milioni 600 mama ntilie waliochanga wakaanzisha *community bank* yao kwa mtaji wao Benki ya Mkoba Tawi la *NMB* Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipotengeneza mazingira dunia hii kila nchi inatengeneza *destiny* yake yenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Endelea mchangiaji malizia kwa sababu muda wako umeisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea haya maneno ili wenzetu wayafanyie kazi. Kama benki nyingine unazipa mtaji unaziwezesha, kwa nini *community bank* usizisamehe madeni yao hii ili wale wakinamama waendelee kukopeshana wenyewe? Tusipoangalia tunapigana wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine ni cha mwisho. *TRA* nawaomba sana *TRA* wao ni Watanzania wanapata *mental health* bila sababu za msingi. Wanakuwa hawana afya nzuri za akili bila sababu za msingi wanakuja kustaafu wanakufa mapema bila sababu za msingi. Wanakosa marafiki mitaani bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiajiriwa *TRA* siyo kwamba umepewa kazi ya kutoa roho za watu. Salimia watu tengeneza mazingira mazuri, hawa Watanzania unayekuwa umemnunia unampa hiyo waliyosema Mheshimiwa Nyamoga lazima alipe shilingi 200,000 lazima akulipe wewe shilingi 50,000 ndiye aliyekuajiri, ndiyo anayekulipa hapo mshahara na kodi yako.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** …Kwa nini usimhudumie vizuri umbambikize kodi kwa sababu hajasoma halafu unakuja unasema usipojua sheria siyo sababu ya kutosamehewa sheria? Wewe ulisomeshwa na kodi yake ili umsaidie kumuelimisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe wakati huo Mheshimiwa Francis Isack Mtinga anajiandaa.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii muhimu na adhimu sana. Ni kama mwaka mmoja na nusu nilisimama hapa na nikasema juu ya mambo muhimu ambayo marehemu Hayati Baba yetu Dkt. Magufuli aliyasema kwa ajili ya kufanya Mji wa Mbeya na Mbeya nzima kuwa ni *hub* ya uchumi kwa nchi za Kusini mwa Afrika na katika mambo hayo nilitaja *TAZARA,* nilitaja Bandari ya Nchi Kavu Inyala lakini nikasema pia juu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninafurahi kusema kwamba ninawashukuru sana waliomshauri Mheshimiwa Rais kubuni mfumo wa *EPC+F;* na hao sio wengine ni Waziri wa Fedha ambaye anajua hizi ni kodi za wananchi ambazo zinaenda kulipa, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulipokea hili. Leo Mbeya tunaenda kujivunia barabara ya njia nne, mbili mbili kutoka Igawa mpaka Tunduma, hili si jambo dogo. Ukilisema kwa maneno mepesi ni dogo lakini kwa kweli nataka niseme, Mheshimiwa Rais ametuheshimisha sana Mbeye, ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, tunaenda kupata *bypass* ambayo ina kilometa 48. Ndugu zangu, Tanzania tulizoea ni barabara moja inatoka huko mpaka inakoishia. Sasa kwa mfano mpya tutapata barabara mbili mbili kila upande kilometa

218. Mimi ni nani leo nisimshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan? Nitakuwa nimekosa kibali mbele ya Mwenyezi Mungu. Na mimi nataka niseme, kama kuna watu wataendelea kushukuru kama kuna watu wataendelea kupiga magoti basi mimi nitaendelea. Kama kuna watu wana wivu nikimshukuru Mheshimiwa Rais basi wanywe sumu wajinyonge, sisi tutaendelea kumshukuru. Haiwezekani leo unafanyiwa mambo makubwa kama haya kwa muda mfupi halafu usishukuru, kwani kuna tatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka niseme, pamoja na haya mambo yote ambayo yamefanyika, nataka nikumbushe baadhi ya mambo katika hizo barabara. Barabara zetu zina matatizo makubwa sana, hasa kwa hawa wanaofanya usanifu. Kwanza ni wakatili wakubwa, wanawakatili walemavu, hawataki walemavu watumie barabara. Ninaomba kwenye barabara hizi zinazojengwa waache mambo ya kujenga vighorofa vya kupandia sehemu ambazo ambazo kunatokea *overpass.* Kwa nini msijenge *subway* ambapo hata mlemavu anao uwezo wa kupita, mtu anayetembea kwa mguu atapita? Mnapojenga vile vidude vya kupanda juu zile ngazi mlemavu hawezi kupanda, tuache ukatili. Ninaomba Mheshimiwa Waziri walisimamie hili, fedha ni za wananchi, walemavu ni walipa kodi pia, wapate ku-*enjoy* kwenye barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, inapoijengwa ile barabara, kuna barabara ambayo itakatisha inatoka Uyole kuelekea Kasumulu, tunaenda kufungua bandari. Wewe ni shahidi na wewe umeshuhudia kwamba sasa bandari yetu inaenda kufunguka. Malawi wataitumia sana, hawataenda tena Kusini kule Beila, wataitumia bandari yetu kwa sababu itakuwa *attractive*. Ninachoomba, tunapojenga hizi barabara tukumbuke kwamba kuna barabara inayotoka Uyole kuelekea Kasumulu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo ninaomba niseme jambo moja ambalo ni muhimu. Jambo hili ni la pongezi nyingi kwa Serikali kwa sababu Serikali hii imekuwa Sikivu. Na leo nataka niwasifu Waheshimiwa Mawaziri wawili na niwashukuru.

Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Ashatu Kijaji Waziri wa Viwanda na Biashara. Nawashukuru kwa sababu wamesikia kilio cha Wanakyela kwa kwenda kukomboa soko la zao la cocoa; ninawashukuru sana. Mmefanya kitu kikubwa na wananchi wa Kyela wanamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwakomboa kwa sababu leo wanatoka kwenye utumwa na fedha zinaenda kukaa mifukoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu malipo ya wafanyakazi wa Kiwira Coal Mine. Ninaomba nikumbushe, Mheshimiwa Rais tarehe 7 Agosti, 2022 alipofika Kyela mliahidi kuwalipa. Ninaomba hili lishikiliwe katika kipindi hiki. Hawa wananchi, hadi wengine wamefariki hawajapata hizo fedha. Wameahidiwa muda mrefu zaidi ya miaka 12. Ninaomba wananchi hawa wapate fedha zao na walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kyela kuna eneo linaitwa Ikombe ninaomba, hata kama kwenye bajeti hakuna fedha, hata tunapojenga haya mambo ya barabara kubwa, trilioni 5.7 ni fedha nyingi mno kwa mwaka mmoja. Nimeangalia nchi nyingi nimefunua hakuna nchi ambayo imesaini mikataba na kujenga kilometa 2,035 kwa mpigo, hata Ulaya hakuna. Wakisaini sana ni kilometa 500. Sisi Samia amesaini 2,035; hii ni ajabu, na ukitaka kuweka kwenye maajabu ya dunia hili ni ajabu mojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya haya ninaomba tusiwasahau wale waliopo kule chini. Kuna watu wilayani kwangu Mheshimiwa Waziri hawajawahi kuona barabara wala kuona gari, Kijiji cha Ikombe, wananchi kule wanakufa. Nimesema hapa mara nyingi, sio utani. Mheshimiwa Waziri nilikubeba hapa tukaenda; niliwahi kumbeba Mheshimiwa Mwenyekiti pale, alishuhudia kilio cha wananchi wa Ikombe wakitulilia. Ninakuomba Waziri, niko chini ya miguu yako, ninapiga magoti, twende tuwakomboe wananchi wa Ikombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka nichangie ni juu ya mambo ambayo yanahusu mikanganyiko ya

wafanyabiashara. Ninakuomba sana wafanyabiashara kukitokea tatizo tusiingie kwenye kutoa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako Mheshimiwa.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba dakika nane zimeisha? Hapana ni dakika tatu hizi. Mimi nimehesabu dakika tatu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la *ETS*. Ninaomba sana hili suala ni muhimu hatutakiwi kuliacha, kinachotakiwa ni kuongeza wigo wa kwenda sehemu zingine. Lakini kwa mambo ambayo yanawaudhi wafanyabiashara ninaomba Serikali wafanyabiashara na watoa huduma mkae pamoja muyafanyie kazi haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaomba niishukuru Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa kunipa shilingi bilioni moja kujenga Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, halmashauri ambayo ilikuwa inakaa kwenye majengo ya mkuu wa wilaya, sasa tunaenda kujenga ofisi nashukuru sana Mungu awabariki sana na kwa maneno haya naomba niunge mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe. Nilimwita Mheshimiwa Francis Isaack Mtinga, atafatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mheshimiwa Ngwasi Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii Kuu ya Serikali kwa mwaka 2023/2024. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kuleta maendeleo anayoifanya katika nchi yetu. Niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara. Kazi mnayofanya ni kubwa na Mungu aendelee kuwatia nguvu ya kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa sababu ni sikivu na inasikiliza sana maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge wengi walilalamika juu ya faini za bodaboda na zilipunguzwa kutoka 30,000 mpaka 10,000. Mimi leo nakuja mbele yako kuomba sasa Wizara na Serikali waangalie pia faini zinazochajiwa katika bajaji za mizigo. Bajaji za mizigo zinachajiwa faini ya shilingi 250,000 kwa kukosa stika ya usafirishaji. Hii imekuwa ni kwa sababu bajaji hizi kwenye sheria zimewekwa kwenye *class* moja na malori ya mizigo. Ni kitu cha ajabu sana kuweka kifaa kinachonunuliwa shilingi milioni tano mpaka sita kwenye class moja ya malipo sawa na kifaa kinachonunuliwa zaidi ya milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa *LATRA* alitangaza kwamba sasa watu hawa waanze kuchajiwa faini ya shilingi 25,000 lakini jambo hili halitekelezwi na watendaji wa chini na hii ni kwa sababu ya mapungufu yaliyoko kwenye sheria. Mimi niiombe Serikali kama tulivyosikia kilio cha waendesha bodaboda tusikie kilio cha waenda bajaji za mizigo. Hawa ni vijana wanaotaka kujikomboa, wanaotaka kujikwamua, tuwashike mkono. Shilingi 250,000 ni fedha nyingi tupunguze fedha hii ifike shilingi 25,000 na tu-*reflect* mapungufu haya kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia Serikali kwa sababu ilisikia kilio cha wafanyabiashara hasa wa soko la Kariakoo kwenye kero mbalimbali walizokuwa wanapitia kwenye biashara na mengi yamerekebishwa; mimi niwapongeze sana. Hata hivyo niiombe Serikali yetu, changamoto zilizoelezwa na wafanyabiashara wa Kariakoo ni changamoto ambazo wanazipitia wafanyabiashara sehemu zote nchi nzima. Kero walizozieleza wafanyabiashara wa Kariakoo ni kero ambazo wanazipitia wafanyabiashara *almost* wote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusisubiri wafanyabiashara wa sehemu nyingine pia wagome ili twende tukatatue changamoto hizo. Mimi naomba yale mliyoyafanya kwa wafanyabiashara wa Kariakoo yaende yakafanyike kwa wafanyabiashara wengine wote nchi nzima. Tutoe mafunzo na maelekezo kwa watumishi wetu wa *TRA,* lugha wanazotumia na *approach* wanayotumia

kwa wafanyabiashara wetu si rafiki sana, waende wakarekebishe ili wafanyabiashara na *TRA* waanze kufanya kazi kwa *harmony* na kwa amani kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kati ya vitu ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa anasisitizia ni namna gani ambayo tunaweza tuka-*widen tax base* kwenye nchi yetu ili tusiumize wale wachache wanaoendelea kutuchangia na kutusaidia katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina jambo la kushauri, kuna kitu kinaitwa *carbon credit,* alizungumza Mheshimiwa Kakoso. Wilaya ya Tanganyika peke yake kwa vijiji nane tu inalipwa takribani bilioni nne mpaka tano kwa malipo haya ya *carbon credit*. Sasa hivi dunia inakoelekea *hot topic* ni *climate change,* mabadiliko ya tabianchi; na itaendelea kuwa *hot topic* kwa sababu ndiko tulipo na ndiko tunakoelekea. Sasa, kwa nchi kama za kwetu za uchumi wa chini tutaendelea kuwa wahanga wakubwa wa mabadiliko haya ya tabianchi. Namna gani tunaweza kufaidika na wale wanaochafua mazingira kutusaidia na sisi kuweza ku-*deal* na athari za mabadiliko ya tabianchi ni kupitia hiki kitu kinachoitwa *carbon credit. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hi kuna nchi, nitolee mfano nchi ya Ghana, kwa miezi sita tu kuanzia Juni mpaka Desemba 2019 wamepokea malipo ya dola za kimarekani milioni 4.9 kwa *carbon payment,* miezi sita tu; na wao wamelipwa fedha hizi kwa hekta milioni sita tu za misitu. Takwimu katika nchi yetu zinaonesha kwamba sisi tuna hekta milioni 48 za misitu. Kama tukisema tunaanza ku-*tap* malipo katika *carbon credit* za misitu hii hekta milioni 48 naamini tunakwenda kukusanya fedha nyingi sana. Kuliko kuendelea kuongeza kodi kwa wale walipa kodi wachache kuendelea kuwaumiza kuna namna nyingine ya kuongeza *tax base* kwa kupokea fedha kutoka katika rasilimali ambazo tumeshapewa na Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa kinara wa mfano wa namna gani tunaweza yukaongeza mapato kupitia rasilimali zetu kwenye *Royal Tour.* Sisi twende mbele zaidi, tuunge

mkono juhudi zake, tutumie hizi *carbon credit* kuzalisha mapato kwa ajili ya kuendelea kuleta maendeleo na kukabili matokeo mabaya au matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuchangia katika Bunge hili na nitaendelea kusema; kwamba hatuwatendei haki wakandarasi wazawa wa ndani. Ripoti ya CAG inaonesha kila mwaka kwamba wakandarasi hawa hatuwalipi kwa wakati. Lakini ni uhalisia, hawa watu wako katika majimbo yetu, tuna malalamiko ya kutosha. Lakini kubwa zaidi wale ni vijana wenzangu na hivyo nina jukumu la kuwasemea. Nilisema na nitaendelea kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekwishakutoa maelekezo, tutoe kipaumbele kuwalipa wakandarasi wa ndani. Hawa ni wazalendo, fedha tunazowalipa zinabaki hapa ndani, mzunguko wake unabaki hapa ndani, wanaajiri Watanzania wenzetu. Tusiendelee kufilisi Watanzania wenzetu kwa kuchelewa kuwalipa ilihali hawa watu wana malipo kwenye *commercial banks.* Ninaomba sana Serikali twende tukaangalie suala hili tuwalipe kwa wakati wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mimi niende kwenye fedha za 4:4:2. Ukurasa wa kumi wa bajeti yetu unaonesha kwamba Serikali iko katika mchakato wa kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais, na pale tutakapokuwa tayari kukamilisha utaratibu wa kupitishia fedha hizi benki utakuja kutupa taarifa. Mimi niwapongeze sana kwa hatua ambazo mnaendelea nazo. Nina machache ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wanakwenda kuchukua fedha katika halmashauri zetu, fedha hizi za 4:4:2 hawakujua kwamba benki zipo, walijua; lakini walikwenda kule kwa sababu kuna changamoto kadha wa kadha kwenye kupata fedha kwenye benki zetu. Kuna changamoto za muda, ukiritimba, gharama, kuna rushwa na nyingine nyingi. Mimi niiombe sana Serikali, inapokuwa inaangalia namna gani ya kupitishia fedha hizi tuangalie pia namna ya kuhakikisha kwamba tunatatua

changamoto hizi, ili hawa watu ambao tunataka tuendelee kuwawezesha kiuchumi kupitia sasa kwenye benki zetu tuhakikishe tunaendelea kuwajengea mazingira yaliyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana *issue* ya gharama, kuna gharama kubwa sana na usumbufu mkubwa sana kwa mtu kwenda ku-*apply* mkopo benki. Cha kwanza tusiwaengue maafisa maendeleo moja kwa moja, tuendelee kufanya kazi kwa karibu sana kati ya benki ya maafisa maendeleo. Pili benki sasa tunakwenda kuzipatia mtaji ambao wao hawana hata ile *cost of funds*, tunakwenda kuwaongezea *capital* kupitia hizi fedha za 4:4:2. Niwaombe sasa ikiwezekana zile gharama za mikopo benki wazibebe wenyewe, wasiwabebeshe vijana wanawake wala watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe sana suala la muda, vijana wengi pia hawana dhamana, benki nyingi zinahitaji dhamana, tuliangalie suala hili. Kule kwenye halmashauri zetu walikuwa wanatubeba kwa nafasi zetu kama tulivyo. Leo hii Mheshimiwa Bashe anajaribu kuanzisha *BBT* ili tusaidie vijana kumiliki ardhi tupate dhamana kuingia benki. Sasa niombe sana hizi fedha zinapopitishiwa benki tuwe makini na kale kautaratibu ni jambo zuri, lakini tuhakikishe pia hatuumizi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni zuri, mimi nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ni kweli kulikuwa na changamoto nyingi, *CAG* ameonesha upotevu mkubwa uliokuwa unatokea kwenye halmashauri zetu. Tunaamini fedha hizi zikipita huku zinakuwa na ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe kuwepo na timu za watu ambao wataendelea kuwa-*monitor* hawa vijana. Hata kama wakishapewa hizi fedha waendelee kuwafatilia ili wahakikishe kwamba fedha hizi zinazaa na zinakuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia Mheshimiwa Rais nimpongeze sana na nimshukuru kwa sababu alitenga fedha shilingi bilioni 20 ili kuhakikisha mikoa ya Kanda ya Ziwa inaweza

kunufaika na rasilimali ziliozoko katika Ziwa Victoria. Walikuja watu wa wizarani tuliunda vikundi vya vijana katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Simuyu, Geita na Mara. Vikundi viliundwa vikawa *vetted* tukaandika maandiko, maandiko yakaenda Wizarani, yakapitiwa yakafanyiwa *vetting* watu wa Wizarani wakaja wakatoa mafunzo kwa vijana na mwisho wa siku ikaja *list* ya vikundi ambavyo vime-*qualify* kupata fedha na idadi ya fedha ambayo vikundi hivyo watapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza cha kushangaza tarehe 13 Juni wamekuja tena watumishi wa Wizarani kule Mwanza kuzungumza na vijana; na badala yake wamekuja kutuambia mambo ambayo ni tofauti kabisa na vile tulivyokuwa tumekubaliana. Vikundi hivi vilitakiwa vianze kufuga samaki kwa njia ya vizimba kwenye Ziwa Victoria. Kwenye makubaliano ya Mwanza vikundi hivi kwenye fedha zile milioni 130 kwa kila kikundi, vilitakiwa vipewe vizimba, samaki, chakula pamoja fedha kwa ajili ya kufanya doria na kutunza vile vizimba kwa miezi nane ili baada ya hapo fedha hizi waweze kuzirejesha, na fedha hizi zilikuwa zinapitia *TADB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza wamekuja watumishi wa Wizara kuja kuwaambia vijana kwamba tofauti na walivyokuwa wamekubaliana, kwamba *venders* wa hivi vizimba, chakula cha Samaki na vifaranga itakuwa ni makubaliano kati ya vijana na Wizara; na fedha ile hawatapewa vijana itaenda kulipwa kwa wale *venders* moja kwa moja; na jambo hilo vijana wamekubali. Changamoto inakuja watumishi wa Wizara wamkuja kuwaambia vijana kwamba wao wenyewe ndio watakaochagua *venders.* Wao ndio watachangua *venders* wa vizimba, Samaki, na chakula. Lakini *experience* inatuonesha kwamba watu wengi wameshaanza kufuga Samaki kwa vizimba na wamefeli. Wamefeli kwa sababu ya uduni wa ubora wa vizimba, uduni na udumavu wa vifaranga pamoja na chakula kisicho bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu Wizara wanakuja kutuambia tutafanya haya, kama hamtaki acheni. Je, hii ndiyo lugha ambayo Mama Samia amewatuma kuja kuwaambia vijana? Hii ndiyo lugha ambayo Mama Samia ametoa bilioni 20 ili

vijana waje waambiwe hivyo? Leo hii vipi kuhusu hivi vizimba vikiletwa na havina ubora? Je, vifaranga vikiletwa na vikadumaa au chakula kisicho na ubora. Mikopo hii wanabebeshwa vijana wao ndio walipe, wanalipaje vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka ni kwamba makubaliano ya mwanzo yabaki vilevile. Vijana wakae na kujadiliana *venders* na Wizara ili wale watakaoridhia ndio wapewe *tender* ya kuleta hivyo vitu ili hata mwisho wa siku hivi vitu vikiwa si bora vijana waweze ku-*own* makosa yao na kulipa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia vijana wamekuja kuambiwa na watumishi wa Wizara kwamba hatutalipa tena fedha kwa ajili ya doria, fedha za kujikimu kwa kila kijana kwa hii miezi nane wakati mnafatilia huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea mradi wa miezi nane, vijana wakati wanafatilia mradi huu watakuwa wanatumia nini? tunatishia vijana kuweza kutekeleza miradi hii ili kwenda kutafuta fedha za kujikimu. Lakini fedha hizi hawapewi bure ziko ndani ya mikopo ambayo maandiko ya wizara yalikuwa yameshakubalia kuwapa fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki ni kitu ambacho soko lipo. Mwanza sasa hivi *as we speak* wanaboresha *airport* iwe ya kimataifa. Tuna Daraja la Magufuli ambalo linatusaidia kutoa Samaki kupeleka nchi za jirani. Tuna *SGR* ambayo pia itatusaidia kusafirirsha bidhaa hizi kwa wepesi. Tuna viwanda vingi sana vya minofu ambavyo mpaka sasa malighafi haitoshi. Zao hili tunaloenda kutoa kwenye Ziwa Victoria wala soko lake halina mashaka. Kwa nini Wizara inapata kigugumizi kutoa fedha hizi kwa vijana kama tulivyokuwa tumekubaliana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinasema fedha hizi milioni 130 kwa kila kikundi zimetoka, hizi fedha ambazo Wizara sasa inasema hazitowapa vijana zimeenda wapi? tunahitaji tuambiwe na hii lugha ya kuwaambia vijana kwamba tutafanya hivyo la sivyo kama hamtaki acheni, basi acheni kwa sababu

mnawatengenezea vijana bomu la kuwapa miradi ambayo itashindwa kuwa *sustainable*. Leo hii tunatengeneza vile vizimba vya zaidi ya milioni 60 mpaka 100 kuweka ndani ya Ziwa Victoria halafu unamnyima kijana milioni mbili tatu ya kijikimu ili kukifatilia kile kizimba. Leo hii mtu anatakiwa kukodi boti ya kwenda kufanya doria za ulinzi na kulisha wale Samaki shilingi 60,000 mpaka 80,000 kwa siku ndani ya miezi nane kijana anapata wapi hizi fedha? Atapata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwatengenezee mazingira vijana ya kuonekana wao hawawezi kufanya kazi, tusiwatengenezee mazingira vijana ya kuonekana wao si wasikivu na wala si wachapakazi. Vijana wanayo nia tuwashike mkono na tufate maelekezo kama Mama Samia anavyotaka. Tusimchonganishe Mama na Vijana wake, hatutakubali. Vijana tumemwelewa Mama tutampigia kura kwa nguvu 2025 kwa sababu tunajua chote anachokifanya ni kuhakikisha vijana wa Tanzania tunanufaika na matunda ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitafurahi sana kama Mheshimiwa Waziri akija katika kuhitimisha hoja yake akatupa majibu vijana wa mikoa hii mitano. Kwamba hii *project* itaishia wapi na nini kinaenda kutokea kwenye zile fedha ambazo Wizara imetuambia kwamba haitazileta ilihali tunajua zimetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamani kwa mchango wako, lakini pia na Waheshimiwa Wabunge wote.

Kabla sijahitimisha shughuli za leo ninaomba nisome tangazo moja la wageni; tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ahmed Shabiby ambao ni viongozi wa Jukwaa la Wazalendo Huru kutoka Gairo, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 113 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wamekuja kwa ajili ya kutembelea na kupata mafunzo

Bungeni, karibuni sana wanafunzi ili mpate fursa ya kujifunza juu ya shughuli za Bunge zinavyoendeshwa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 23 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*